@15/-WHAT 0721634274
Scheme, notes, lesson plan Exams Jesma , targeter etc latest

# Yaliyomo


1. USAFI WA KIBINAFSI ..... 1
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ..... 1
Kusikiliza na kujibu ..... 1
B. KUSOMA ..... 3
Ufahamu wa kifungu cha simulizi ..... 3
C. KUANDIKA ..... 8
Viakifishi ..... 8
D. SARUFI ..... 10
Aina za nomino ..... 10
I. Nomino za pekee ..... 10
II. Nomino za kawaida ..... 12
2. LISHE BORA ..... 15
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ..... 15
Kusikiliza kwa kina ..... 15
B. KUSOMA ..... 17
Kusoma kwa mapana ..... 17
C. KUANDIKA ..... 20
Barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko ..... 20
D. SARUFI ..... 23
Aina za nomino ..... 23
I. Nomino za makundi ..... 23
II. Nomino za dhahania ..... 25
3. UHURU WA WANYAMA ..... 29
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ..... 29
Tanzu za Fasihi ..... 29
B. KUSOMA ..... 34
Kusoma kwa kina - Novela ..... 34
C. KUANDIKA ..... 37
Insha za kubuni ..... 37
D. SARUFI ..... 38
Aina za nomino ..... 38
I. Nomino za wingi ..... 38
II. Nomino za vitenzi-jina ..... 39
4. AINA ZA MALIASILI ..... 43
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ..... 43
Nyimbo za watoto na bembelezi ..... 43
B. KUSOMA ..... 46
Kusoma kwa ufasaha ..... 46




KICD Kimeidhinishwa na KICD

C. KUANDIKA ........ 48
Insha za kubuni — Masimulizi ........ 48
D. SARUFI ........ 50
Nyakati ........ 50
5. UNYANYASAJI WA KIJINSIA ........ 55
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 55
Mazungumzo mahususi ........ 55
B. KUSOMA ........ 58
Kusoma kwa ufahamu ........ 58
C. KUANDIKA ........ 61
Insha ya maelekezo ........ 61
D. SARUFI ........ 63
Nyakati na hali ........ 63
6. USALAMA SHULENI ........ 67
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 67
Kusikiliza kwa kufasiri — Matini ........ 67
B. KUSOMA ........ 68
Kusoma kwa kina — Maudhui na dhamira ........ 68
C. KUANDIKA ........ 69
Insha ya masimulizi kutokana na picha ........ 69
D. SARUFI ........ 72
Aina za vitenzi ........ 72
Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi ........ 72
7. KUHUDUMIA JAMII SHULENI ........ 75
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 75
Kusikiliza kwa ufahamu ........ 75
B. KUSOMA ........ 77
Ufupisho ........ 77
C. KUANDIKA ........ 79
Insha ya kubuni — Maelezo ........ 79
D. SARUFI ........ 80
Aina za vitenzi — Vitenzi vishirikishi ........ 80
8. ULANGUZI WA BINADAMU ........ 83
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 83
Kuzungumza ili kupasha habari ........ 83
B. KUSOMA ........ 86
Kusoma kwa kina ........ 86
I. Mandhari ........ 86
II. Ploti ........ 88
C. KUANDIKA ........ 91
Viakifishi — Kiulizi na koma ........ 91

D. SARUFI .......... 93
Ngeli na upatanisho wa kisarufi .......... 93
I. Ngeli ya A-WA .......... 93
II. Ngeli ya U-I .......... 94
9. MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA MAWASILIANO .......... 97
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA .......... 97
Kusikiliza kwa kina .......... 97
B. KUSOMA .......... 98
Ufahamu wa kifungu cha kushawishi .......... 98
C. KUANDIKA .......... 100
Insha za kubuni — Masimulizi .......... 100
D. SARUFI .......... 102
Ngeli na upatanisho wa kisarufi .......... 102
I. Ngeli ya KI-VI .......... 102
II. Ngeli ya LI-YA .......... 104
10. KUJITHAMINI .......... 107
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA .......... 107
I. Nyimbo za kazi .......... 107
II. Nyimbo za dini .......... 109
B. KUSOMA .......... 110
Kusoma kwa kina — Wahusika .......... 110
C. KUANDIKA .......... 112
Barua ya kuomba msamaha .......... 112
D. SARUFI .......... 114
Vinyume vya maneno .......... 114
I. Vinyume vya nomino .......... 114
II. Vinyume vya vivumishi .......... 117
11. MAJUKUMU YA WATOTO .......... 119
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA .......... 119
Kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara .......... 119
B. KUSOMA .......... 121
Kusoma kwa mapana .......... 121
C. KUANDIKA .......... 122
Insha za kubuni — Maelezo .......... 122
D. SARUFI .......... 124
Mnyambuliko wa vitenzi .......... 124
I. Kauli ya kutenda .......... 124
II. Kauli ya kutendea .......... 126
III. Kauli ya kutendwa .......... 127



KICD Kimeidhinishwa na KICD

12. MAGONJWA AMBUKIZI ........ 129
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 129
Kusikiliza kwa makini ........ 129
B. KUSOMA ........ 130
Kusoma kwa ufasaha ........ 130
C. KUANDIKA ........ 131
Hotuba ya kupasha habari ........ 131
D. SARUFI ........ 133
Aina za sentensi ........ 133
I. Sentensi sahili ........ 133
II. Sentensi ambatano ........ 134
13. UTATUZI WA MIZOZO ........ 137
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 137
Wahusika katika nyimbo ........ 137
B. KUSOMA ........ 139
Kusoma kwa kina — Mbinu za lugha ........ 139
C. KUANDIKA ........ 141
Insha za kubuni — Maelezo ........ 141
D. SARUFI ........ 142
Ukanushaji kwa kuzingatia nyakati ........ 142
14. MATUMIZI YA PESA ........ 147
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 147
Lugha katika nyimbo ........ 147
B. KUSOMA ........ 149
Ufahamu wa kifungu cha mjadala ........ 149
C. KUANDIKA ........ 153
Insha ya maelekezo ........ 153
D. SARUFI ........ 154
Ukubwa wa nomino ........ 154
15. MAADILI YA MTU BINAFSI ........ 159
A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA ........ 159
Kusikiliza habari na kujibu ........ 159
B. KUSOMA ........ 160
Ufupisho ........ 160
C. KUANDIKA ........ 162
Kuandika kidijitali — Baruapepe ........ 162
D. SARUFI ........ 164
Usemi halisi na usemi wa taarifa ........ 164

# 1 USAFI WA KIBINAFSI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza na kujibu

### Kichocheo

1. Je, unaposikiliza mtu akizungumza unafaa kufanya nini ili uupate ujumbe kikamilifu?
2. Unapomjibu mtu katika mazungumzo, unazingatia mambo gani ili akuelewe vilivyo?

**Shughuli ya 1:** Vipengele vya kuzingatia katika usikilizaji wa mazungumzo

1. Tazama picha hii:



Simba anazungumza na Mnyama Mgeni



KICD Kimeidhinishwa na KICD

2. Mweleze mwenzako kuhusu picha uliyoitazama. Unaweza kuongozwa na maswali haya:
   (a) Unafikiri ni kwa nini Simba ameshika pua yake?
   (b) Ni ishara gani inayoonyesha kuwa Mnyama Mgeni anamsikiliza Simba kwa makini?
   (c) Unafikiri ni kwa nini Simba wameangaliana ana kwa ana na Mnyama Mgeni?
3. (a) Sikilizeni mazungumzo kati ya Simba na Mnyama Mgeni ambayo mwalimu atawasilisha.
   (b) Taja vitendo ambavyo wanyama walifanya kuonyesha kuwa walikuwa wanasikiliza wakati wa mazungumzo yao.
   (c) Eleza umuhimu wa vitendo vifuatavyo unapomsikiliza mwenzako:
      (i) kusikiliza kwa makini
      (ii) kumtazama mzungumzaji
      (iii) kutikisa kichwa
      (iv) kutumia vihisishi
      (v) kuepuka vizuizi vya mawasiliano.

### Shughuli ya 2: Vipengele vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo

Ukiwa na mwenzako:

1. Jadilini tabia za kinidhamu alizozingatia Mnyama Mgeni wakati wa kumjibu Simba.
2. Mweleze kwa nini ni muhimu kuzingatia tabia zifuatazo wakati wa kumjibu mtu katika mazungumzo:
   (a) kutumia lugha ya adabu
   (b) kutomkata kalima mzungumzaji
   (c) ubadilishanaji zamu ufaao
   (d) kujibu kwa kujikita katika kiini cha swali.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa kuna mambo muhimu ya kuzingatia katika mawasiliano ili kuwe na maelewano. Mambo hayo ni kama vile, kusikiliza kwa makini, kumtazama mzungumzaji, kutikisa kichwa, kutumia vihisishi na kuepuka vizuizi vya mawasiliano.

### Shughuli ya 3: Vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo

1. Mkiwa wawiliwawili, zungumzieni kuhusu usafi wa mwili mkizingatia:
   (a) kusikiliza kwa makini

(b) kumtazama mzungumzaji kwa makini ili upate ishara za uso
(c) kutikisa kichwa ili kuonyesha kukubaliana na kauli
(d) kutumia maneno au vihisishi vya kuhimiza kuendelea kuzungumza kama vile *ehee*!
(e) kuepuka vizuizi vya mazungumzo
(f) kutumia lugha ya adabu
(g) kutomkata kalima mzungumzaji
(h) kubadilishana zamu ifaavyo wakati wa mazungumzo
(i) kujibu kwa kujikita katika kiini cha swali.

**Changamkia**

Igiza mazungumzo ya simu na mwenzako. Zungumzieni kuhusu usafi wa kibinafsi.

### Tembea na majira

Mkiwa katika kikundi:

1. Tumieni vifaa vya kidijitali kama vile simu, tabuleti au kipakatalishi kutafuta na kusikiliza video ya mazungumzo mtandaoni kuhusu usafi wa kibinafsi.
2. Tambueni vipengele vifaavyo vya kusikiliza na kujibu mazungumzo katika video hiyo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Ukiwa na mzazi au mlezi wako, zungumzieni kuhusu namna ya kutunza vifaa vinavyotumika katika usafi wa kibinafsi.
2. Zingatia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo.

## B. KUSOMA

### Ufahamu wa kifungu cha simulizi

### Kichocheo

1. Kwa nini unasoma ufahamu?
2. Je, ni mambo gani yanaweza kukusaidia kupata ujumbe katika kifungu cha ufahamu?

**Shughuli ya 1:** Habari mahususi katika kifungu cha ufahamu

Mkiwa wawiliwawili:

1. Tazameni picha ifuatayo. Zungumzieni kuhusu kinachofanyika. Toeni maelezo kwa zamu.



2. (*a*) **Soma kifungu hiki cha masimulizi kisha ujibu maswali.**

Kito alirauka kuliko kawaida yake. Usingizi ulikuwa umemwishia. Alianza kukurukakara jikoni. Mama yake aliposikia glasi zikigongana jikoni alikwenda kuangalia.

"Kito! Unafanya nini jikoni asubuhi hii? Umenishtua!" Mama alisema kwa hofu.

"Niwie radhi kwa kukushtua. Umesahau kuwa leo ni siku ya sherehe ya kuzaliwa kwangu? Nataka kila kitu kiwe mahali pake wageni wangu wakifika. Nimeanza matayarisho. Nataka kupanga glasi za kunywea

sharubati ziwe tayari. Wageni wakifika kazi itakuwa rahisi sana, ni kuzitoa nje tu," Kito alimwambia mama yake.

"Msafiri ni aliye bandarini. Hata hivyo, unanishangaza sana wewe. Sawa, endelea na matayarisho yako lakini usiwapigie wenzako kelele bado wamelala," Mama alisema kwa tabasamu.

"Asante mama. Nitamakinika ili nisiwapigie wenzangu kelele," Kito alisema kwa upole.

Kito alipanga kila kitu alichotaka, alivyokitaka. Alirudi chumbani mwake kujinadhifisha. Aliingia maliwatoni akaoga kwa maji na sabuni na kupiga mswaki kwa kutumia dawa ya meno. Alijipangusa kwa taulo safi na kujipaka mafuta mwili wote. Alivaa rinda lake la buluu lenye mistari ya kupendeza. Alisimama mbele ya kioo na kujisemea, "Napendeza kweli. Rinda langu limeshika pasi vilivyo. Najua marafiki zangu watashangazwa na jinsi rinda hili lilivyolandana na keki yangu." Kito alichukua kikata kucha na kuangua kucha zake za mikono na miguu. Halafu alichana nywele zake kwa kitana na kuzifunga pamoja nyuma kwa kibanio cheusi. Alipangusa viatu vyake kwa taulo ndogo na kuviweka tayari.

Wageni wa Kito walipoanza kuwasili, Kito alikuwa ametayarisha kila kitu.

"Siku njema huonekana asubuhi. Siku yako itafana Kito. Naupenda moyo wako wa bidii," Baba yake Kito alimwambia binti yake.

"Asante sana baba. Nimebakisha kuweka chakula mezani tu, kisha sherehe yetu ianze. Marafiki zangu watanisaidia," Kito alisema kwa bashasha.

Chakula chote kilipangwa mezani kwenye hema nje ya nyumba yao. Keki pia ililetwa mezani ikiwa ndani ya boksi. Marafiki wake Kito walitaka kuiona keki lakini alidinda kuwaonyesha. Alitaka kuwaweka katika taharuki ili wawe na hamu ya sherehe. Marafiki zake nao pia walidinda kumwonyesha zawadi ambazo walikuwa wamemletea. Nao pia walitaka zifunguliwe tu baada ya keki kukatwa. Hali hii iliwatia wote mshawasha, sherehe ilinoga.

Chakula chote kilipowekwa mezani wageni walikaribishwa. Wakanawa mikono kwa sabuni na maji safi. Kito aligundua kuwa chakula kilikuwa kinapoa. Alikwenda mbio jikoni kumjuza mama yake.

"Usitie shaka. Nimeweka mishumaa spesheli chini ya kila chombo chenye chakula. Mishumaa hii ina vidude vyenye gesi spesheli. Nitawasha moto ili chakula kisipoe," Mama alimwambia Kito.

Watu walipomaliza kunawa mikono walianza kupakua. Kito, mama yake na marafiki wake walisaidia kuwapakulia chakula wageni. Walipokuwa wakiendelea kupakua, Kito alimwona mtoto mchafu sana kwenye lango lao. Alikuwa anachungulia mara kwa mara. Alionekana mwenye njaa na mnyonge. Alivaa mararu. Alitamani sana kumkaribisha katika sherehe yake, lakini alimwogopa.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

"Mama, mama, kuna mtoto anayeonekana mgeni pale kwenye lango kuu. Naomba kumpelekea chakula. Nafikiri ana njaa," Kito alimrai mama yake.

"Usimpelekee chakula nje. Wacha niende kumkaribisha," Mama alimkaribisha mtoto yule na kumshika mkono wakielekea katika hema. Mama na mtoto yule waliingia katika eneo la karamu. Mama alimwelekeza mahali pa kwenda kunawa mikono.

Punde tu ukatokea mlipuko wa sauti 'Puu!' Mlipuko huu ulisikika kwa sauti ya juu sana. Ikawa ni mguu niponye. Kila mtu alitaka kuokoa maisha yake. Moto ulianza kuwaka pale mezani. Watu walikimbia kuchota maji ili kuuzima moto. Wengine walikimbia nje ya lango kuu kwa woga. Mtoto yule mchafu alipoona hivyo alitoa blanketi kwenye gunia lake alilobeba na kukimbia nalo kwenye hema. Aliugubika moto huo kwa blanketi hilo. Moto huo ulizima ghafla. Ilikuwa ni kama muujiza. Watu hawakuamini. Walirudi hapo kwenye hema halahala ili kujionea lililojiri. Hakuna hasara kubwa iliyotokea. Mtoto yule aliyeonekana mchafu alikuwa amewaokolea hali. Watu walimpongeza kwa kuwa na moyo wa simba.

"Unaitwa nani mtoto?" Mama alimuuliza.

"Luna." Mtoto huyo alisema kwa woga.

Baada ya Luna kudadisiwa kwa muda iligunduliwa kuwa alikuwa yatima. Aliishia mtaani baada ya kufiwa na wazazi wake. Watu walimhurumia sana Luna. Kito alidondokwa na chozi la huruma.

Sherehe iliendelea. Kitambaa cha mezani ambacho kilikuwa kimechomeka kiliondolewa na kingine kikatandikwa. Kito alikata keki huku akiimbiwa. Aliwagawia keki watu wote waliokuwa kwenye sherehe. Alipewa zawadi kemkem.

Sherehe ilipokamilika, Luna alielekezwa bafuni kujinadhifisha. Alipotoka bafuni alionekana nadhifu kweli.

(b) **Maswali:**

(i) Kito aliamka lini?
(ii) Sherehe ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa Kito ilifanyika wapi?
(iii) Ni nani aliyezima moto?
(iv) Kwa nini moto ulizimika ulipofunikwa kwa blanketi?
(v) Kito alidumisha usafi wake vipi?

3. Ukiwa na mwenzako, elezeni:

(a) Kito alionyesha kuwa alikuwa na mawazo safi kwa kumtendea Luna kitendo gani?

(b) Luna alifanya kitendo gani kuonyesha kuwa alikuwa na mawazo safi ingawa alionekana mchafu wa mwili?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa ili nidondoe habari muhimu katika kifungu, ninafaa kujibu maswali kama: lini? wapi? nani? nini? na vipi?

## Shughuli ya 2: Jinsi matukio hufuatana katika kifungu cha ufahamu

Yafuatayo ni matukio katika hadithi uliyosoma. Mkiwa katika kikundi, yapangeni matukio haya yanavyofuatana katika kifungu.

1. moto kuwaka
2. wageni kuwasili
3. Kito kupanga glasi
4. Kito kumwona mtoto mchafu
5. keki kuliwa
6. Kito kurauka
7. Luna kuzima moto
8. keki kukatwa
9. mama kumkaribisha Luna
10. Luna kujinadhifisha
11. Kito kupewa zawadi
12. watu kukimbia
13. watu kunawa mikono
14. Luna kuulizwa maswali.

## Shughuli ya 3: Utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu

1. Jibu maswali yafuatayo:
   (a) Uliposoma aya ya kwanza ulifikiri ni nini kingetokea katika kisa hiki? Mweleze mwenzako.
   (b) Je, uliyodhani yangetokea yalitokea ulivyotarajia au yalikuwa tofauti? Mweleze mwenzako.
   (c) Je, unafikiri marafiki wake Kito walimpa zawadi gani?
   (d) Unafikiri moto mezani ulisababishwa na nini?
   (e) Unafikiri Luna alikosa haki gani za kimsingi?

## Shughuli ya 4: Msamiati katika kifungu cha ufahamu

1. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu ulichosoma:
   (a) kujinadhifisha
   (b) taharuki
   (c) kitana
   (d) wakanawa
   (e) kudadisiwa.
2. Eleza maana ya vifungu vya maneno vifuatavyo:
   (a) msafiri ni aliye bandarini
   (b) siku njema huonekana asubuhi

(c) mguu niponye

(d) kuwa na moyo wa simba

(e) kuangua kucha.

### Tembea na majira

1. Mkiwa katika kikundi, someni kifungu mtandaoni kuhusu usafi wa kibinafsi. Jibuni maswali haya:
   (a) Tajeni wahusika katika kifungu mlichosoma.
   (b) Ni mambo gani ambayo wahusika wanafanya ili kudumisha usafi wa kibinafsi?

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako sentensi zifuatazo:
   (a) Nilioga mwili baada ya mazoezi uwanjani.
   (b) Alinawa mikono baada ya kutoka msalani.
   (c) Aliosha kitana chake baada ya kukitumia.
2. Jadili naye maana za maneno yaliyopigiwa mstari.

## C. KUANDIKA

### Viakifishi

### Kichocheo

1. Je, herufi kubwa hutumiwa vipi katika maandishi?
2. Kikomo hutumiwa vipi katika maandishi?

**Shughuli ya 1:** Matumizi ya herufi kubwa na kikomo katika matini

### I. Herufi kubwa

Mkiwa katika kikundi, elezeni matumizi ya herufi kubwa katika sentensi zifuatazo:

1. Kasim amepewa tuzo ya usafi shuleni kwao.
2. Miji ya Nairobi, Mombasa, Kisumu na Nakuru ina idadi kubwa ya watu.
3. Mwalimu Roda na wanachama wa Chama cha Mazingira wamesafisha soko.
4. Mbuga ya wanyama ya Tsavo ni kivutio kikubwa cha watalii.
5. Gugumaji lililovamia Ziwa Victoria sasa linaondolewa.

### II. Kikomo

Mkiwa wawiliwawili:

1. Someni sentensi zifuatazo:
   (a) Mumi alinunua sabuni kwa bei ya shilingi 80.50.

(b) Anwani ya shule yetu ni S.L.P. 18, Ngazini.
(c) Aha! Kumbe mmejiunga na timu ya waogeleaji nchini?
(d) Bw. Kiberenge ni mkulima hodari, amevuna matunda mengi msimu huu.
(e) Nitaondoka saa 12.45 tarehe 22.12.2022 kwenda ughaibuni.

2. Elezeni kikomo kimetumiwa wapi katika sentensi.
3. Jadilini matumizi tofauti ya kikomo.
4. Mkiwa wawiliwawili, someni kifungu kifuatacho kisha mtambue matumizi ya herufi kubwa na kikomo.

Rita alimwambia Kivu, "Usafi wa kibinafsi ni suala nyeti sana. Mtu anastahili kuchukua jukumu la kujisafisha bila kutarajia kukumbushwa wala kushinikizwa." Kivu alikubaliana na Rita. Alisema, "Watu wengi hutoa vijisababu ili wasidumishe usafi wa kibinafsi. Utamsikia mtu mmoja au mwingine akisema, 'Lo! Siogi leo kuna baridi,' ilhali anaweza kupasha maji moto akaoga. Wengine hunuka vinywa kwa sababu wamekosa dawa ya meno. Tukumbuke kuwa kuna mbinu za kiasili za kusafisha meno kama vile kutumia vijiti na mizizi ambayo watu wa kale walitumia. Mbinu hizo bado zinaweza kutumika hata sasa.

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa herufi kubwa hutumika mwanzoni mwa sentensi na kuandikia mianzo ya nomino za pekee.
Vilevile, nimetambua kuwa kikomo ambacho pia huitwa kitone hutumika mwishoni mwa sentensi, kutenga saa na dakika, katika uandishi wa tarehe, kutenga shilingi na senti na katika maneno yaliyofupishwa.

## Shughuli ya 2: Kutumia herufi kubwa na kikomo ipasavyo katika matini

1. Tunga sentensi ukizingatia matumizi ya herufi kubwa. Utaongozwa na maelekezo yafuatayo:
   (a) mwanzoni mwa sentensi
   (b) kuandika nomino za pekee
   (c) maneno yaliyofupishwa
   (d) kuandika tarehe
   (e) kuandika saa.
2. Shirikiana na mwenzako kusahihisha kifungu kifuatacho kwa kuweka herufi kubwa na kikomo ipasavyo.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

Nina aliingia bafuni ili kuoga Aliweka maji yake kwenye beseni na kuvua nguo alijimwagia Maji na kujipaka sabuni Mara alisikia sauti ya paka wake kiki akilia kwa uchungu. Nina alishtuka na kukodoa macho alilia kwa sauti pia naye, "Mama weee!"

Nina alitaka kutoka bafuni mbio lakini hakuweza kuuona mlango sabuni ilikuwa imemwingia Machoni baada ya kukodoa macho.

3. Tunga kifungu daftarini kuhusu usafi wa kibinafsi. Tumia herufi kubwa na kikomo ipasavyo.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu ulichoandika katika shughuli ya 2, swali la 3.
2. Wasambazie wenzako ili wakitolee maoni.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizoandika katika shughuli ya 2, swali la 1.

## D. SARUFI

### Aina za nomino

### I. Nomino za pekee

### Kichocheo

Je, kuna aina gani za nomino?

**Shughuli ya 1:** Matumizi ya nomino za pekee katika matini

1. Mkiwa wawiliwawili, someni kifungu kifuatacho kisha mjibu maswali.

Jina langu ni Mwari. Ninasomea katika shule ya msingi ya Kaloleni. Leo ni siku ya Jumatatu. Mimi ni mwanaskauti. Nimerauka na kujinadhifisha ili niende shuleni kupandisha bendera ya Kenya. Mwanaskauti anatakiwa kuwa kielelezo kizuri kwa kudumisha usafi wa kibinafsi.

Mwezi ujao, tunatarajia kutembelea Msitu wa Kakamega wakati wa likizo yetu. Huko tutaweza kufanya ziara ya mbugani kwa msaada wa maafisa wa Idara ya Ulinzi wa Wanyama Pori. Kesho yake tutazuru Ziwa Victoria ambapo maji ya Mto Yala humiminika.

**Maswali:**

(a) Msimulizi anaitwa nani?

(b) Msimulizi anasomea shule gani?

(c) Msimulizi alipandisha bendera siku gani?
(d) Msimulizi anapandisha bendera ya nchi gani?
(e) Msitu uliotajwa uko wapi?

2. Majibu mliyoyatoa katika swali la 1 ni nomino za aina gani? Mweleze mwenzako.
3. Ukiwa na mwenzako tambueni nomino za pekee katika orodha ifuatayo ya maneno. Ziandikeni kwenye madaftari yenu.

Mwalimu, baba, Melina, Mto Tana, Bahari ya Hindi, Ulaya, Dubai, jijini, shule, chakula, punda, Turkana, mbuzi, mjomba na rais.

4. Soma sentensi hizi. Tambua nomino za pekee na uziandike kwenye daftari lako.
   (a) Nchi ya Tanzania ni ya kwanza katika Afrika Mashariki kuwa na rais wa kike.
   (b) Mji wa Naivasha una vivutio vingi vya watalii.
   (c) Stefano atasafiri kwa ndege siku ya Alhamisi, tarehe tatu mwezi wa pili kwenda kumtembelea dada yake.
   (d) Watu wanaoishi kandokando ya Mto Athi wameshauriwa kupanda miti kwa wingi.
   (e) Ninaweza kuchora ramani ya Afrika.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa nomino za pekee hutaja majina halisi kama vile ya watu, siku, nchi, miezi, Mungu, mito, milima, miji na sikukuu. Nomino hizo huanza kwa herufi kubwa.

## Shughuli ya 2: Aina za nomino za pekee katika matini

1. Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kutaja aina za nomino za pekee zilizotolewa:

| | Aina za nomino za pekee | Mifano ya nomino za pekee |
|---|---|---|
| (a) | | Njeri, Ongeri, Maria, Gonzi |
| (b) | | Eldoret, Lodwar, Garissa, Kilifi, Isiolo |
| (c) | | Kiswahili, Ekegusii, Kimaasai, Kiborana |
| (d) | | Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Ijumaa |


KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | | |
|---|---|---|
| (e) | | Februari, Mei, Oktoba, Novemba |
| (f) | | Msumbiji, Uganda, Afrika Kusini, Sudani Kusini |
| (g) | | Kilimanjaro, Elgon, Evaresti |
| (h) | | Mirihi, Zuhura, Zebaki, Kausi |

2. Tambua aina za nomino za pekee katika sentensi hizi:
   (a) Sayari ya Utaridi iko mbali sana na Dunia.
   (b) Nitafanya mazoezi ya kutosha ili mwezi wa Mei nijiunge na timu ya kandanda shuleni.
   (c) Ninapenda kusoma vitabu vya Kiswahili.
   (d) Tuliimba nyimbo za kizalendo katika sherehe ya Sikukuu ya Mashujaa.
   (e) Ziwa Magadi lina manufaa ya kiuchumi kwetu.
3. Soma kifungu hiki. Tambua aina nne za nomino za pekee zilizotajwa. Ziandike kwenye daftari lako.

> Mama Rehema anaishi karibu na Mto Tana. Kila siku ya Jumatatu hupitia karibu na mto huo akielekea sokoni. Wakati mwingine huwaona na kuwafurahia kima wakicheza kwenye miti kando ya mto huo. Yeye hujisemea kimoyomoyo,
>
> "Mandhari haya yananikumbusha kuwa nchi yetu ya Kenya ina rasilimali nyingi. Tuna Ziwa Elementaita, Mto Ramisi na Mbuga ya Tsavo. Hii ni mifano michache tu. Ni sharti tulinde rasilimali zetu kwa vyovyote vile."

**Shughuli ya 3:** Kutumia nomino za pekee ipasavyo katika matini

1. Tumia nomino za pekee kutunga sentensi tano.
2. Ukiwa na mwenzako:
   (a) Andikeni kifungu kifupi cha maneno kilicho na nomino za pekee.
   (b) Wasomee wenzako darasani kifungu ulichoandika ili watoe maoni yao.

## II. Nomino za kawaida

**Shughuli ya 1:** Matumizi ya nomino za kawaida katika matini

1. (a) Tazama picha hizi:



(b) Taja majina ya vitu unavyoviona kwenye picha.
(c) Andika majina uliyotaja kwenye daftari lako.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa majina ya vitu nilivyotaja ni mifano ya nomino za kawaida. Nomino za kawaida ni majina ya vitu vya kawaida kama vile uwanja, ng'ombe na bendera.

**Shughuli ya 2:** Nomino za kawaida katika matini

1. Chagua nomino za kawaida kati ya maneno yafuatayo:

   wali, Jumapili, sahani, Otieno, kiota, ua, Busia, nyasi, uji, mbwa, samli, nesi, asali, nanasi, uzi, chumvi, chama, Machi, ufuta, mwavuli, simu.

2. Nomino za kawaida ulizochagua zinarejelea vitu gani?

**Shughuli ya 3:** Matumizi ya nomino za kawaida katika sentensi na vifungu

1. Jaza nafasi katika sentensi hizi kwa kutumia nomino za kawaida.
   (a) ____________ waliovaa sare wanapendeza.
   (b) ______________ mweusi ameyaatamia mayai.
   (c) ______________ amempa mgonjwa dawa za kumeza kila asubuhi.
   (d) Rina anasoma ______________chenye kurasa nyingi.
   (e) Abiria walimuonya _________ aliyekuwa akiliendesha gari kwa kasi sana.

2. Jaza nafasi katika kifungu kifuatacho kwa kutumia nomino za kawaida.

   Lelo ni _______ mwenye bidii. Yeye hufuga ____________ , _________ na bata. Juzi alitembelea soko la Chepkazi. Huko aliuza ______________ ya _________. Alipata ______ nyingi. Alinunua ___________ ,___________ , ________ na ________ ili atumie nyumbani.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Changamkia

Ukiwa na mwenzako:

1. Tengenezeni kadi za maneno yafuatayo:

   mtu, baiskeli, ofisi, mawingu, Mola, taifa, Rwanda, Evaresti, Lamu, simu, kadhi, nywele, sinema, bahari, kusini, Ijumaa, Februari, bwawa, mswaki, Kipchoge.

2. Tumieni maneno kwenye kadi mlizotengeneza kutunga vifungu vya maneno vyenye:

   (i) nomino za pekee (ii) nomino za kawaida.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mtajie mzazi au mlezi wako nomino za pekee na za kawaida.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Tatua

Chukulia kuwa una jirani wa rika lako anayeonekana mchafu.
Utamshauri vipi ili azingatie usafi wa kibinafsi?

# 2 LISHE BORA

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza kwa kina

#### Kichocheo

Ni maneno gani unayojua ambayo yana sauti **dh** au **th**? Waeleze wenzako darasani.

**Shughuli ya 1:** Sauti **dh** na **th** katika silabi na maneno

Mkiwa katika kikundi:

1. (a) Sikilizeni silabi zitakazotamkwa na mwalimu au zilizorekodiwa.
   (b) Taja ikiwa silabi uliyoisikia ina sauti **dh** au **th**.
2. (a) Sikiliza maneno utakayotamkiwa na mwalimu au yaliyorekodiwa.
   (b) Taja ikiwa neno ulilosikia lina sauti **dh** au **th**.
3. Sikiliza tena kisha uandike maneno yaliyotamkwa yenye sauti:
   (a) **dh**
   (b) **th**
4. Mkielekezwa na mwalimu, sahihisheni kazi zenu pamoja katika kikundi.

**Shughuli ya 2:** Matamshi ya sauti **dh** na **th** katika silabi na maneno

Mkiwa wawiliwawili:

1. Mtamkie mwenzako naye akutamkie sauti **dh** na **th** katika silabi zifuatazo:
   dha, dhe, dhi, dho, dhu.
   tha, the, thi, tho, thu.
2. (a) Tamka maneno yafuatayo yenye sauti **dh** na **th**:

| | |
|---|---|
| (i) dhamani | thamani |
| (ii) adhiri | athiri |
| (ii) dhibiti | thibiti. |

   (b) Mwambie mwenzako akurekebishe pale ambapo hukutamka ifaavyo.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

3. (a) Nakili daftarini jedwali lifuatalo:

| **Kusikiliza na kuzungumza: Kusikiliza kwa kina** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jina lako: | Umilisi unaotathminiwa (Weka alama ya √ pale inapofaa) | | | | Maoni ya mwalimu |
| | Ninaweza kutambua sauti **dh** na **th** katika silabi na maneno. | | Ninaweza kutamka sauti **dh** na **th** ipasavyo katika silabi na maneno. | | |
| | Ndio | La | Ndio | La | |
| Sauti **dh** | | | | | |
| Sauti **th** | | | | | |
| Sahihi ya mwalimu: | | | | Tarehe: | |

(b) Likamilishe kuonyesha kama uliweza kutambua na kutamka sauti ifaavyo.

(c) Muombe mwalimu akupe maoni yake.

**Shughuli ya 3:** Matumizi ya maneno yenye sauti **dh** na **th** katika sentensi

1. Mkiwa wawiliwawili, tungeni sentensi mkitumia maneno yafuatayo:
   (a) thamini — dhamini
   (b) thakilisha — dhalilisha
   (c) adhiri — athiri
   (d) dhibiti — thibiti
   (e) thumni — madhumuni.

### Changamkia

Mkiwa katika kikundi, undeni vitanzandimi kwa kutumia jozi za maneno zifuatazo:

1. afadhali — tafadhali
2. thelathini — themanini
3. dhahabu — thawabu
4. wadhifa — dhifa
5. theluji — themometa

### Tembea na majira

1. Tumieni kifaa cha kidijitali kuandika vitanzandimi mlivyounda.
2. Mtumieni mwalimu vitanzandimi mlivyounda kwa kutumia kifaa cha kidijitali ili awape maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi kifungu kifuatacho:

> Chakula bora kinathaminiwa sana kila mahali. Thamani ya lishe bora inapatikana katika uwezo wake wa kukinga mwili dhidi ya athari tele. Chakula bora huupa mwili uwezo mkuu wa kudhibiti maradhi kama utapiamlo. Thibitisho zuri ni kula vyakula vyenye ladha kadha wa kadha.

2. Mwombe mzazi au mlezi wako akupe maoni yake kuhusu matamshi yako.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa mapana

#### Kichocheo

1. Ni kitabu gani cha hadithi ulichosoma kikakufurahisha zaidi?
2. Wasimulie wenzako katika kikundi kisa ulichowahi kusoma.

**Shughuli ya 1:** Msamiati katika matini

1. Chagua matini kutoka maktabani au kwenye mitandao salama ili uisome.
2. Soma matini uliyoichagua.
3. Baada ya kusoma matini:
   (a) Nakili daftarini maneno yoyote ambayo huelewi maana yake.
   (b) Tumia kamusi au mtandao kutafuta maana ya maneno hayo. Unaweza pia kufikiria maana ya neno kulingana na muktadha wa jinsi lilivyotumiwa.
   (c) Andika maana za maneno hayo daftarini.

**Shughuli ya 2:** Kutumia msamiati kutoka kwenye matini

Katika kikundi:

1. Tunga sentensi daftarini ukitumia msamiati uliojifunza kutoka kwenye matini uliyosoma.
2. Wape wenzako sentensi ulizotunga ili wazisome nawe usome zao.
3. Toeni maoni yenu kuhusu sentensi hizo.
4. Sahihisheni sentensi hizo pamoja. Pateni ushauri wa mwalimu.

**Shughuli ya 3:** Ujumbe wa matini

Mkiwa wawiliwawili:

1. Jadili na mwenzako kichwa cha matini uliyosoma.
2. Mweleze mwenzako ujumbe uliopata kutokana na matini uliyoisoma.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

## Shughuli ya 4: Muhtasari

Katika kikundi:

1. Andika muhtasari wa uliyoyasoma.
2. Wasilisha kwa wenzako muhtasari ulioandika.
3. Waulize wakupe maoni yao kuhusu uliyowaeleza.
4. Wape nafasi wenzako wakusimulie waliyoyasoma.
5. Wape maoni yako kuhusu kazi zao.

## Shughuli ya 5: Kuweka rekodi

1. Chora jedwali linalofuata kwenye kijitabu maalumu. Kiite kijitabu hicho Jarida langu. Kila ukisoma hadithi au makala, fungua ukurasa mpya na kuchora rekodi hii kisha uijaze ili kuweka rekodi ya mambo au hadithi uliyosoma.

Jarida langu

| | |
|---|---|
| Shule | |
| Jina | |
| Gredi | |
| Tarehe | |
| Anwani ya matini niliyosoma | |
| Ujumbe niliopata | |
| Maoni ya wanafunzi wenzangu | |
| Hisia au maoni yangu | |
| Maoni ya mwalimu | |

2. Mpe mwalimu jarida lako ulilojaza ili atoe maoni yake.

## Changamkia

1. Tazama kwa makini picha zifuatazo:




2. Jadili na mwenzako mambo yanayohusu kusoma kwa mapana unayoyaona katika picha 1(a) hadi 1(c).
3. Andikeni shughuli za kusoma kwa mapana zinazojitokeza katika picha 1(a) hadi 1(c).
4. Jadili na mwenzako unachopenda kusoma ili kupata habari zaidi.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Tembea na majira

1. Ukielekezwa na mwalimu, tafuta matini inayohusu lishe bora mtandaoni ili uisome.
2. Waeleze wenzako darasani kuhusu uliyoyasoma.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mweleze mzazi au mlezi wako kuhusu uliyoyasoma mtandaoni.
2. Mwombe mzazi au mlezi wako akupe maoni yake.

## C. KUANDIKA

### Barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko

### Kichocheo

1. Je, ni shughuli gani ambayo inaweza kukufanya umwandikie rafiki yako barua ya kutoa mwaliko?
2. Ni mambo gani unayozingatia unapoandaa vidokezo vya barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko? Mweleze mwenzako.

**Shughuli ya 1:** Umuhimu wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko

Ukiwa na wenzako katika kikundi, elezeni umuhimu wa barua ya kirafiki ya mwaliko.

**Shughuli ya 2:** Ujumbe wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko

1. (*a*) Ukiwa na mwenzako, soma barua ya kirafiki ifuatayo:

S.L.P. 98 -10100,
MUTHINGA.
22.12.2022

Kwa dada yangu mpendwa,

Pokea salamu nyingi kama mchanga wa baharini kutoka kwangu. Dada yetu Pendo, mama na baba wote wanakusalimu na kuzidi kukuombea mema.

Je, u hali gani? Ni matumaini yangu kuwa u mzima kama kigongo. Sisi huku nyumbani tunashukuru kuwa hatujambo. Dada Pendo anaendelea vizuri masomoni. Mwaka ujao ataingia Gredi ya Sita. Dada amejifunza mengi shuleni. Hivi sasa anaweza kusimulia hadithi mbalimbali na kuandika visa vya kuvutia. Huwa anafua nguo zake mwenyewe. Mama humsaidia tu kuzipiga pasi. Mama na baba wanaendelea na kazi zao za ukulima. Msimu huu mvua ilinyesha vizuri na mazao yanaendelea kunawiri shambani. Tunatarajia mavuno kochokocho.

Lengo la kukuandikia barua hii ni kukujulia hali na vilevile kukualika kwenye sherehe ya kuadhimisha siku yangu ya kuzaliwa. Sherehe yenyewe itakuwa tarehe 2.1. 2023. Itaandaliwa jioni baada ya shughuli za siku.

Siku hiyo tumepanga kuwa na dhifa murua. Tumeamua kuwa tutaandaa matunda mbalimbali kama matufaha, maparachichi, matikitimaji na ndizi. Hali kadhalika, kutakuwepo na samaki, nyama, maharagwe, njugu na pojo. Isitoshe, ugali, wali, viazi na chapati vitakuwepo kwa wingi. Vinywaji kama maji na sharubati pia vitakuwepo kwa wingi.

Dada, nakuomba ukubali kuongoza shughuli ya ukataji keki siku hiyo. Tafadhali usikose kufika ili tuonane, tujumuike pamoja na tufurahie siku hii muhimu.

Nilitaka upate barua hii haraka iwezekanavyo. Baba ameniruhusu kutumia simu yake. Nimeipiga picha barua hii nikakutumia kwa mtandao wa 'WhatsApp' badala ya kuituma kwa posta. Nitafurahi iwapo utaweza kunijibu kwa njia ii hii kupitia simu ya baba.

Ni mimi ndugu yako mpendwa,
Karani Karamu.

**Swali:**

2. Mweleze mwenzako ni ujumbe gani wa mwaliko ambao Karani anampa dada yake katika barua ya kirafiki uliyosoma.

**Shughuli ya 3:** Vipengele vya kimuundo vya barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko

1. Chora muundo wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko uliyosoma ukizingatia vipengele vifuatavyo:
   (a) anwani
   (b) tarehe
   (c) mtajo
   (d) mwili wa barua
   (e) hitimisho.
2. Jadilini yaliyomo katika kila kipengele cha barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko.

**Shughuli ya 4:** Kuandika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko

1. Ukiwa na mwenzako, jadilini matumizi ya lugha katika barua mliyosoma. Mnaweza kuongozwa na maswali haya:
   (a) Je, ni maneno gani yanayoonyesha:
      (i) Uhusiano wa karibu kati ya watu waliotajwa?
      (ii) Heshima na upole?
      (iii) Ukarimu?
      (iv) Ushirikiano?
   (b) Unakusudia kuandaa karamu ya kusherehekea kujiunga na shule ya upili. Sherehe yenyewe itafanyika wakati wa likizo ijayo. Sherehe itahusisha watu wachache tu. Unakusudia kumwalika rafiki yako. Andika barua


KICD Kimeidhinishwa na KICD

kumwalika kuhudhuria sherehe hiyo. Hakikisha umezingatia mambo yafuatayo:

| Mambo ya kuzingatia | Weka alama ya √ ikiwa umezingatia |
|---|---|
| Anwani yako | |
| Tarehe | |
| Mtajo | |
| Maamkuzi | |
| Ujumbe | |
| Lugha ya adabu | |
| Sarufi sahihi | |
| Hijai sahihi | |
| Hati nadhifu | |
| Tamati | |
| Jina lako | |

3. Ukiwa na mwenzako, someni barua uliyoandika na mrekebishe makosa mtakayogundua.
4. Andika nakala safi ya barua baada ya kuirekebisha.
5. Ihifadhi kwenye potifolio kisha umpe mwalimu aisahihishe.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kupiga picha barua ya mwaliko uliyoandika.
2. Mtumie mwalimu wako wa Kiswahili kwa kutumia mtandao kama vile *WhatsApp*.
3. Muombe mwalimu aisome kisha akupe maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwonyeshe mzazi au mlezi barua ya kirafiki uliyoandika katika shughuli ya 4.
2. Msomee barua hiyo.
3. Muombe akupe maoni yake kuhusu ujumbe wa barua yako.

## D. SARUFI

### Aina za nomino

### I. Nomino za makundi

**Kichocheo**

Je, ni vitu gani unavyojua ambavyo vinapatikana katika mafungu au vikundi katika mazingira yako?

**Shughuli ya 1:** Nomino za makundi

Mkiwa wawiliwawili:

1. Tazameni picha zinazofuata:


(a) fungu la maembe


(b) bunda la noti


(c) shada la maua


(d) thurea ya nyota


(e) chane ya ndizi


(f) shehena ya mizigo


(g) baraza la wazee


(h) mtumba wa nguo


(i) msitu wa miti



KICD Kimeidhinishwa na KICD

2. Someni majina ya vitu vinavyopatikana katika mafungu kwenye picha hizi.
3. Nomino zinazopatikana katika mafungu huitwa nomino gani? Mweleze mwenzako.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa nomino za makundi hutaja vitu vingi vilivyo pamoja kama kitu kimoja. Vitu hivi hujitokeza katika kundi au fungu. Mifano ni kama vile; fungu la maembe, bunda la noti au shada la maua.

4. Nakili kifungu kifuatacho daftarini kisha upigie mstari nomino tano za makundi zilizotumika.

Mama alichukua bunda la noti akaenda sokoni. Ilimchukua muda mrefu kufika sokoni kutokana na mlolongo wa magari barabarani.

Hatimaye alipofika sokoni, alikuta soko limejaa umati wa watu waliokuwa wamehudhuria mkutano wa Gavana. Gavana alikuwa anawazungumzia watu kuhusiana na udumishaji wa usafi sokoni.

Baadaye, mama alinunua mkungu wa ndizi na kurudi nyumbani. Alipofika nyumbani, alichukua kuni chache kutoka kwenye tita la kuni lililokuwa nyuma ya nyumba. Aliingia jikoni na kuanza kupika.

## Shughuli ya 2: Matumizi ya nomino za makundi

1. Ukiwa na mwenzako, kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchagua nomino sahihi kwenye orodha:

| | |
|---|---|
| **mkururo** | **baraza** |
| **shungi** | **mlolongo** |
| **tita** | **bodi** |
| **umati** | **kicha** |
| **genge** | **biwi** |

(a) Sokoni palikuwa na ______________ cha mboga.

(b) Askari walikamata ______________ la majambazi lililohatarisha usalama wa raia.

(c) ______________ wa siafu ulielekea shimoni.

(d) Tuliona ____________________ wa magari wa maafisa wa afya waliokuwa wakihamasisha umma kuhusu lishe bora.

(e) Rais alizungumzia ________________ la mawaziri.

(f) Mzazi wake ni mwanachama wa ________________ ya wasimamizi wa shule.

(g) Lufi alijiandaa kufua ________________ la nguo chafu.

(h) Wazoaji taka wameondoa ______________la takataka uwanjani.

(i) ____________________ la nywele la Bi. arusi lina ua maridadi.

(j) Karamu ilihudhuriwa na ________________ wa watu.

2. Ukiwa na mwenzako, tunga sentensi ukitumia nomino za makundi zifuatazo:
   (a) mtungo wa samaki
   (b) hadhira ya watazamaji
   (c) safu ya milima
   (d) kundi la ng'ombe
   (e) kidimbwi cha maji.
3. (a) Andika aya moja kuhusu lishe bora ukitumia angalau nomino mbili za makundi.

   (b) Ukiwa na mwenzako, sahihisheni aya mlizoandika.

## II. Nomino za dhahania

### Kichocheo

Ni nomino gani zinazotaja hali au vitu vya kufikirika tu?

**Shughuli ya 1:** Nomino za dhahania

Mkiwa wawiliwawili:

1 (a) Someni nomino zilizo kwenye chati.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | |
|---|---|
| **usingizi** | **utandawazi** |
| **furaha** | **wema** |
| **shibe** | **ualimu** |
| **elimu** | **maendeleo** |
| **maisha** | **huzuni** |
| **mapenzi** | **njaa** |

(b) Je, umegundua nini kuhusu nomino hizi ukirejelea uwezekano wa kuonekana kwa macho au kushikika kwa mikono? Mweleze mwenzako.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa nomino za dhahania ni majina ya vitu visivyoweza kuonekana au kushikika kwa mikono. Ni majina ya vitu ambavyo ni vya kufikirika tu.

2. Chagua nomino za dhahania kati ya nomino zilizo katika kapu la maneno lifuatalo:




**Shughuli ya 2:** Kutumia nomino za dhahania

Mkiwa wawiliwawili:

1. Tungeni sentensi mkitumia nomino zifuatazo:
   (a) umoja
   (b) upendo
   (c) amani
   (d) uwajibikaji
   (e) maumivu.
2. (a) Andika aya moja kuhusu lishe bora ukitumia nomino za dhahania.
   (b) Ukiwa na mwenzako, sahihisha aya uliyoiandika.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Changamkia

1. Ukiwa na mwenzako, fanyeni mchezo ambapo mmoja anataja neno la sehemu ya nomino ya makundi na kisha mwenzake anataja maneno yatakayokamilisha nomino ya makundi inayolengwa. Kwa mfano, mmoja akitaja *shada*, mwenzake anasema *la maua*. Fanyeni hivi kwa zamu.
2. Mkiwa katika kikundi, tajeni nomino za dhahania mzijuazo mmojammoja kwa zamu. Wanafunzi wengine katika kikundi waseme ikiwa aliyetaja ametaja nomino sahihi ya dhahania au la.

### Tembea na majira

Katika kikundi:

1. Tumieni kifaa cha kidijitali kutafuta nomino za makundi na za dhahania kwenye mtandao.
2. Andikeni nomino hizo kwenye chati. Chati moja iwe ya nomino za makundi na chati nyingine iwe ya nomino za dhahania.
3. Bandikeni chati hizo darasani ili wanafunzi wengine wawape maoni yao.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mtajie mzazi au mlezi nomino za makundi na za dhahania ukirejelea mazingira ya nyumbani. Mwombe akupe maoni yake.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

# 3 UHURU WA WANYAMA

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Tanzu za fasihi

**Kichocheo**

1. Je, umewahi kusimuliwa hadithi gani?
2. Je, umewahi kusoma tungo gani?

**Shughuli ya 1:** Fasihi ni nini?

1. Mkiwa katika kikundi, jadilini mambo mnayoyaona kwenye picha zifuatazo:



(a)



KICD Kimeidhinishwa na KICD


Ninatangaza uhuru,
kwa wanyama wa
mwituni, Naonya
tunapozuru,
tusiwatishe mbugani.
Haki zao na uhuru,
wanyama wote wapeni,
Ni kosa kubwa kudhuru,
wanyama wetu nyumbani.
(b)


Kitabu Cha
Hadithi
(c)




2. Mkiwa wawiliwawili, someni mazungumzo yafuatayo kati ya mwalimu na mwanafunzi:

**Mwalimu:** Je, unaweza kueleza nini kuhusu picha mlizozijadili?

**Mwanafunzi:** Katika picha mna wachezaji wa nyimbo za kitamaduni na wanafunzi wanaokariri shairi. Tumeona picha ya kobe na sungura wakisoma kitabu cha hadithi. Picha ya mwisho inaonyesha nyanya akiwasimulia watoto hadithi.

**Mwalimu:** Kweli kabisa mwanafunzi. Hii ni mifano ya fasihi ya jamii zetu.

**Mwanafunzi:** Mwalimu, kwa hivyo fasihi ni kama nyimbo, mashairi na hadithi?

**Mwalimu:** Aha! Fasihi ni ufundi unaotumia lugha kwa ubunifu kueleza kuhusu jamii. Fasihi ikisimuliwa huitwa **fasihi simulizi**. Ikiandikwa huitwa **fasihi andishi**.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa fasihi ni kazi inayotumia lugha na ishara kwa ubunifu ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 2:** Sifa za tanzu za fasihi

1. (a) **Soma hadithi ifuatayo:**



Mkutano wa wanyama

Siku moja adhuhuri wanyama walifanya mkutano. Mkutano wenyewe ulihudhuriwa na wanyama wa kufugwa na wale wa porini. Pundamilia alisafisha koo kisha akawakaribisha wote waliofika. Mkutano huo uliitishwa ili kujadili uhuru wa wanyama.

Ng'ombe aliomba kutoa maoni yake. Alitoa malalamishi yake dhidi ya binadamu. Alisema kuwa licha ya kumpa maziwa mwanadamu, kuna wakati angekosa kupewa chakula bora. Si hayo tu. Ng'ombe aliendelea kulalamika kuwa alilala sakafuni ambayo ilijaa matope. Wakati mwingine angepigwa mijeledi. Alimwomba Pundamilia kufikisha malalamishi yake kwa binadamu. Mbuzi na Kondoo walisema walipitia shida sawa na za Ng'ombe.

Twiga alisema kuwa hakuwa na raha tena porini. Mahali pake pa malisho palijengwa hoteli mbalimbali za kifahari. Alilazimika kuhamahama kila ujenzi wa hoteli kama hizo ulipofanyika. Aliwauliza wanyama wenzake, "Je, mwanadamu akimaliza kujenga humu mwangu porini anatarajia mimi nitaishi mjini kwenye ghorofa?"



KICD Kimeidhinishwa na KICD

Pundamilia alimwona Swara amejiinamia kwa huzuni. Akamuuliza, "Ndugu Swara unaonekana kuhuzunika. Nini chanzo cha huzuni yako?" Swara alitikisa kichwa kama ambaye alitaka mawazo yake kujipanga akilini. Alisema huzuni yake ilitokana na namna yeye na Swara wengine wanavyowindwa na mwanadamu. Alisikitika kuwa ati wanawindwa ndipo mwanadamu apate kitoweo. Vilevile, ngozi za Swara zilihitajika kushonea mikoba na kutengenezea ngoma.

Pundamilia alisema, "Wanyama wenzangu, ni jukumu letu kuhudhuria na kujadili uhuru wetu kama tulivyofanya leo. Nitafikisha ujumbe huu kwa mwanadamu. Ni matumaini yangu kuwa akijua tumeanza kukutana atakoma kututusi, kutupiga na kutuwinda. Tena, mnaoishi naye atawaweka katika mazingira safi." Mkutano ulimalizika na kila mnyama kurudi alikotoka.

Wanyama waliona mabadiliko makubwa maishani mwao. Walifurahia uhuru wao waliokuwa wameukosa kwa miaka mingi.

(b) Msikilize mwalimu akikusimulia hadithi.

(c) Mweleze mwenzako tofauti kati ya hadithi ya kusoma na hadithi ya kusimuliwa.

2. Mkiwa katika vikundi, jadilini sifa za fasihi simulizi na zile za fasihi andishi.

**Shughuli ya 3:** Aina za tungo za fasihi simulizi na fasihi andishi katika matini

1. Igizeni mazungumzo kati ya Ngamia na Ng'ombe.

(*Ngamia na Ng'ombe wamekutana. Urafiki wao umekuwa wa chanda na pete. Leo wanashiriki mazungumzo. Wako chini ya mbuyu.)*

**Ngamia:** Ndugu Ng'ombe, naona hali ya anga ni shwari.

**Ng'ombe:** *(Akiangalia juu)* Kweli muhibu wangu. Joto si jingi kama wiki jana tulipokutana. Kwetu tuna msemo kuwa jana si leo.

**Ngamia:** *(Akionyesha kufurahia usemi wa Ng'ombe)* Wakati kama huu ndio mimi hujikuta nikiimba nyimbo za furaha. Sikiliza kipande hiki:

*Jua zuri x2, angaza*
*Upepo mzuri x2, vuma*
*Wanyama kwa pamoja x2, imbeni*
*Mungu Muumba x2, twakushukuru.*

**Ng'ombe:** *(Akimpongeza)* Una sauti kama ya ninga! Hongera. Hebu nawe tegua kitendawili changu: Ndugu wawili hufanya kazi kwa zamu.

**Ngamia:** *(Anatikisa masikio yake halafu anajibu)* Mikono!

**Ng'ombe:** La, umenoa.

**Ngamia:** Miguu!

**Ng'ombe:** Hapana.

**Ngamia:** Basi nakupatia mji wa Funua.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Ng'ombe:** Naupenda mji wa Funua. Jibu ni jua na mwezi.

**Ngamia:** *(Anaonyesha kuridhika)* Kuhusu tungo za fasihi sishindani nawe. Yaelekea ulipata msingi bora kutoka kwa mzazi wako.

**Ng'ombe:** Nashukuru. Mtoto wa nyoka ni nyoka. Mzazi wangu alikuwa simba wa fasihi katika jamii yetu. Ninaweza kukusimulia hadithi nyingi. Vilevile, mimi ni stadi wa kuimba mashairi.

**Ngamia:** Unaweza kunisimulia hadithi gani?

**Ng'ombe:** Siku nyingine tafadhali. Naona usiku utanipata hapa nyumbani kwako. Hebu niondoke nirudi kiamboni. Kesho majaliwa nitakuja na novela kuhusu uhusiano wa wanyama. Utaifurahia tukiisoma pamoja.

*(Wanaagana.)*

2. Tajeni tungo za fasihi kutoka kwenye mazungumzo ambayo mmeyaigiza.

**Shughuli ya 4:** Kuwasilisha utungo wa fasihi

1. Chagua mojawapo kati ya tungo za fasihi simulizi zifuatazo:

   (a) hadithi (b) ushairi (c) nyimbo (d) semi.

   Wasilisha mbele ya wenzako, utunzi ambao umewahi kusikia wa utungo huo.

2. Waombe wenzako wakutolee maoni yao.

**Changamkia**

Mkiwa katika kikundi, imbeni wimbo mnaojua kuhusu nchi yetu ya Kenya.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kunasa utungo uliowasilisha katika shughuli ya 4.
2. Mwombe mwenzako kusikiliza utungo uliounasa na akupatie maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mwombe mzazi au mlezi wako kusikiliza utungo uliounasa kisha akupatie maoni yake.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa kina – Novela

**Kichocheo:**

Unafurahia kusoma vitabu gani vya hadithi?

**Shughuli 1:** Maana ya novela

1. (a) Tazama picha zifuatazo (a) na (b).




(a)



KOVU LA HUBA

Kovu la huba ni novela inayosimulia kisa cha binti anayefiwa na mamake mzazi akiwa kikembe. Sidi anaishia mikononi mwa malimwengu. Anapata hela za kurudi tena masomoni kwa njia ya mtandao. Anasomea shahada ya uanahabari. Akiwa huko kazini, anapendana na Baraka mtoto wa mwajiri wake. Baraka pia ni mwanafunzi wa chuo kikuu. Sidi anapata mimba ya Baraka. Wanachumbiana. Katika pilkapilka hizo, Mzee Solomoni ambaye ni Baba yake Baraka, anajaribu kumshawishi Sidi kufanya mapenzi naye.

Sidi anajithamini. Anakataa vishawishi vya zawadi na pesa. Solomoni anaamua kumbaka Sidi. Kwa bahati mbaya, bastola ambaye mzee huyo amashikia Sidi inafyatuka. Mzee Solomoni anajipiga risasi mwenyewe. Anaanguka na kuzirai. Sidi anakamatwa nakutiwa ndani. Anashtakiwa kwa kosa la jaribio la mauaji. Baraka anamlaani na kumkana. Sidi anapata uchungu wa mimba akiwa kizimbani.

Anajifungua mtoto wa kiume siku hiyo hiyo. Anamwita Johari. Hadithi inapelekea kwisha, ukweli unadhihirika. Solomoni ndiye mwenye makosa. Je Sidi atamfungulia mashtaka Mzee Solomoni ambaye sasa ni babu ya Johari?

1 234567 890128 >

(b)

(b) Je, zinahusu nini? Mweleze mwenzako.

2. Tazama kitabu cha hadithi utakachoonyeshwa na mwalimu.
3. Soma anwani ya kitabu hicho.

4. Ukiwa na mwenzako, elezeni kitabu hicho ni cha aina gani.
5. Tumia kamusi au mtandao kutafuta maana ya **novela**.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa novela ni maandishi ya nathari yaliyo na ploti ya moja kwa moja na wahusika wake huwa wachache.

**Shughuli ya 2:** Sifa za novela

1. Soma sehemu ya novela iliyoteuliwa na mwalimu.
2. Ukiwa na wenzako katika kikundi, jadilini sifa za novela mliyosoma mkirejelea:
   (a) idadi ya kurasa
   (b) idadi ya wahusika
   (c) yanayozungumziwa.
3. (a) Tafuteni maktabani au mtandaoni sifa zaidi za novela.
   (b) Andika sifa hizo kwenye daftari lako.

### Tembea na majira

1. Ukiwa na mwenzako, tumieni mtandao kutafiti zaidi kuhusu sifa za novela.
2. Waelezeni wenzenu sifa za novela mlizozipata mtandaoni.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mwonyeshe mzazi au mlezi wako novela unayoisoma na kumtajia wahusika waliomo.

## C. KUANDIKA

### Insha za kubuni

### Kichocheo

1. Ni kisa gani unachoweza kuandikia insha ya kubuni?
2. Unaweza kuandika vidokezo gani kuhusu kisa ulichotambua?

**Shughuli ya 1:** Mada na ujumbe wa kuandikia insha ya kubuni

1. Jadili na mwenzako mada mbalimbali za kuandikia insha ya kubuni kuhusu wanyama.
2. Chagua mojawapo ya mada hizo ili kuandika insha ya kubuni.
3. Eleza ujumbe wa insha yako utakuwa upi.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 2:** Vidokezo kulingana na mada ya kuandikia insha ya kubuni

1. Mshirikishe mwenzako:
   (a) Kutafiti vitabuni, magazetini au mtandaoni kuhusu mada uliyoichagua ya insha ya kubuni.
   (b) Kujadili vidokezo vya mada ya insha uliyochagua.

**Shughuli ya 3:** Vidokezo vyenye ujumbe unaolingana na mada ya insha ya kubuni

1. Andika daftarini vidokezo vya insha ya kubuni uliyoichagua.
2. Panga vidokezo hivyo kwa mtiririko unaofaa.

**Shughuli ya 4:** Kuandika insha ya kubuni

1. Tumia vidokezo ulivyovipanga kuandika insha ya kubuni.
2. Wasomee wenzako insha ya kubuni uliyoiandika. Waombe kutoa maoni yao kuhusu insha hiyo.
3. Andika nakala safi ya insha hiyo na kuihifadhi kwenye potifolio.
4. Wasilisha potifolio kwa mwalimu ili aisahihishe insha yako.

**Tembea na majira**
1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika upya insha yako ukizingatia maoni uliyopewa na wenzako.
2. Hifadhi insha yako kidijitali ili kuirejelea baadaye.

**Shirikisha mzazi au mlezi**
1. Msomee mzazi au mlezi wako insha uliyoiandika ili atoe maoni yake.
2. Hifadhi insha hiyo katika potifolio. Utairejelea wakati utakapoihitaji.

## D. SARUFI

### Aina za nomino

### Nomino za wingi na nomino za vitenzi-jina

### I. Nomino za wingi

**Kichocheo**
Ni vitu gani unavyojua ambavyo hupatikana katika wingi tu?

**Shughuli ya 1:** Nomino za wingi katika matini

1. (a) Soma kila neno katika kapu maneno:



Nomino kwenye kapu maneno

(b) Tambua nomino za wingi katika kapu maneno.
(c) Andika daftarini nomino za wingi ulizotambua.

2. Mhusishe mwenzako kutambua na kuandika nomino za wingi za vitu vinavyopatikana:
   (a) shuleni
   (b) nyumbani.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya nomino za wingi katika matini

1. Tunga sentensi ukitumia nomino za wingi zifuatazo:
   (a) mvua
   (b) chumvi
   (c) mate
   (d) mchanga
   (e) unga
   (f) asali
   (g) vumbi
   (h) samli
   (i) wali
   (j) maziwa.
2. Tumia nomino za wingi zisizopungua tano kuandika aya ya maneno hamsini kuhusu uhuru wa wanyama. Pigia mstari nomino za wingi ulizotumia.

## II. Nomino za vitenzi-jina

### Kichocheo

Unafikiri nomino za vitenzi-jina ni gani?

**Shughuli ya 1:** Nomino za vitenzi-jina katika matini

1. (a) Tafuta katika mraba wa maneno nomino za vitenzi-jina zifuatazo:
   Kusafisha, kugawa, kubeba, kulea, kufaidi, kula na kutibu.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | U | S | A | F | I | S | H | A | O | K | M | T |
| Z | R | M | G | J | O | A | B | A | K | U | L | A |
| K | U | G | A | W | A | L | B | A | W | F | P | D |
| T | U | Y | V | N | P | K | U | L | E | A | H | A |
| R | W | L | E | V | U | A | K | U | T | I | B | U |
| H | Z | J | A | L | M | S | W | Z | J | D | K | Y |
| K | U | B | E | B | A | P | E | R | G | I | F | V |
| K | N | A | O | M | E | B | A | T | D | T | P | L |

(b) Andika nomino hizo daftarini.

(c) Soma kifungu kifuatacho:

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa nomino za vitenzi - jina ni aina za vitenzi ambapo vitenzi mzizi hutiwa kiambishi awali ku-. Hutumiwa katika wakati uliopita na ujao. Hata hivyo, maana ya kitenzi jina huwa ni sawa na kitenzi-jina chake.

**Shime tulinde mazingira**

Kutunza mazingira ni jambo la faida. Ninamhimiza kila mwanadamu kuzingatia utunzaji mazingira. Sisi sote, mimea na wanyama tutafaidi sana. Hebu waza kama watu wataanza kukata miti bila mpango maalum. Wakifanya hivyo tutajuta kwa kukosa mvua ya kutosha. Majangwa yatazidi kuenea. Chakula kitakuwa shida kupata. Dhiki kuu itakuwa imegubika dunia.

Hivi majuzi mjini Glasgow Uingereza, kumefanyika makutano kujadili mabadiliko ya hali ya anga na athari zake. Kila mshiriki wa mkutano alikubali kuwa kiwango cha joto duniani kinaongezeka kwa kasi. Hali hiyo inatokana na mwanadamu kuchafua mazingira yake. Hali ikiendelea hivyo, kutazuka janga duniani. Kwa mfano, barafu itayeyuka milimani. Mito itakauka kwa kuwa vyanzo vyake vitakuwa vimeathirika.

Ni vizuri kuhimiza watu kutumia gesi na kawi itokanayo na jua pale inapowezekana. Watu wakifanya hivyo, anga haitachafuliwa kama ilivyo sasa. Ninawasihi tuungane sote kulinda mazingira. Mazingira safi ni uhai bora.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

(d) Andika daftarini nomino za vitenzi-jina zilizo katika kifungu ulichokisoma.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya nomino za vitenzi-jina katika matini

1. Tunga sentensi ukitumia nomino za vitenzi-jina zifuatazo:
   (a) kutunza
   (b) kuchoka
   (c) kutetea
   (d) kupumzika
   (e) kupona
   (f) kulisha
   (g) kupanda
   (h) kuosha
   (i) kutibu
   (j) kusaidia.
2. Tumia nomino za vitenzi-jina zisizopungua tano kuandika aya ya maneno hamsini. Pigia mstari nomino za vitenzi-jina ulizotumia.
3. Wasilisha kazi yako kwa mwalimu wako ili aisahihishe na kukupa maoni yake.

**Changamkia**

Mkiwa wawiliwawili, fanyeni mchezo ambapo mmoja akitaja nomino ya wingi au ya kitenzi-jina mwenzake anatunga sentensi akiitumia. Fanyeni hivi kwa zamu.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika sentensi tano zenye:
   (a) nomino za wingi
   (b) nomino za vitenzi-jina.
2. **Koleza rangi** nomino za wingi.
3. Andika katika *italiki* nomino za vitenzi-jina.
4. Hifadhi rekodi ya sentensi hizo kwenye faili ya kidijitali ili uirejelee utakapoihitaji.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizoandika daftarini kuhusu nomino za wingi na za vitenzi-jina.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu sentensi hizo.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Tatua

Umempata mbuzi amekazwa kwa kamba shingoni.
Kuna watu wazima karibu ila hawamwoni mbuzi huyo.
Eleza mwenzako ungefanya nini kumwokoa mbuzi huyo.

# 4 AINA ZA MALIASILI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Nyimbo za watoto na bembelezi

### I. Nyimbo za watoto

**Kichocheo**

1. Je, ni nyimbo gani za watoto unazozijua katika jamii yako?
2. Unapoimba nyimbo za watoto, unazingatia mambo gani ili mtoto atulie au kulala?

**Shughuli ya 1:** Nyimbo za watoto

1. (a) Sikiliza wimbo ufuatao ukiimbwa na mwalimu au mgeni mwalikwa:

*Mabata wadogo wadogo x2*
*Wanaogelea x 2*
*Katika ziwa letu la maji safi*
*Wanafanya kwa kwa kwa X2*
*Katika ziwa letu la maji safi.*

*Tumbili wadogo wadogo x2*
*Wanarukaruka x2*
*Katika mitu yetu ya miti ya juu*
*Wanafanya ki ki ki X2*
*Katika mitu yetu ya miti ya juu.*

*Vifaru wadogo wadogo x2*
*Wanatembea x2*
*Wanapanda mlima kwa kwato zao*
*Wanafanya ngwa ngwa ngwa x2*
*Wanapanda mlima kwa kwato zao.*

(b) Je, unafikiri ni akina nani huimba wimbo kama huu katika jamii yako?

(c) Unafikiri wimbo huu huimbwa wakati gani?



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa nyimbo za watoto ni nyimbo zinazoimbwa na watoto.

**Shughuli ya 2:** Sifa za nyimbo za watoto

Mweleze mwenzako sifa za wimbo uliosikiliza katika shughuli ya 1 ukirejelea:

(a) urefu

(b) urudiaji wa maneno

(c) mahadhi.

**Shughuli ya 3:** Mitindo ya uwasilishaji wa nyimbo za watoto

1. Shirikiana na mwenzako kuimba wimbo wa watoto mliosikiliza katika shughuli ya 1.
2. Mshirikishe mwenzako kujadili namna ya kuwasilisha nyimbo za watoto mkirejelea:
   (a) sauti
   (b) urudiaji
   (c) miondoko ya mwili.

**Shughuli ya 4:** Kuwasilisha nyimbo za watoto

(a) Chagua wimbo wa watoto unaoujua.

(b) Imba wimbo huo mbele ya wenzako ukizingatia mitindo ya uwasilishaji wake kama vile kuchezesha viungo na sauti ifaayo.

## II. Bembelezi

### Kichocheo

1. Je, ni nyimbo gani unazozijua katika jamii yako ambazo huimbwa ili kumbembeleza mtoto?
2. Unapoimba bembelezi, unazingatia mambo gani ili mtoto atulie au kulala?

**Shughuli ya 1:** Bembelezi

1.(a) Sikiliza wimbo ufuatao ukiimbwa na mwalimu au mgeni mwalikwa:

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Mama anakuja lala,*
*Akupe maziwa lala.*

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Baba anakuja lala,*
*Akupenda toto lala.*

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Nyanya anakuja lala,*
*Akuoshe toto lala.*

*Lala mtoto lala*
*Lala mtoto lala*
*Babu anakuja lala,*
*Alete zawadi lala.*

(b) Eleza mwenzako wimbo mliousikiliza unaimbiwa nani.

(c) Jadilini na mwenzako watu wanaoimba wimbo huo.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa bembelezi ni nyimbo ambazo huimbiwa mtoto ili awache kulia au alale. Bembelezi huimbwa na watoto au watu wazima.

**Shughuli ya 2:** Sifa za bembelezi

Mweleze mwenzako sifa za wimbo uliosikiliza katika shughuli ya 1 ukirejelea:

(a) urefu

(b) urudiaji wa maneno

(c) mahadhi.

**Shughuli ya 3:** Mitindo ya uwasilishaji wa bembelezi

1. Shirikiana na mwenzako kuimba bembelezi mlizosikiliza katika shughuli ya 1.
2. Mshirikishe mwenzako kujadili namna ya kuwasilisha bembelezi mkirejelea:
   (a) sauti
   (b) urudiaji
   (c) miondoko ya mwili.


Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 4:** Kujadili mitindo ya uwasilishaji wa bembelezi

(d) Chagua wimbo bembelezi unaoujua.

(e) Imba wimbo huo mbele ya wenzako ukizingatia mtindo ya uwasilishaji wake kama vile kuchezesha viungo na sauti ifaayo.

**Changamkia**

Jifunze nyimbo za watoto na bembelezi kutoka jamii mbalimbali.

### Tembea na majira

Mwombe mwenzako akurekodi ukiimba wimbo uliouchagua wa watoto na bembelezi.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Imbeni na mzazi au mlezi wako wimbo wa watoto na bembelezi ambao huimbwa katika jamii yenu.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa ufasaha

**Kichocheo**

Unazingatia nini ili kusoma makala kwa ufasaha?

**Shughuli ya 1:** Matamshi bora

1. (*a*) **Msomee mwenzako kifungu kifuatacho kwa sauti:**

Koza alikuwa amejiandaa kuingia katika awamu nyingine ya maisha yake. Alitaka kubadilisha jina lake. Alikuwa amechoshwa mno kuitwa mhuni na tapeli. Hakuelewa ni kwa nini alibandikwa majina hayo. Koza alishuku kuwa alipewa majina hayo kwa kukosewa heshima tu. Koza aliendelea kuwa na tumaini kwamba angeimarika kiuchumi. "Asiye na wake ana Mungu," alijisemea.

Koza alimsubiri baba yake kwa hamu na ghamu. Kulingana na mkataba wa awali walikuwa wameafikiana kwamba baba angemletea stakabadhi za makubaliano ya kukodi shamba. Tangu aipoteze kazi yake, Koza aliwekeza katika biashara kadha wa kadha. Alipata faida kidogo tu. Kwa muda mrefu aliwazia kuwekeza katika kilimo. Tatizo kubwa lilikuwa ukosefu wa shamba.

Mlio wa gari ulisikika kwa mbali. Koza alikodoa macho na moyo ukampapa nusura kifua kipasuke. Koza aliliona gari la baba yake. "Leo ni leo, asemaye kesho ni muongo," aliwaza kimoyomoyo. Baba alishuka kutoka garini huku ameweka bahasha kuukuu kwapani. Alimwashiria Koza waingie nyumbani.

"Kupoteza kazi si mwisho wa matumaini. Natumai kupitia biashara zako umejifunza kuwa bidii na mikono yako inaweza kukukimu katika maisha. Nakukabidhi mkataba wa kukodi shamba hili. Kuna utajiri usiopimika hapa mchangani!"

Koza alipiga magoti na kuinua mikono yake. "Asante sana baba. Nimejifunza mengi. Nitajitahidi katika kilimo." Alimwambia baba yake.

Miezi sita baadaye, Koza alivuna tani ishirini za vitunguu alivyouza na kupata pesa nyingi. Alinunua trekta ili aendeleze kilimo chake. Ubavuni mwa trela la trekta lake paliandikwa UDONGO NI RASLIMALI TOSHA.

(b) Mwombe mwenzako akutolee maoni yake kuhusu matamshi yako.

**Shughuli ya 2:** Kutumia kasi ifaayo unaposoma

1. Soma tena kifungu katika shughuli ya 1 kwa kasi huku mwenzako akikuhesabia idadi ya maneno uliyoyasoma kwa muda wa dakika moja.
2. Mwombe mwenzako akuhesabie maneno ambayo umeweza kusoma katika muda wa dakika moja.
3. Weka rekodi ya idadi ya maneno ili ikufae katika kuboresha kazi yako ya usomaji.

**Shughuli ya 3:** Kutumia sauti ipasavyo unaposoma

1. Ukiwa na mwenzako: Soma aya za kwanza mbili katika kifungu cha shughuli ya 1 kwa kuzingatia kiwango cha sauti kifaacho.
2. Mwombe mwenzako akupe maoni kuhusu usomaji wako.

**Shughuli ya 4:** Kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo

Wasomee wenzako aya mbili za mwisho za kifungu cha shughuli ya 1 ukizingatia ishara kama za uso na mikono.

**Changamkia**

1. Msikilize mwanahabari akitangaza taarifa.
2. Mwigize mtangazaji huyo mbele ya wenzako darasani.

## Tembea na majira

1. Jirekodi ukimwigiza mtangazaji wa habari.
2. Msambazie mwenzako rekodi hiyo kwa kutumia kifaa cha kidijitali ili akupe maoni yake.

## Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwasilishie mzazi au mlezi wako habari uliyorekodi ukimwigiza mtangazaji.
2. Mwombe akutolee maoni kuhusu utamkaji wako.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

## C. KUANDIKA

### Insha za kubuni — Masimulizi

**Kichocheo**

Unazingatia mambo gani unapoandika insha ya masimulizi?

**Shughuli ya 1:** Lugha ya kiubunifu katika insha za masimulizi

1. (a) Soma kielelezo cha insha ya masimulizi kifuatacho:

MVUMILIVU HULA MBIVU

Ama kweli bidii ni mali. Katika kitongoji cha Sura, paliishi kijana mmoja aliyefahamika kama Kawesa. Kawesa alikuwa katika Gredi ya Saba shule ya Kipepeo. Eneo la Kipepeo lilikumbwa na matatizo kadha wa kadha. Kulikuwa na ukame na ukosefu wa ajira kwa vijana wengi. Kawesa hakufanya ajizi masomoni. Alifahamu fika kuwa ajizi ni nyumba ya njaa. Dhamira yake ikawa kuikomboa jamii yake kutoka katika lindi la umaskini.

Kawesa alikuwa na talanta ya ukimbiaji. Alifanya mazoezi ya mara kwa mara kwenye milima na mabonde. Mwalimu wake wa michezo alimhimiza, "Mtaka cha mvunguni sharti ainame. Ukitia bidii siku moja utakuwa mwanariadha tajika. La muhimu kwa sasa ni kutumia muda wako vizuri katika masomo na michezoni." "Asante sana Bi. Faraja kwa ushauri wako." Kawesa alimwambia.

Kawesa alifuzu na kujiunga na chuo kikuu. Huko, alisomea Elimu ya Mazingira. Pia alijiunga na timu ya wanariadha. Wakati mmoja aliteuliwa kushiriki katika mashindano ya kimataifa ya riadha. Alishinda mbio za nyika. Kawesa alipata tuzo spesheli kwa kuvunja rekodi ya dunia.

Siku ya kurudi nyumbani Kawesa alikaribishwa na wanakijiji katika uwanja wa ndege. Walimwimbia na kumsifu. Alihojiwa na mwanahabari kuhusu tuzo yake. "Je, utaitumia vipi tuzo yako Bwana Kawesa?" "Nataka kuanzisha mradi mkubwa wa maji huko kwetu Kipepeo," Kawesa alimjibu kwa bashasha. Wanakijiji walishangilia na kurukaruka kama ndama.

Ahadi ni deni. Kawesa aliwaleta vijana pamoja na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kushirikiana. Alianzisha mradi wa kuchimba kisima baada ya kupata kibali kutoka kwa maafisa wa mazingira, Wizara ya Maji na Shirika la Ukadiriaji wa Ubora wa Bidhaa. Kisima hicho kiliwafaidi wakazi wa Kipepeo kwa njia tofauti. Walipata maji ya kutumia nyumbani mwao. Wafugaji walipata maji ya mifugo yao.

Waliokuza mimea mbalimbali walinyunyizia mashamba yao maji. Vijana nao wakaanzisha mradi wa kupakia na kuuza maji. Eneo la Kipepeo liliimarika sana kimaendeleo. Kweli, kuinamako ndiko kuinukako.

(b) Shirikiana na mwenzako kutoa mifano ya semi zifuatazo kutokana na kielelezo ulichosoma cha insha ya masimulizi:
   (i) methali
   (ii) nahau
   (iii) tashbihi
   (iv) misemo.

**Shughuli ya 2:** Umuhimu wa lugha ya kiubunifu katika insha za masimulizi

1. Jadili na mwenzako umuhimu wa kutumia methali, nahau, tashbihi na misemo katika insha ya masimulizi.
2. Jadili na mwenzako mbinu zingine za kiubunifu zinazoweza kutumiwa katika insha ya masimulizi.

**Shughuli ya 3:** Wahusika na mandhari katika insha za masimulizi

Ukirejelea kielelezo cha insha ya masimulizi ulichokisoma katika shughuli ya 1(a) eleza:

(a) wahusika waliotumiwa

(b) mandhari yaliyotajwa.

**Shughuli ya 4:** Umuhimu wa wahusika na mandhari katika insha za masimulizi

Fanyeni shughuli hii mkiwa katika kikundi.

1. Jadilini umuhimu wa wahusika katika insha uliyosoma mkizingatia mambo yafuatayo:
   (a) majina yao
   (b) tabia zao
   (c) mambo wanayofanya
   (d) uhusiano wao
   (e) maneno wanayosema.
2. Jadilini umuhimu wa mandhari katika insha mliyosoma mkizingatia mambo yafuatayo:
   (a) Mahali mbalimbali palipotajwa katika insha.
   (b) Wakati mhusika mkuu alifanya mambo mbalimbali yaliyoelezwa katika insha.

**Shughuli ya 5:** Kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia lugha, wahusika na mandhari

1. Andika insha ya masimulizi inayoanza hivi:

   Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuzuru mbuga ya wanyama. Siku hiyo ...

2. Mwasilishie mwalimu wako insha ya masimulizi uliyoandika ili akutolee maoni yake.
3. Andika nakala safi ya insha baada ya mwalimu kukurekebisha.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Changamkia**

1. Mpe mwenzako insha yako asome.
2. Mwombe atoe maoni kuhusu matumizi yako ya lugha, wahusika na mandhari.

**Tembea na majira**

1. Tumia kifaa cha kidijitali kupiga chapa insha ya masimulizi uliyoandika katika shughuli ya 5 swali la 3.
2. Hifadhi insha hiyo katika faili kidijitali ili uirejelee unapoihitaji.

**Shirikisha mzazi au mlezi**

Msomee mzazi au mlezi wako insha uliyoiandika daftarini ili atoe maoni yake.

## D. SARUFI

### Nyakati

**Kichocheo**

Kwa nini tunatumia nyakati mbalimbali katika mawasiliano?

### I. Wakati uliopo

**Shughuli ya 1:** Vitenzi vilivyo katika wakati uliopo

1. Soma maneno yafuatayo:

| Neno. | Sehemu za neno |
|---|---|
| (a) ninalima | ni na lima |
| (b) unachimba | u na chimba |
| (c) anatengeneza | a na tengeneza |
| (d) mnatangaza | m na tangaza |
| (e) tunauza | tu na uza |

2. Umegundua nini kuhusu maneno na sehemu za maneno katika swali la 1?
3. Ni sehemu gani ya neno inayowakilisha wakati katika maneno uliyoyasoma katika swali la 1 ?
4. Mweleze mwenzako kipande hicho cha neno kinawakilisha wakati gani?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wakati uliopo huwakilishwa na sehemu ya neno -na- katika neno. Kila neno katika swali la kwanza lina sehemu ya -na- kwenye neno kuonyesha kwamba kitendo kinafanyika wakati huo.

5. Andika daftarini vitenzi kwenye kifungu kifuatacho na utambue vitenzi katika wakati uliopo.

Eneo la Mokolo linajulikana kwa migodi ya dhahabu. Watu wengi wanafaidika kutokana na biashara ya dhahabu. Hata hivyo, uchimbaji wa migodi ya dhahabu wakati mwingine unahatarisha maisha. Matumizi ya teknolojia ya uchimbaji wa dhahabu yanaweza kuhakikishia wachimbaji migodi usalama wao. Kupanda miti kwa wingi katika eneo la Mokolo kunaimarisha mazingira. Biashara ya dhahabu inaweza kuleta maendeleo makubwa nchini.

**Shughuli ya 2:** Kutumia wakati uliopo katika sentensi

Chagua neno moja moja katika A, B na C kwenye jedwali lifuatalo ili kuunda sentensi katika wakati uliopo.

| | A | B | C |
|---|---|---|---|
| (a) | Mchuuzi | anajenga | madini |
| (b) | Mwanariadha | anatengeneza | kamba |
| (c) | Chiriku | anakagua | kiota |
| (d) | Mhandisi | anauza | mradi. |
| (e) | Mhunzi | anaruka | sanamu |

## II. Wakati uliopita

**Shughuli ya 1:** Kutambua wakati uliopita

1. Ukiwa na mwenzako, someni maneno yafuatayo kwa zamu:

| | |
|---|---|
| **nilinunua** | **walienda** |
| **walishirikiana** | **alivuna** |
| **walienda** | **ulitangaza** |



KICD Kimeidhinishwa na KICD

2. Ni kipande gani cha neno kinachowakilisha wakati katika maneno uliyoyasoma?

3. Mweleze mwenzako kipande hicho cha neno kinawakilisha wakati gani?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wakati uliopita huwakilishwa na -li- katika neno. Mfano ni alilima, kuonyesha kuwa alifanya kitendo hicho na muda umepita tangu afanye kitendo hicho.

**Shughuli ya 2:** Kutumia wakati uliopita katika sentensi

Panga maneno yafuatayo ifaavyo ili kuunda sentensi sahihi.

1. yake kazi Roda mapema alimaliza
2. dhahabu soko katika iliuzwa
3. shuleni jana kitabu alisoma
4. vizuri zilikauka nguo zake
5. ilinyesha mwaka uliopita mvua.

### III. Wakati ujao

**Shughuli ya 1:** Kutambua wakati ujao

1. Soma maneno yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **nitapika** | **mtashinda** | **utasaka** |
| **tutaomba** | **atafikiri** | |

2. Ni kipande gani cha neno kinachowakilisha wakati katika maneno uliyoyasoma katika swali la 1?

3. Mweleze mwenzako kipande hicho cha neno kinaonyesha kitendo kilifanyika au kitafanyika wakati gani?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wakati ujao huwakilishwa na -ta- katika neno.

4. Andika daftarini vitenzi kwenye kifungu kifuatacho na utambue vitenzi katika wakati uliopo.

   Mgeni mteule atawasili saa sita kamili. Atalakiwa na kundi la wanamazingira. Watapiga foleni mbele ya darasa na kuimba Wimbo wa Taifa. Wanafunzi wengine watashangilia.

**Shughuli ya 2:** Kutumia wakati ujao katika sentensi

1. Tumia vitenzi vifuatavyo ili kuunda sentensi kuonyesha wakati ujao
   (a) shona
   (b) chimba
   (c) pakua
   (d) fua
   (e) zima
2. Andika upya sentensi kwenye jedwali kuonyesha wakati uliotajwa.

| | Wakati uliopita | Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|---|---|
| (a) | Balozi aliwasalimu wajumbe. | | |
| (b) | | Katibu anahutubia wateja. | |
| (c) | | | Mechi itachwezwa leo. |

**Changamkia**

Mkiwa katika kikundi, tungeni sentensi kwa zamu kuwakilisha nyakati tofauti.

### Tembea na majira

1. Andika na uhifadhi sentensi ulizotunga katika shughuli ya 2 kwenye kifaa cha kidijitali na kuwasambazia wenzako mtandaoni.
2. Waombe wakupe maoni yao kupitia kwa njia hiyo hiyo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizotunga daftarini.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu sentenzi hizo.

## Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada ndogo.

| Mada ndogo | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Jumuika na jamii

1. Mwombeni mwalimu wenu kumwalika mwanamazingira shuleni ili awazungumzie kuhusu umuhimu wa kutunza miti.
2. Kutokana na mazungumzo hayo, andaeni mabango yenye maandishi kuhusu faida za miti.
3. Elekezwa na mwalimu mahali pa kutundika mabango hayo ili wengine wayasome.

**Tatua**

Chukulia kuwa wewe ni kiongozi wa vijana mtaani kwenu. Hapo karibu na kwenu kuna mto. Umegundua kuna watu msiowajua wanaochafua mto huo. Eleza namna ya kutatua tatizo hilo.

# 5 UNYANYASAJI WA KIJINSIA

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Mazungumzo mahususi

### Kichocheo

1. Je, wewe huwaamkua na kuwaaga watu vipi?
2. Je, ni maamkuzi na maagano gani yanayotumika katika jamii yako?
3. Unafikiri ni kwa nini ni muhimu kujua maamkuzi na maagano mbalimbali?

**Shughuli ya 1:** Maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali za siku

Mkiwa na mwenzako:

1. Igizeni mazungumzo haya.

*(Ni asubuhi. Bati na Roba wamekutana shuleni nje ya madarasa yao.)*

Bati: Habari ya asubuhi? *(Akimsalimia Roba.)*

Roba: Nzuri. Sijui na wewe? Umeamkaje?

Bati: Sijambo, nashukuru. Leo tutakutana jioni kwa mazoezi ya kukariri shairi?

Roba: *(Kwa uchangamfu)* Bila shaka. Leo lazima tujifunze beti mbili za shairi.

Bati: Sawa basi. Shinda salama. *(Akiingia darasani.)*

Roba: Kwaheri. Tutaonana jioni. *(Akiingia darasa tofauti.)*
*(Baadaye jioni hiyo, Bati na Roba wanakutana ukumbini.)*

Bati: Masalkheri?

Roba: Aheri. Naomba tuanze mazoezi ya kukariri shairi. Muda unatupa kisogo.

Bati: Haya tuanzeni. Beti zenyewe ni nyepesi. Tutazishika haraka.

**Maswali:**

2. Tajeni maneno ya maamkuzi na maagano yaliyotumika katika mazungumzo mliyoigiza.
3. Mkiwa katika kikundi, tambueni maneno ambayo ni maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali za siku katika chati hii:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **heko** | **hongera** | **umeshindaje** | **mzuri** |
| **shukrani** | **hujambo** | **tuonane tena** | **umeamkaje** |
| **wema** | **buriani** | **lala salama** | **alamsiki** |



KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | | | |
|---|---|---|---|
| **sabalkheri** | **asante** | **kwaheri** | **shabashi** |
| **habari** | **buheri** | **habari za asubuhi** | **masalkheri** |

## Shughuli ya 2: Majibu ya maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali za siku

1. Mkiwa na mwenzako chagueni maamkuzi na majibu yake katika chati hili:

| | |
|---|---|
| **1. Habari ya asubuhi?** | **Sina la kuamba au salama.** |
| **2. Sabalkheri?** | **Binuru.** |
| **3. Habari?** | **Marahaba.** |
| **4. Alamsiki?** | **Njema au nzuri.** |
| **5. Umeshindaje?** | **Salama.** |
| **6. Umeamkaje?** | **Njema au nzuri.** |
| **7. Habari za kutwa?** | **Masalkheri au aheri.** |
| **8. Masalkheri?** | **Sabalkheri.** |
| **9. Shikamoo?** | **Vyema.** |

2. Tajeni maagano na majibu yake katika kapu hili:




Kapu maneno

## Shughuli ya 3: Maamkuzi yanayotumiwa na makundi mbalimbali ya kijamii pamoja na majibu ya maamkuzi hayo

Mweleze mwenzako uhusiano unaojitokeza katika maamkuzi katika picha zifuatazo:




2. Mweleze mwenzako maamkuzi yanayotumiwa na makundi yafuatayo:
   (a) mtoto kwa mtu mzima
   (b) watu wa rika moja
   (c) mwanafunzi kwa mwalimu.

### Shabashi!

Nimegundua kuwa kuna maamkuzi ya nyakati mbalimbali za siku kama vile, asubuhi, mchana, jioni na usiku. Vilevile, kuna njia tofauti za kuagana katika nyakati mbalimbali. Nimegundua pia kuwa maamkuzi hutumiwa kwa njia tofauti na makundi mbalimbali ya watu katika jamii kwa kutegemea mambo kama vile umri, cheo na rika. Mfano ni mtoto anaweza kumwamkua mtu mzima kwa kusema, "shikamoo?" naye mtu mzima amjibu, "marahaba."

## Shughuli ya 4: Maamkuzi na maagano mwafaka katika miktadha mbalimbali

1.(a) Igizeni mazungumzo haya mkiwa katika kikundi.

| | |
|---|---|
| **Lufi:** | Shikamoo? |
| **Maka:** | Marahaba Lufi! U hali gani? |
| **Lufi:** | Njema. Nimefurahi kukuona (*Huku akitabasamu na uso wake ukimetameta kwa mwangaza wa jua.*) |
| **Maka:** | Nami pia. Habari za nyumbani? Watu hawajambo? |
| **Lufi:** | Habari za nyumbani ni nzuri. Watu wote hawajambo. |
| **Maka:** | Kaka yako amekwenda chuoni? |
| **Lufi:** | La hasha, yuko nyumbani anatayarisha chamcha. Hiki ni kipindi chake cha likizo. |
| **Maka:** | Anajua kupika? |
| **Lufi:** | Ndio, ni mpishi hodari sana. Ameniomba nikurudishie kipakatalishi hiki ulichomuazima jana. Amesema kimemfaa sana. Asante! |
| **Maka:** | Karibu. |
| **Lufi:** | Naomba kurudi haraka ili nimsaidie kaka. Alamsiki. |
| **Maka:** | Binuru. |

**Swali:**

(b) Ukiwa na mwenzako, amkuaneni na kuagana mkitumia maamkuzi na maagano mliyoyaigiza.

**Changamkia**

**Mkaririe mwenzako ubeti huu wa shairi:**

Zangu salamu pokea, rafiki habari gani?
Hali ninakujulia, hujambo huko nyumbani?
Mimi hapa natulia, niko salama mwandani
Salamu nakutumia, sijambo huku mjini.

### Tembea na majira

Rekodi ubeti uliokariri katika sehemu ya 'changamkia' kwenye kifaa cha kidijitali. Msambazie mwenzako ili akutolee maoni.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi wako maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali za siku.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa ufahamu

### Kichocheo

Ni mambo gani unayozingatia unapotaka kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu?

## Shughuli ya 1: Kutafuta habari mahususi katika kifungu cha ufahamu

1. (*a*) **Soma kifungu hiki cha ufahamu.**

Sali aliketi kando ya barabara iliyoelekea mjini. Alisoma maandishi HAKI NA UKWELI kwenye trela ambalo lilikuwa linapita. Aliyaona maandishi hayo kama ishara nzuri ya matumaini katika maisha yake. Aliiangalia barabara hiyo kwa tuo zaidi. Aliona mabonde na milima ambayo iliwakabili wasafiri. Baadhi ya magari yalishindwa kupanda milima na kujikokota kama konokono. Aliyalinganisha maisha yake na magari hayo.

Aliyaangalia magari hayo na kujiangalia. Machozi yalimtiririka njia mbilimbili kwenye uso wake. Matone mengine yalikiangukia kifua chake. **Alilia kwi kwi kwi**. Alipangusa machozi hayo harakaharaka. Aliyaangalia tena magari yale yaliyokuwa yanajikokota. Mengine yalikuwa yamefanikiwa kupanda mlima na kuifikia sehemu tambarare. Yalikuwa yanashika kasi. "Hivi kumbe maisha ni panda shuka." Sali alijiliwaza.

Sali alikumbuka alikotoka. Huko kulikuwa na giza totoro. Alikumbuka ajali iliyotokea mwezi wa sita kwenye barabara iyo hiyo na kuwachukua **wavyele** wake akiwa **kikembe**. "Ama kweli maisha ni kitendawili. Barabara hii iliyonisababishia **simanzi** na kilio kisicho kifani ndiyo itakayoniletea furaha na kicheko leo." Sali alijisemea.

Wazazi wa Sali walipoupungia ulimwengu mkono wa buriani, alibaki yatima. Lililokuwa limebaki ni kukesha na kuomba dua kwa Maulana amjalie **mbawazi** ili aweze kuendelea na maisha na elimu yake.

Sali alichukuliwa na mjomba wake Dori. Dori alimuahidi kuwa angempa usaidizi kwa hali na mali. Sali hakuwa wa hulka mbaya, kwa hivyo mjomba Dori alimpenda na kumtunza kama mwanawe. Kwa upande mwingine, mkewe Dori alimchukia na kumtesa Sali. Alimfanyisha kazi za sulubu, kumpimia chakula na wakati mwingine kumcheleweshа Sali kwenda shuleni. Kusudi lake lilikuwa kumhini Sali fursa ya kujiendeleza kielimu. Mjomba Dori alipodadisi mambo haya, bibi yake alimjibu kwa ukali, "Unampendelea Sali, utamharibu mtoto wa dadako. Sali ni mtoto wa kike, lazima apike, aoshe nguo na asafishe nyumba. Kumbuka kuwa mchelea mwana kulia, hulia yeye." Mjomba alisema, "Si lazima majukumu haya mazito yafanywe na mtoto wa kike. Kila mtoto anafaa kujifunza kufanya haya yote kwa kadri. Kumbuka Sali bado ni mtoto."

Baada ya kuchunguza, Dori aligundua kuwa mkewe alikuwa akimdhulumu Sali. Aliamua kumpeleka Sali mjini kwa dadake mdogo.

Sali aligutushwa na mlio wa honi la gari la Dori. Alinyanyuka kwa furaha kuingia garini. "Shangazi yako anakusubiri kwa hamu na ghamu. Atahakikisha kuwa utapata muda wa kuendeleza elimu yako. Tayari amekutafutia nafasi katika shule ya Melo." Dori alisema.

"Asante mjomba Dori. Najua unanijali. Nitajitahidi ili nifaidi." Sali alimwambia mjomba wake.



Kimeidhinishwa na KICD

Baada ya muda, mkewe Dori alijihisi mpweke. Alimtamani Sali. Aliamua kufunga safari kwenda kumtembelea Sali mjini. Alipofika, Sali alimkaribisha kwa moyo mkunjufu. Aligundua kuwa afya ya Sali imeimarika na amekuwa mchangamfu zaidi. Aliambiwa kuwa Sali alikuwa ameonyesha umahiri shuleni na kuwa kipenzi cha wengi. Bibi yake Dori alimwambia Sali, "Tafadhali nisamehe. Nimegundua nilikukosea. Naomba uwe ukinitembelea mara kwa mara." Sali na mke wa Dori walidondokwa na machozi ya furaha huku wakikumbatiana.

**Maswali**:

(b) Ukiwa na mwenzako, jibu maswali yafuatayo:

(i) Ni nani aliyekuwa ameketi kando ya barabara?

(ii) Sali alilinganisha maisha yake na nini?

(iii) Mjomba alimpeleka Sali wapi?

(iv) Ajali iliyompokonya Sali wazazi wake ilifanyika lini?

(v) Sali alipelekwa shule gani?

3. Jadili na mwenzako maelezo ya kudondoa habari mahususi zinazosimuliwa katika kifungu.

**Shughuli ya 2:** Habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi

Ukiwa na mwenzako:

1. Elezeni ujumbe katika kila aya ya kifungu mlichosoma kwa sentensi moja moja.
2. Tumieni sentensi hizo kueleza habari za kifungu cha ufahamu mlichosoma kwa ufupi.

**Shughuli ya 3:** Maana ya msamiati kulingana na muktadha wa kifungu cha ufahamu

Mkiwa katika kikundi:

1. Elezeni maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu:

(a) kujikokota (b) wavyele (c) mbawazi

(d) imarika (e) umahiri.

2. Tumieni kamusi kuthibitisha maana ya maneno yaliyotumika katika kifungu mliyoyaelezea kimuktadha.

### Tembea na majira

Sakura mtandaoni kifungu cha ufahamu kuhusu suala la kijinsia usome. Dondoa habari muhimu katika kifungu hicho. Wasambazie wenzako habari hizo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Wasilishia mzazi au mlezi wako habari muhimu katika kifungu cha ufahamu ulichosakura mtandaoni kuhusu suala la kijinsia. Mwombe akutolee maoni yake.

## C. KUANDIKA

### Insha ya maelekezo

**Kichocheo**

Je, unaweza kumuelekeza vipi rafiki yako kufika nyumbani kwenu ili asipotee?

**Shughuli ya 1:** Insha ya maelekezo

Mwelekeze mwenzako jinsi ya kufika shuleni kutoka sokoni. Fuata utaratibu huu:

1. Njia atakayotumia ni gani?
2. Safari itachukua muda gani?
3. Atapitia vituo gani?
4. Ataona vitu gani muhimu njiani?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa insha ya maelekezo ni maelezo ambayo unahitajika kuzingatia katika kutenda shughuli fulani. Hunuia kueleza waziwazi utaratibu wote na hatua zote za kufuata katika kutenda jambo hilo.

**Shughuli ya 2:** Aina za insha za maelekezo

1. Tazama picha hizi.




(a)



(b)

2. (a) Je, unafikiri watu kwenye picha wanatoa maelekezo kuhusu nini? Mweleze mwenzako.
   (b) Andika maelezo ya maelekezo daftarini mwako.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

## Shughuli ya 3: Sifa za insha ya maelekezo

1. Soma kielelezo hiki cha maelekezo ukiwa na mwenzako.

Jinsi ya kufika KITUO CHA AMANI kutoka Sifa

Fuata maelekezo yafuatayo ili kufika KITUO CHA AMANI kutoka Sifa:

(a) Safari itachukua muda wa karibu saa moja.
(b) Abiri gari nambari 27.
(c) Basi likishaingia katikati ya jiji shuka kwenye kituo cha mabasi cha Leba.
(d) Ukiangalia ng'ambo ya pili ya barabara utaona hoteli kubwa yenye maandishi KULA STAREHE.
(e) Vuka barabara hiyo ili kuelekea upande wa hoteli hiyo.
(f) Kisha fuata barabara inayoitwa FURAHA.
(g) Ifuate hadi pale inapopinda.
(h) Hapo utaona kituo cha Polisi cha LINDA WATU.
(i) Piga kona kushoto ufuate barabara ya RIZIKI.
(j) Endelea nayo hadi ufike barabara pacha (upande wa kushoto).
(k) Vuka barabara hiyo pacha na utakuwa kwenye lango kuu la uwanja wa michezo wa MABINGWA.
(l) Hatua chache, mbele utaona kibao kilichobandikwa maandishi KITUO CHA AMANI kwa rangi nyekundu kushoto.
(m) Tembea kwa mita karibu mia tano utafika kwenye lango kuu la KITUO CHA AMANI.

Unaweza kutumia hatua hizi kuandika insha kamilifu ya maelekezo.

2. Ukiwa na mwenzako zungumzieni kuhusu sifa za insha ya maelekezo. Zingatieni vipengele hivi:
   (a) anwani
   (b) usahihi wa habari
   (c) mpangilio wa maelezo unaoeleweka
   (d) lugha sahili
   (e) maelezo yanayotoka upande mmoja.

## Shughuli ya 4: Mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo

1. Ukiwa katika kikundi, shirikiana na mwenzako kuandaa mpangilio ufaao wa hatua za insha za maelekezo. Zingatieni utaratibu huu:
   (a) muda wa safari
   (b) njia atakayotumia
   (c) gari atakaloabiri
   (d) vituo atakavyopitia
   (e) vitu muhimu atakavyoona.
2. Nakili mpangilio mlioandaa kwenye daftari lako.

**Shughuli ya 5:** Kuandika insha ya maelekezo

1. Andika insha ya maelekezo ili kumwelekeza mwenzako kufika kwenu kutoka shuleni. Tumia mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo mlioandaa katika shughuli ya 4.
2. Msomee mwenzako insha ya maelekezo uliyoiandika. Mwombe akupe maoni yake kuhusu insha yako.
3. Andika nakala safi ya insha yako kwa kuzingatia maoni uliyopewa na kuihifadhi kwenye potifolio.
4. Wasilisha potifolio kwa mwalimu ili aisahihishe insha yako.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika upya insha yako ya maelekezo baada ya masahihisho ya mwalimu.
2. Hifadhi insha yako kidijitali ili uirejelee unapohitaji kufanya hivyo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako insha ya maelekezo uliyohifadhi katika potifolio.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu insha yako.

## D. SARUFI

### Nyakati na hali

#### Kichocheo

Kwa nini tunazingatia nyakati na hali katika mawasiliano yetu?

### I. Wakati uliopo hali ya kuendelea

**Shughuli ya 1:** Vitenzi vilivyo katika wakati uliopo hali ya kuendelea

1. Mweleze mwenzako kitendo unachokifanya sasa.
2. Igiza kitendo ulichokitaja.
3. Jadilini hali ya wakati wa kitendo unachoigiza sasa.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wakati uliopo hali ya kuendelea huonyesha kuwa kitendo kinaendelea kufanyika sasa.

4. Chagua vitenzi vinavyobainisha wakati uliopo hali ya kuendelea katika sentensi zifuatazo:
   (a) Mama anatukaribisha nyumbani.
   (b) Mtetezi wa haki anazungumza kuhusu haki za kijinsia.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

(c) Msichana anakariri shairi kuhusu usawa katika jamii.
(d) Mwanafunzi anaandika insha yake.
(e) Rais wa nchi anatoa taarifa sasa.

5. Nakili kifungu kifuatacho kisha upige mstari chini ya vitenzi vilivyo katika wakati uliopo hali ya kuendelea.

Charo anawazungumzia wanakijiji. Anawahimiza kuheshimiana. Anatoa ushauri kwa wote. Anawaomba wanaume na wanawake kushirikiana na kutangamana kwa upendo. Anasema kuwa wasaidiane katika shughuli za maisha ya kila siku.

**Shughuli ya 2:** Wakati uliopo hali ya kuendelea

1. Tunga sentensi tano katika wakati uliopo hali ya kuendelea.
2. Tunga kifungu cha aya moja ukitumia maneno matano katika wakati uliopo hali ya kuendelea.

## II. Wakati uliopita hali ya kuendelea

**Shughuli ya 1:** Vitenzi katika wakati uliopita hali ya kuendelea

1. (a) Mweleze mwenzako kitendo ulichokuwa ukifanya jana kabla ya kulala.
   (b) Jadilini hali ya wakati wa kitendo ulichokuwa ukifanya.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wakati uliopita hali ya kuendelea huonyesha kuwa kitendo kilikuwa kikiendelea wakati uliopita.

2. Nakili sentensi zifuatazo kisha upige mstari chini ya vitenzi vinavyobainisha wakati uliopita hali ya kuendelea.
   (a) Wanafunzi walikuwa wakicheza uwanjani.
   (b) Mkulima alikuwa akivuna mazao yake.
   (c) Wakili alikuwa akimwakilisha mshtakiwa.
   (d) Wanariadha walikuwa wakifanya mazoezi milimani.
   (e) Msichana alikuwa akifurahia kazi yake.
3. Nakili kifungu kifuatacho kisha uchoree mviringo vitenzi vilivyo katika wakati uliopita hali ya kuendelea.

Badi alikuwa akiimba. Alikuwa akienda shuleni kumuona mwalimu. Alikuwa akitia bidii ndipo aiwakilishe shule yake. Alikuwa akikumbuka kuwa bidii huzaa matunda.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya wakati uliopita hali ya kuendelea

1. Geuza sentensi hizi ziwe katika wakati uliopita hali ya kuendelea.
   (a) Nitakapofika dada atakuwa anafyeka nyasi.
   (b) Chifu atakuwa akihutubia kuhusu ubora wa mtoto wa kike na wa kiume.
   (c) Jamii imekuwa ikipewa mafunzo kuhusu umuhimu wa jinsia zote.
   (d) Dagita amekuwa akitia bidii mchezoni.
   (e) Haya yamekuwa mawaidha bora.
2. Tunga kifungu cha aya moja ukitumia maneno matano katika wakati uliopita hali ya kuendelea.

## III. Wakati ujao hali ya kuendelea

**Shughuli ya 1:** Vitenzi katika wakati ujao hali ya kuendelea

1. (a) Mweleze mwenzako kitendo utakachokuwa ukifanya kesho.
   (b) Jadilini hali ya wakati wa kitendo utakachokuwa ukifanya.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wakati ujao hali ya kuendelea huonyesha kuwa kitendo kitakuwa kikiendelea siku za usoni.

2. Soma sentensi zifuatazo kisha uandike vitenzi vinavyobainisha wakati ujao hali ya kuendelea.
   (a) Mhudumu atakuwa akiwaelekeza wageni.
   (b) Dereva wa kike atakuwa akiendesha gari jipya.
   (c) Galgalo atakuwa akiwahamasisha kuhusu tamaduni zilizopitwa na wakati.
   (d) Yosi atakuwa akitazama habari kwenye runinga.
   (e) Chifu atakuwa akiwatahadharisha dhidi ya ndoa za mapema.
3. Soma kifungu kifuatacho kisha unakili daftarini vitenzi vilivyo katika wakati ujao hali ya kuendelea.

Atieno atakuwa akiwaongoza wenzake darasani kama kiranja. Atakuwa akitarajiwa kuwa kielelezo bora kwa wenzake. Wenzake darasani watakuwa wakimsikiliza. Pia watakuwa wakimpa mapendekezo yao. Atieno atakuwa akiyawasilisha kwa mwalimu wa darasa.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya wakati ujao hali ya kuendelea

1. Chagua sehemu ya sentensi kutoka A na nyingine kutoka B ili kuunda sentensi sahihi kuonyesha wakati ujao hali ya kuendelea.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | A | B |
|---|---|---|
| (a) | Rais alikuwa akiwahutubia | wakunywe maziwa mara mbili kwa siku. |
| (b) | Watoto wamekuwa | mbunge atakapotutembelea. |
| (c) | Barabara itakuwa ikitengenezwa | wananchi mvua ilipoanza kunyesha. |
| (d) | Juzi nimekuwa na maumivu | wakati kelele hizo zitasikika. |
| (e) | Sherehe itakuwa imenoga | akiwapa dawa za minyoo. |
| (f) | Ng'ombe wake watakuwa na afya nzuri | nikaenda kumwona daktari. |

2. Tunga kifungu cha aya moja ukitumia maneno matano katika wakati ujao hali ya kuendelea.

**Changamkia**

Tungeni sentensi mkitumia:
1. Wakati uliopita hali ya kuendelea.
2. Wakati uliopo hali ya kuendelea.
3. Wakati ujao hali ya kuendelea.

### Tembea na majira

Tumia kifaa cha kidijitali kuandika upya sentensi zifuatazo ziwe katika nyakati na hali ulizopewa katika mabano:
1. Hukumu inatolewa na hakimu. (wakati uliopita hali ya kuendelea)
2. Mlezi alikuwa akiwalea watoto vyema. (wakati ujao hali ya kuendelea)
3. Wazazi watakuwa wakiwapeleka watoto shuleni. (wakati uliopo hali ya kuendelea)
4. Wenyeji walikuwa wakiwakaribisha wageni. (wakati ujao hali ya kuendelea)
5. Sherehe zilikuwa zikifanyika katika Uwanja wa Uhuru. (wakati uliopo hali ya kuendelea)

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizoandika katika kifaa cha kidijitali.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu sentensi hizo.

**Tatua**

Chukulia kuwa wewe ni kiranja wa darasa lako. Kuna wanachama wa shirika lisilo la kiserikali ambao wamekuwa wakitembelea shule yenu. Kila wanapofika shuleni huwatenga na kuwazungumzia wanafunzi wa kike peke yao. Wakati mwingine huwaletea wanafunzi wa kike zawadi pia. Wanafunzi wa kiume wamekuletea malalamishi yao. Je, utalitatua vipi tatizo hili?

# 6 USALAMA SHULENI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza kwa kufasiri

### Matini

### Kichocheo

Je, ni mambo gani unayoyazingatia unapofafanua habari unayosikiliza?

**Shughuli ya 1:** Masuala yanayozungumziwa katika matini ya kusikiliza

1. Sikiliza kwa makini mwalimu wako akisoma kifungu.
2. Shirikiana na mwenzako kueleza kuhusu suala kuu linalozungumziwa katika matini uliyosikiliza.

**Shughuli ya 2:** Habari katika matini ya kusikiliza

Jibu maswali yafuatayo:

1. Kwa nini ni muhimu kumjulisha mzazi au mwalimu kuhusu safari unayopanga?
2. Je, ni mambo gani hatari unayoweza kukumbana nayo shuleni?
3. Watoto hujikuta katika shida gani vita vinapozuka?

**Shughuli ya 3:** Maana ya msamiati kama ulivyotumika katika matini ya kusikiliza

1. Andika daftarini msamiati utakaosomewa na mwalimu.
2. Mkiwa katika kikundi, elezeni maana ya msamiati mlioandika kama ulivyotumika katika matini uliyoisikiliza mwalimu akisoma darasani.

**Shughuli ya 4:** Kutabiri kitakachotokea katika matini kwa kurejelea vidokezo katika matini ya kusikiliza

Ukiwa na mwenzako, eleza:

1. Mwalimu alipoanza kusoma habari ulifikiri ingehusu nini?
2. Je, mambo uliyofikiri yangezungumziwa katika habari ya mwalimu yalitokea?
3. Unafikiri ni hatari gani inayoweza kutokea mwanafunzi asipozingatia ushauri unaotolewa katika matini uliyosikiliza?

**Changamkia**

Mwanafunzi mgeni amejiunga na shule yenu. Mweleze mnavyozingatia usalama shuleni.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kunasa mazungumzo yako na mwanafunzi mgeni ukimweleza kuhusu usalama shuleni mwenu.
2. Msambazie mwalimu mazungumzo uliyoyanasa ili akutolee maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Tumia kifaa cha kidijitali kumfungulia mzazi au mlezi wako mazungumzo uliyoyanasa ili ayasikilize na kutoa maoni yake.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa kina

### Maudhui na dhamira

### Kichocheo

Vitabu vya hadithi ulivyowahi kusoma vinazungumzia nini?

**Shughuli ya 1:** Maana ya maudhui na dhamira katika fasihi

1. Hapo awali ulianza kusoma novela. Ukiwa na mwenzako, jadili:
   (a) Mambo yanayozungumziwa na mwandishi katika sehemu ya novela uliyosoma.
   (b) Maoni yako kuhusu lengo la mwandishi kuzungumzia mambo hayo.
2. Tazama kitabu cha hadithi utakachoonyeshwa na mwalimu.
   (a) Mweleze mwenzako anwani ya kitabu hicho inahusu nini?
   (b) Blabu inaonyesha mazingira gani?
3. Jadili na mwenzako maana ya:
   (a) dhamira (b) maudhui.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa dhamira ni lengo la mwandishi kutunga kazi yake.
Maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi.

**Shughuli ya 2:** Maudhui katika novela

1. Soma sehemu ya novela iliyoteuliwa na mwalimu.
2. Ukiwa na wenzako katika kikundi, jadilini maudhui mbalimbali katika sehemu ya novela mliyosoma.
3. Andika maudhui hayo kwenye daftari lako.

**Shughuli ya 3:** Dhamira katika novela

1. Ukiwa na wenzako katika kikundi, jadilini dhamira katika sehemu ya novela mliyosoma.
2. Andika dhamira hiyo kwenye daftari lako.

**Shughuli ya 4:** Muhtasari wa dhamira na maudhui kuhusu novela

1. Andika daftarini muhtasari kuhusu dhamira iliyojitokeza katika novela uliyosoma.
2. Wasilishia wenzako darasani muhtasari wa dhamira na maudhui ya sehemu ya novela uliyosoma.

**Shughuli ya 5:** Kujenga mazoea ya usomaji wa kazi za fasihi katika maisha ya kila siku

1. Soma vitabu mbalimbali vya fasihi.
2. Weka rekodi ya usomaji wako katika **Jarida langu.**

| | |
|---|---|
| Shule | |
| Jina | |
| Gredi | |
| Tarehe | |
| Anwani ya novela niliyosoma | |
| Muhtasari wa ujumbe niliopata na kuwasilisha kwa wenzangu | |
| Maoni waliyotoa wanafunzi wenzangu | |
| Maoni yangu | |
| Maoni ya mwalimu | |

3. Mwasilishie mwalimu jarida ili asome na atoe maoni yake.

### Tembea na majira

1. Piga chapa maudhui na dhamira ya kazi za shughuli ya 2 na ya 3.
2. Hifadhi kazi hiyo kwenye faili ya kidijitali utakayoiita '**Kazi ya fasihi**'.
3. Msambazie kidijitali mwalimu wako nakala ya kazi hiyo ili atoe maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi wako mafunzo uliyopata kutokana na novela uliyoisoma.

## C. KUANDIKA

### Insha za masimulizi kutokana na picha

#### Kichocheo

Je, ni vigezo vipi utakavyozingatia wakati wa kuandika insha ya masimulizi kutokana na picha?

**Shughuli ya 1:** Anwani inayooana na kisa kinachosimuliwa kutokana na picha katika matini

1. (*a*) Tazama picha zifuatazo kwa makini:




(b) Eleza unachokiona katika kila picha.

2. Unaweza kuipa anwani ipi hadithi inayotokana na picha hizi?

**Shughuli ya 2:** Maelezo dhahiri kuhusu matukio katika picha kwenye matini

Eleza mambo yanayotokea katika picha zifuatazo:






**Shughuli ya 3:** Maelezo dhahiri kutokana na picha katika matini

1. Panga na uandike vidokezo utakavyotumia kuandika insha ya masimulizi kuhusu picha za shughuli ya 2.
2. Andika daftarini insha ya masimulizi kutokana na vidokezo ulivyoandika.
3. Mpe mwalimu insha yako aisahihishe.
4. Andika nakala safi ya insha baada ya kusahihishwa.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Changamkia

Mkiwa wawiliwawili, tafuteni picha za vitu na matukio mbalimbali. Chezeni mchezo wa kuonyeshana kwa zamu picha mlizozipata huku mkitoleana masimulizi kuzihusu.

### Tembea na majira

1. Chagua picha moja kutoka zoezi la changamkia.
2. Tumia kifaa cha kidijitali:
   (a) Kuandaa vidokezo kuhusu picha hiyo.
   (b) Kuandika insha ya masimulizi inayohusu picha hiyo.
   (c) Msambazie mwalimu wako insha hiyo kupitia baruapepe ili aisome na kutoa maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako insha ya masimulizi uliyoandika daftarini au kidijitali.
2. Mwombe akupe maoni yake.

## D. SARUFI

### Aina za vitenzi

### Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi

### Kichocheo

Kuna tofauti gani kati ya vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi?

**Shughuli ya 1:** Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi

1. Mkiwa wawiliwawili:
   (a) Igizeni vitendo vifuatavyo kwa zamu:
      (i) ruka
      (ii) tembea
      (iii) cheza
      (iv) cheka
      (v) andika.
   (b) Soma sentensi zifuatazo:
      (i) Mumi alikuwa anaruka.
      (ii) Lufi angali anatembea.
      (iii) Dama aliweza kucheka.
      (iv) Kepa aliwahi kucheza kandanda.
      (v) Mashindano ya muziki yangali yanaendelea.
   (c ) Je, ni maneno gani yanayoonyesha vitendo maalum vilivyofanywa katika sentensi ulizosoma? Mweleze mwenzako.

(d) Je, ni neno gani linalotumiwa kabla tu ya kitendo kuwezesha kueleza kitenzi katika kila sentensi ulizosoma?

(e) Je, vitenzi vikitanguliwa na maneno kama vile; **alikuwa, angali, aliweza, aliwahi** na **ilibidi** huitwaje? Jadilini.

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa:

1. Kitenzi kikuu hupatikana katika sentensi na ndicho hutoa dhana au wazo kuu katika sentensi hiyo. Kitenzi hiki hutangulizwa kwa kitenzi kingine. Huwa cha pili katika mfuatano wa vitenzi viwili kwenye sentensi moja. Mfano ni; Mtoto alikuwa akilia kwa sauti ya juu. Neno **akilia** ndicho **kitenzi kikuu**.
2. Kitenzi kisaidizi husaidia kitenzi kikuu kufanikisha wazo kuu. Huandamana na kitenzi kikuu kutoa taarifa kamili. Huwa **cha kwanza** katika msururu wa vitenzi. Huchukua viambishi awali vya nafsi, ngeli, wakati na hali. Mfano ni; Mtoto alikuwa akilia kwa sauti ya juu. Neno **alikuwa** ndicho **kitenzi kisaidizi**.

2. (a) Nakili daftarini kifungu kifuatacho:

Marita alitaka kukimbia alipoisikia sauti ya radi. Mwalimu wake alikuwa amesimama karibu na darasa lao. Mwalimu aliweza kumwona. Alimsimamisha. Alitaka kumtuliza ili asiogope sana. Akamwambia, "Marita, umesahau shule yetu ni salama. Tuliwaeleza kuwa imewekwa vidhibiti radi." "Asante mwalimu kwa kunikumbusha. Itabidi niwakumbushe wenzangu."

(b) Pigia mstari vitenzi vikuu katika kifungu ulichonakili daftarini.

(c) Dondoa vitenzi visaidizi na uviandike daftarini.

## Shughuli ya 2: Matumizi ya vitenzi vikuu na visaidizi ipasavyo katika matini

Tunga sentensi kumi ukitumia vitenzi vikuu mbalimbali pamoja na vitenzi visaidizi vifuatavyo:

kuwa, weza, wahi, kuja, -ngali, bidi.

**Changamkia**

Andika kifungu kuhusu usalama shuleni ili uwasomee wanafunzi wenzako. Tumia vitenzi visaidizi na vitenzi vikuu katika kifungu utakachoandika.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kupiga chapa kifungu ulichoandika katika sehemu ya changamkia.
2. **Koleza rangi** vitenzi vikuu kwenye kifungu hicho.
3. Weka katika *italiki* vitenzi visaidizi kwenye kifungu hicho.
4. Mwonyeshe mwalimu wako kazi uliyoandika ili akupe maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwonyeshe mzazi au mlezi wako kazi uliyofanya kuhusu vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi daftarini.
2. Mwombe akupe maoni yake.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

**Tatua**

Andika maelezo mafupi kudhihirisha jinsi unavyolinda usalama wako njiani. Msomee mzazi ili atoe maoni yake.

# 7 KUHUDUMIA JAMII SHULENI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza kwa ufahamu

### Kichocheo

1. Ni mambo gani yanayokusaidia kupata ujumbe vizuri unaposikiliza habari fulani?
2. Je, kusikiliza kwa makini kuna faida gani?

**Shughuli ya 1:** Ujumbe katika ufahamu wa kusikiliza

1. (a) Tazama picha hizi:

Picha ya kwanza



Picha ya pili



(b) Unaona nini katika picha ya kwanza?
(c) Unaona nini katika picha ya pili?
(d) Eleza tofauti iliyopo kati ya unachoona katika picha ya kwanza na ya pili.

2. Msikilize mwalimu kwa makini akikusomea kifungu cha ufahamu kisha ujibu maswali.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Maswali:**

(a) Kwa nini watu huenda shuleni?
(b) Elimu hupatikana wapi?
(c) Jamii ya shule ni gani?
(d) Shule huhudumia jamii vipi?
(e) Wanajamii wanaifaidi shule vipi?

3. Jadili na mwenzako ujumbe katika kifungu cha ufahamu ulichokisikiliza.

### Shughuli ya 2: Maana ya msamiati ulio katika ufahamu wa kusikiliza

1. Sikiliza tena ukisomewa kifungu cha ufahamu.
2. Ukiwa na mwenzako:
   (a) Elezeni maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu ulichosomewa.
      (i) thamani
      (ii) anuwai
      (iii) washikadau
      (iv) mikakati
      (v) Juma la huduma
      (vi) maendeleo endelevu.
   (b) Tumieni kamusi kutafuta maana ya maneno katika shughuli ya 2(a).

### Shughuli ya 3: Ujumbe kutokana na ufahamu wa kusikiliza

1. Ukiwa na mwenzako, jibu maswali haya:
   (a) Unafikiri ni kwa nini mwandishi alitumia methali, 'samaki mkunje angali mbichi', katika kifungu ulichosikiliza?
   (b) Kulingana na kifungu, 'ukielimisha mtoto umeelimisha jamii nzima'. Eleza ukweli wa maneno haya.
   (c) Eleza faida za ushirikiano wa shule na wanajamii.

**Changamkia**

Mwombe mwenzako akusomee kifungu kifupi cha ufahamu huku ukisikiliza kwa makini kisha akuulize maswali.

### Tembea na majira

Sikiliza habari ikisomwa katika redio au televisheni. Mweleze mwenzako ujumbe wa habari uliyosikiliza.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi kuhusu habari uliyosikiliza kwenye redio au televisheni.

## B. KUSOMA

### Ufupisho

**Kichocheo**

1. Umewahi kupewa ujumbe gani kwa njia ya ufupi?
2. Unaondoa nini katika habari ili kuitoa kwa ufupi?

**Shughuli ya 1:** Ufupisho

1. (a) Tazama picha hii:




(b) Mweleze mwenzako unachoona katika kiwambo cha televisheni.
(c) Jadili na mwenzako kuhusu habari kwenye kiwambo cha televisheni.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa habari inaweza kuwasilishwa kwa maneno machache. Huo ndio ufupisho wa habari.

**Shughuli ya 2:** Habari kuu za aya

1. Soma kifungu hiki.

Elimu barani Afrika imekuwepo kwa miaka na mikaka. Kabla ya majilio ya wamishenari, watoto walipata mafunzo yao nyumbani. Nyanya na babu walikuwa na nafasi kubwa katika kuwaelekeza na kuwafunza watoto. Elimu hii haikuwa imeratibiwa lakini wanajamii walipata mafunzo kuhusu masuala yote ya maisha. Elimu kuhusu kilimo, biashara, dini, uzazi na ndoa ilitolewa.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

Aidha, ulikuwa wajibu wa kila mwanajamii kuhakikisha kuwa kuna maadili na nidhamu.

Wamishenari walianzisha shule barani Afrika na kubadili elimu. Elimu ya wamishenari ilichukua mkondo tofauti na ile ya Mwafrika. Elimu ya wamishenari ilikuwa na urasmi na iliendelezwa katika shule. Mwanzoni, ni Waafrika wachache tu waliteuliwa kujiunga na shule hizo.

Elimu ya shule ilimsaidia Mwafrika kugundua hila za mkoloni. Alianzisha harakati za kupigania uhuru. Hatimaye, nchi za Kiafrika zilijikomboa. Ukombozi huu umesaidia nchi za Kiafrika kujitegemea kijamii, kisiasa na kiuchumi. Si hayo tu, elimu imeendelea kuwasaidia wanajamii kutambua na kuheshimu haki zao za kibinadamu.

Elimu ya shule hufungua akili za mtu, kupanua mawazo na mtazamo wake wa maisha. Jamii huwa na sura mpya zipatapo wataalamu na mafundi mbalimbali kama vile walimu, wasusi, wafanyabiashara, mahakimu, wahandisi na wakulima. Elimu hii huwafanya watu kuwa na maono na matarajio mbalimbali ya maisha yao ya baadaye. Elimu huchochea ndoto za watu katika maisha. Ndoto hizi hupandwa na kupaliliwa katika shule kupitia mafunzo, ushauri na vielelezo.

Siku hizi elimu ya shule inapatikana kwa njia nyingi. Njia mojawapo ni ya kiteknolojia. Ujuzi na maarifa mengi yanapatikana katika mitandao rasmi na isiyo rasmi. Mtu anaweza kupata mafunzo na kufuzu kwa njia ya teknolojia ya habari na mawasiliano, yaani TEKNOHAMA.

**Maswali:**

1. Ukiwa na mwenzako andikeni sentensi moja kuhusu kila aya ya kifungu mlichosoma kisha kila mmoja aseme alichoandika.
2. Muombe mwalimu kutoa maoni kuhusu mlivyofupisha aya nzima kwa sentensi moja.

### Shughuli ya 3: Kufupisha kifungu

1. Unganisha sentensi ulizoziandika kutokana na kila aya katika shughuli ya 2 kwa mpangilio ufaao.
2. Msomee mwenzako kifungu cha ufupisho ulichoandika kutokana na sentensi ulizounganisha. Mwombe akutolee maoni yake.
3. Andika nakala safi ya ufupisho kwa kuzingatia maoni uliyopewa.
4. Mwasilishie mwalimu nakala safi ya ufupisho wako ili akusahihishie.

**Changamkia**

Soma kifungu katika gazeti la Kiswahili. Andika habari ulizosoma kwa ufupi.

### Tembea na majira

1. Ukitumia kifaa cha kidijitali andika upya ufupisho ulioandika katika sehemu ya changamkia.

2. Hifadhi ufupisho huo kidijitali kwa madhumuni ya kuurejelea baadaye.

**Shirikisha mzazi au mlezi**
Msomee mzazi au mlezi wako ufupisho ulioandika daftarini ili atoe maoni yake.

## C. KUANDIKA

### Insha za kubuni — Maelezo

**Kichocheo**
1. Je, ni jambo gani ambalo umewahi kumweleza mtu?
2. Ni lugha ya aina gani uliyotumia ili kuwasilisha picha kamili?

**Shughuli ya 1:** Maana ya insha ya maelezo

1. (a) Soma kifungu kifuatacho:

KUJIKINGA DHIDI YA UGONJWA WA KORONA

Ugonjwa **hatari** wa korona ni ugonjwa wa **kuambukiza**. Kuna njia mbalimbali za **kujikinga** kutokana na ugonjwa wa korona. Njia mojawapo ni kuvaa maski. Tunashauriwa kuvaa maski safi na inavyostahili. Pia, maski ivuliwe kwa njia inayofaa.

Mtu anaweza kujikinga dhidi ya ugonjwa wa korona kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji **safi** mara kwa mara. Sabuni huua **virusi** vya korona. Kukaa **mbali** na mwenzako ni njia nyingine ya kujikinga kutokana na maradhi ya korona. Wataalam wanahimiza watu kila uchao kukaa umbali wa mita moja na nusu au zaidi hasa wakati wa **mkurupuko** wa ugonjwa huu.

**Chanjo** dhidi ya ugonjwa wa korona imethibitishwa kuwa ni njia mwafaka ya kupambana vilivyo na makali ya korona.

**Maswali:**

(b) Je, kifungu ulichosoma kinatoa taarifa kuhusu nini? Mweleze mwenzako.

(c) Ukiwa na mwenzako elezeni maana ya insha ya maelezo.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa insha ya maelezo ni insha ambayo inatoa taarifa kuhusu kitu au jambo.

**Shughuli ya 2:** Msamiati ufaao katika kutoa maelezo

1. Ukiwa na mwenzako, elezeni:
   (a) Ni maneno gani yaliyotumiwa katika kifungu ulichosoma ambayo yanahusu magonjwa?
   (b) Ni maneno gani yaliyotumiwa kushawishi watu kujikinga?

2. Taja vivumishi na vielezi ambavyo vimetumika katika kifungu **'Kujikinga dhidi ya ugonjwa wa korona'**.

**Shughuli ya 3:** Umuhimu wa msamiati ufaao katika insha ya maelezo

Ukiwa na mwenzako, elezeni umuhimu wa kutumia msamiati unaofaa kulingana na mada ya insha ya maelezo.

**Shughuli ya 4:** Matumizi ya msamiati ufaao kwa ufasaha katika kuandika insha ya maelezo

1. (a) Mshirikishe mwenzako kuorodhesha msamiati unaofaa kuandika insha ya maelezo kuhusu jinsi shule yako inavyohudumia jamii.
   (b) Andika insha ya maelezo ukitumia msamiati ufaao kupasha habari, kuburudisha na kushawishi.
2. Msomee mwenzako insha ya maelezo uliyoandika. Mwombe akupe maoni yake kuhusu maneno uliyotumia.
3. Iandike upya insha yako ukizingatia maoni uliyopewa na mwenzako.
4. Iweke nakala safi ya insha yako kwenye potifolio na umpe mwalimu ili atoe maoni yake.

**Changamkia**

1. Chagua mada uipendayo na uandike insha ya maelezo.
2. Ukitumia matini mbalimbali, fanya utafiti kuhusu vigezo muhimu vya insha ya maelezo.
3. Andika vigezo hivyo mkiwa katika kikundi.
4. Andika insha ukitumia vigezo mlivyojadili.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika upya insha kuhusu mada uliyoichagua.
2. Tumia msamiati ufaao kama vile nomino, vivumishi na vielezi katika kutoa maelezo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi wako insha uliyoandika ili akupe maoni yake.

## D. SARUFI

### Aina za vitenzi – Vitenzi vishirikishi

### Kichocheo

1. Ni aina gani ya maneno ambayo huelezea kufanyika kwa kitendo?
2. Kuna aina gani za vitenzi?

## Shughuli ya 1: Vitenzi vishirikishi

1. (a) Soma kifungu kifuatacho:

Sungura, Fisi, Tumbili na Kobe **ni** wanafunzi wa Shule ya Upili ya Mwituni. Huko **ndiko** wanakokwenda shule kila siku. Siku moja Sungura alijificha na kwenda kula miwa ya jirani yao Bwana Nyati. Nyati alimlalamikia Mwalimu Simba kwa kusema, "Wanafunzi wako **ndio** wanaopitia shambani mwangu wakila miwa."

Mwalimu Simba aliwaita wanafunzi wote na kuwakanya. Kobe alimshuku Sungura **ndiye** mwizi wa miwa. Aliamua kumtega Sungura. Aliona miwa miwili iliyokuwa imekomaa vizuri. Alijua bila shaka Sungura angeitamani miwa hiyo. Kobe aliipaka miwa hiyo gundi ikametameta. Alijificha kwenye miwa. Punde Sungura alifika. Aliangalia huku na kule. Alijisemea, "**Si** kawaida kupata miwa ya kupendeza kama hii. Lazima ni mitamu kama asali. Hapa **ndipo** pahali pangu."

Sungura aliushika muwa mmoja ili auvunje. Mkono wake wa kulia ukanata. Alishika muwa wa pili kwa mkono wa kushoto, ukanata. Alilia kwa sauti. Sauti ilisikika kwa mbali. Kobe alijitokeza na kushangaa, "Kumbe Sungura **ndiwe** mwizi wa miwa ya Bwana Nyati? Kwa hakika siku za mwizi ni arubaini." Nyati aliwasili mara moja. Sungura alijua **yu** mashakani. Nyati alimwangalia Sungura kwa macho makali. Sungura alitetemeka kwa uoga na aibu. Alimwomba Nyati msamaha. Aliahidi kumpandia Nyati miwa mingine. Nyati alimsamehe Sungura kwa masharti makali.

**Swali:**

(b) Maneno yaliyokolezwa ni aina gani ya vitenzi? Mweleze mwenzako.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa vitenzi vishirikishi ni maneno ambayo hushirikisha mtu au kitu na hali au tabia fulani. Mifano ni kama vile: **ni**, **si**, **yu**, **ndiye**, **ndio**, **ndipo**, **ndiko** na **ndiwe**.

2. Mkiwa katika kikundi, tambueni vitenzi vishirikishi vilivyotumika katika sentensi hizi:
   (a) Shule yetu i karibu na kituo cha polisi.
   (b) Pale ndipo pachafu.
   (c) Mwanafunzi angali safarini.
   (d) Tuta hilo ndilo zuri.
   (e) Yeye si mbishi, ni mtiifu wa sheria.
   (f) Ateyo yu mwenye afya.
   (g) Ziwa hili li miongoni mwa rasilimali za nchi yetu.
   (h) Ushirikiano kati ya shule na jamii u wa kiwango cha juu.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

(i) Hawa ndio wawakilishi wetu katika maonyesho ya kilimo ya kitaifa.
(j) Vigae vile ndivyo vyao.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya vitenzi vishirikishi katika matini

1. (a) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vishirikishi vifuatavyo:
    (i) ni
    (ii) ndicho
    (iii) li
    (iv) u
    (v) i
    (vi) yu
    (vii) ndiye.
   (b) Msomee mwenzako sentensi ulizotunga ili akupe maoni yake.
2. (a) Tunga kifungu kifupi daftarini mwako kuhusu kuhudumia jamii shuleni. Tumia vitenzi vishirikishi.
   (b) Wasilisha kifungu ulichotunga kwa mwalimu ili asahihishe na kukupa maoni yake.

**Changamkia**

Rejelea vitu na hali katika mazingira yako na utunge sentensi ukitumia vitenzi vishirikishi. Nakili sentensi hizo daftarini.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika upya sentensi ulizonakili daftarini.
2. **Koleza rangi** vitenzi vishirikishi ulivyotumia katika sentensi hizo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizotunga na kuziandika daftarini ili akupe maoni.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

**Tatua**

Shule yenu imeathiriwa pakubwa na tatizo la mbu. Pendekeza mambo ambayo mnaweza kufanya kutatua tatizo hilo.

# 8 ULANGUZI WA BINADAMU

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kuzungumza ili kupasha habari

### Kichocheo

1. Je, ni habari gani muhimu ambazo umewahi kupashwa kwa njia ya mazungumzo?
2. Je, aliyekupasha habari hizo alitumia njia zipi?

**Shughuli ya 1:** Maana ya kuzungumza ili kupasha habari

1. (a)Tazama picha hizi:


(a)


(b)

   (b) Eleza mwenzako unaona nini katika kila picha.
   (c) Unafikiri ni picha gani inayoonyesha kuwa mzungumzaji anapasha wasikilizaji wake habari? Mweleze mwenzako.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa kuzungumza ili kupasha habari ni mazungumzo yanayotoa ujumbe kuhusu kitu, mada au jambo fulani.

**Shughuli ya 2:** Aina za kuzungumza ili kupasha habari

1. Sikiliza mfano wa kuzungumza ili kupasha habari ambao mwalimu atawasilisha.
2. Kuzungumza ulikosikiliza kulihusu nini? Mweleze mwenzako.
3. Mwambie mwenzako kinachojitokeza katika kuzungumza ulikosikiliza.
4. Ni tofauti gani zilizopo katika ujumbe wa kuzungumza ili kupasha habari ulikosikiliza? Jadili na mwenzako.
5. Umetambua aina ngapi za kuzungumza ili kupasha habari?
6. Ukiwa na mwenzako, jadili aina zifuatazo za kuzungumza ili kupasha habari na jinsi zinavyoweza kutumiwa kupasha habari:
   (a) hotuba
   (b) majadiliano
   (c) mahojiano
   (d) mihadhara
   (e) mafunzo shuleni
   (f) semina.

**Shughuli ya 3:** Vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza ili kupasha habari

1 (a) Mkiwa katika kikundi, igizeni mazungumzo haya:

**Afisa:** Hamjambo wanafunzi?

**Wanafunzi:** (*Kwa pamoja*) Hatujambo mgeni wetu. Karibu. (*Mgeni anasonga hatua chache kwenye ukumbi ili kuwakaribia wanafunzi.*)

**Afisa:** Asanteni sana. Jina langu ni Tofa Biba. Mimi ni afisa wa masuala ya watoto kutoka Kituo cha Salmini. Nimepata mwaliko wa mwalimu wenu kuja kuwazungumzia kuhusu ulanguzi wa watoto. Siku hizi, watoto wanachukuliwa na watu wasio na nia njema. Watoto hao mara nyingi wanakwenda kutumikishwa. Wanaowachukua hutumia mbinu mbalimbali kama vile kuwateka nyara, kuwadanganya, kuwaahidi maisha mazuri na hata kuwapa zawadi za kuvutia. Wengine huwahadaa kwa kuwapa vitu vidogo vidogo kama vile pipi. Ulanguzi huu wa watoto umeenea sana. Jambo hili limefanya idara yetu kujitolea vilivyo kukomesha kitendo hiki kiovu. Leo nimefika hapa ili kutoa habari zitakazowasaidia msiingie katika mtego wa walanguzi. Wanafunzi wapendwa, ni vizuri kutahadhari kabla ya hatari. Je, kuna yeyote mwenye swali kuhusiana na habari nilizowapasha?

(*Wanafunzi kadhaa wanainua mikono. Afisa anamchagua mwanafunzi wa kwanza.*)



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Mwanafunzi 1:** Naomba kuuliza, nitawezaje kuwatambua walanguzi hao?

**Afisa:** Hilo ni swali zuri sana. Walanguzi wanaweza kuwa watu unaowajua au usiowajua. Waovu hao hawataki kuonekana wakizungumza na wewe hadharani, huwa na wasiwasi mkuu, huonyesha urafiki wa upesi na jambo kuu zaidi ni ukarimu wao kwako ni wa kupita kiasi. Kwa mfano, wanaweza kutaka kukubeba kwa gari lao au kukuhadaa kuwa watakununulia zawadi yoyote utakayopenda. Wengine watataka kujua mambo mengi kukuhusu. Wanaweza kukuuliza jina lako, la mzazi, makao yenu na hata unakokwenda shule. Kuna walanguzi ambao huwa wametafiti mambo ya maisha yako na kukupatia habari za kweli kukuhusu.

(*Wanafunzi wanaonekana kushangazwa na maelezo ya Afisa.*)

**Mwanafunzi 1:** Asante sana Afisa kwa maelezo ya kina.

**Mwanafunzi 2:** Je, nikikutana na walanguzi hao nikiwa peke yangu nitafanyaje?

**Afisa:** Aha! Tumia mbinu yoyote ile kujiokoa. Mbinu hizo ni kama kupiga mayowe, kukimbia na kupiga firimbi kama unayo ili kuteka makini ya watu waje kukuokoa. Ni muhimu sana kuepuka maeneo yaliyojitenga. Je, kuna mwingine aliye na swali?

*(Wanafunzi wote wanaonekana kuridhika na maelezo ya Afisa.)*

Naona nimejibu maswali ambayo wengi wenu wangeyauliza. Asanteni kwa kunisikiliza. Kwaherini.

**Wanafunzi wote:** Kwaheri ya kuonana.

**Maswali:**

(b) Jibu ukiwa na mwenzako:

(i) Kichwa cha mazungumzo haya kinaweza kuwa gani?
(ii) Je, kuna ukweli upi katika mazungumzo mliyoyaigiza?
(iii) Lugha iliyotumika katika mazungumzo mliyoyaigiza ina sifa gani?
(iv) Unafikiri mwasilishaji alijitayarisha vipi ili atoe mazungumzo hayo?

**Shughuli ya 4:** Kupasha habari kwa kutumia vipengele vifaavyo vya mazungumzo ya kupasha habari

1 (*a*) Mkiwa katika kikundi, chagueni mada mtakayoandalia kuzungumzia ili kupasha habari. Kwa mfano, zungumzeni kuhusu namna ya kulinda usalama wenu mkiwa nje ya shule.

(b) Jadilini vipengele mtakavyotumia kuandaa mfano wa kuzungumzia ili kupasha habari kuhusu mada mliyoichagua.

(c) Andaeni mfano wa kuzungumzia ili kupasha habari kuhusu mada mliyoichagua.

(d) Igizeni mazungumzo ya kupasha habari mliyoyaandaa. Mwalimu atawapa maoni yake baada ya kuigiza kwenu.



Kimeidhinishwa na KICD

**Changamkia**

1. Sikiliza au tazama mazungumzo ya watu wanaopasha habari kupitia redio au televisheni na vifaa vingine vya kidijitali.
2. Yaigize mazungumzo hayo mbele ya kioo au mbele ya wenzako au katika kikundi ili kujifunza kufanya mazoezi ya kuzungumza ili kupasha habari.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kunasa mfano wa kuzungumza ili kupasha habari wasilisha mbele ya wenzako.
2. Hifadhi mazungumzo hayo ili uyarejelee wakati wa kudurusu.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Wasilishia mzazi au mlezi wako mazungumzo uliyoyanasa na kuhifadhi katika kifaa cha kidijitali ili ayasikilize na akupe maoni yake.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa kina

### I. Mandhari

### Kichocheo

Ni mazingira gani ya matukio yaliyokuvutia katika vitabu vya hadithi ambavyo umewahi kusoma?

**Shughuli ya 1:** Maana ya mandhari katika fasihi

1. (a) Ukiwa na wenzako zungumzieni kuhusu mazingira ya picha hizi:


(a)


(b)


KICD Kimeidhinishwa na KICD




(b) Jibuni maswali haya:

(i) Watoto walio kwenye picha (a) wako kwenye mazingira gani?

(ii) Watoto walio kwenye picha (b) wanaonekana wakiwa wapi?

(iii) Polisi katika picha (c) wako kwenye eneo gani?

(iv) Simba na wanyama wenzake wanaonekana wakiwa sehemu gani?

(c ) Tumia kamusi kutafuta maana ya neno mandhari.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa mandhari ni mazingira au mahali ambapo matukio hutendekea au hutokea.

**Shughuli ya 2:** Mandhari mbalimbali ya novela

1. Shirikiana na mwenzako kujibu maswali yafuatayo mkirejelea novela iliyoteuliwa na mwalimu.
   (a) Wahusika wako mahali gani?
   (b) Ni vitu gani vinavyopatikana katika mazingira ya wahusika?
2. (a) Msomee mwenzako sehemu ya novela iliyoteuliwa na mwalimu.
   (b) Mweleze mwenzako kuhusu mandhari ya sehemu uliyomsomea.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 3:** Umuhimu wa mandhari ya novela

1. Ukiwa na mwenzako jibu maswali yafuatayo mkirejelea novela iliyoteuliwa na mwalimu:
   (a) Wahusika wamekuzwa wakiwa katika mandhari gani?
   (b) Je, mandhari katika novela yamekusaidia vipi:
      (i) kuelewa ujumbe
      (ii) kukumbuka hadithi
      (iii) kutambua sifa za wahusika
      (iv) kukuza hamu ya kuendelea kusoma novela?
2. Jadili umuhimu wa mandhari katika novela.

**Shughuli ya 4:** Maelezo mafupi kuhusu mandhari ya novela

1. Andika maelezo mafupi kuhusu mandhari ya novela uliyoisoma.
2. Msomee mwenzako maelezo hayo mafupi uliyoyaandika.
3. Mkielekezwa na mwalimu, muombe mwenzako akupe maoni yake.
4. Andika upya maelezo yako ukizingatia maoni ambayo umepewa na mwenzako.

**Changamkia**

Mweleze mwenzako kuhusu mandhari yaliyokupendeza zaidi katika novela uliyoisoma. Mweleze kuhusu picha uliyoipata akilini mwako kuhusu mandhari hayo.

### Tembea na majira

1. Ukitumia kifaa cha kidijitali, andika maelezo mafupi kuhusu mandhari ya novela uliyoisoma.
2. Hifadhi maelezo hayo katika kifaa cha kidijitali.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi wako kuhusu mandhari ya novela uliyosoma.

## II. Ploti

### Kichocheo

1. Je, ni matukio gani muhimu yaliyo katika novela uliyosoma?
2. Matukio uliyotaja yamefuatana vipi katika novela uliyoisoma?

**Shughuli ya 1:** Maana ya ploti katika fasihi

1. (a) Ukiwa na mwenzako eleza kinachotendeka kwenye picha hizi:



(b) Jibu maswali haya na mwenzako kuhusu matukio katika picha hapo juu shughuli ya 1(a) hadi (d):

(i) Watoto walio kwenye picha (a) wanafanya nini?
(ii) Unafikiri mtu kwenye picha (b) anawaita watoto kwa nini?
(iii) Je, unadhani ni jambo gani ambalo linamfanya mtu katika picha (c) kuwakimbiza watoto?
(iv) Unafikiri watoto katika picha (d) wanamwambia nini mwenye duka?

2. Msimulie mwenzako hadithi fupi ukirejelea matukio kwenye picha (a) hadi (d).



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa mfuatano wa matukio katika kazi ya fasihi kama vile novela huitwa ploti.

**Shughuli ya 2:** Ploti ya novela

1. Shirikiana na mwenzako:
   (a) Kutaja mfuatano wa matukio katika sehemu ya novela uliyoisoma.
   (b) Kuandika mfuatano wa matukio katika sehemu ya novela uliyoisoma.
2. Waeleze wenzako mfuatano wa matukio katika sehemu ya novela uliyoisoma.
3. Waombe wakupe maoni yao.

**Shughuli ya 3:** Umuhimu wa ploti katika novela

1. Jibu maswali yafuatayo ukiwa na wenzako katika kikundi:
   (a) Je, mfuatano wa matukio katika novela uliyosoma umekusaidia vipi:
      (i) kuelewa ujumbe?
      (ii) kukumbuka hadithi?
      (iii) kutambua sifa za wahusika?
      (iv) kukuza hamu ya kuendelea kusoma novela?
   (b) Ploti ina umuhimu gani katika novela?

**Shughuli ya 4:** Maelezo kuhusu ploti

1. Andika maelezo mafupi kuhusu ploti ya novela uliyoisoma.
2. Msomee mwenzako maelezo hayo mafupi uliyoyaandika.
3. Mkielekezwa na mwalimu, mwombe mwenzako akupe maoni yake.
4. Andika upya maelezo yako ukizingatia maoni ambayo umepewa na mwenzako.

**Changamkia**

Waeleze wenzako katika kikundi kuhusu matukio yaliyokuvutia sana katika novela uliyoisoma. Waeleze kwa nini yalikuvutia.

### Tembea na majira

1. Ukitumia kifaa cha kidijitali, andika maelezo mafupi kuhusu ploti ya novela uliyoisoma.
2. Hifadhi maelezo hayo katika kifaa cha kidijitali.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi wako kuhusu ploti ya novela uliyosoma.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

## C. KUANDIKA

### Viakifishi

### I. Kiulizi

**Kichocheo**

Kiulizi hutumiwa vipi katika maandishi?

**Shughuli ya 1:** Matumizi ya kiulizi

1. (a) Andika daftarini kifungu kifuatacho:

ULANGUZI WA BINADAMU

Je, umewahi kusikia kisa cha ulanguzi wa binadamu? Serikali yetu ya Kenya inapambana vikali na jinamizi hili. Siku moja dada yangu aliniuliza,

"Ulanguzi wa binadamu hutokea wapi?" Swali hilo lilikuwa gumu kwa kuwa hakuna mahali maalum pa ulanguzi.

"Ulanguzi unaweza kutokea popote pale na wakati wowote ule lakini wezi hao wa watu wanapenda mahali penye faragha." Nilimjibu dada yangu.

"Lo! Kwa hivyo hatuna usalama." Dada yangu alisema kwa woga.

"La hasha! Tunao usalama mikononi mwetu.Tunafaa kujilinda na kuwalinda wenzetu dhidi ya ulanguzi." Nilimwambia dada yangu.

Je, wewe unasaidia serikali vipi katika kupambana na jinamizi hili?

**Maswali**:

(b) Chorea mviringo alama ya kiulizi pale ilipotumika katika kifungu ulichonakili.

(c ) Mkiwa katika kikundi, waeleze wenzako matumizi ya kiulizi katika kifungu ulichonakili.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya kiulizi ipasavyo katika matini

1. Nakili daftarini sentensi zifuatazo:
   (a) Je, Sikukuu ya Mashujaa husherehekewa lini
   (b) Unaenda wapi
   (c) Rafiki yangu aliniuliza,"Unapenda mchezo gani"
   (d) Kwa nini ni muhimu kumsamehe mwenzako
2. Tumia kiulizi mahali panapofaa katika sentensi ulizonakili daftarini.

### II. Koma

**Kichocheo**

Je, koma hutumiwa vipi katika maandishi?

**Shughuli ya 1:** Matumizi ya koma

1. (a) Nakili daftarini sentensi zifuatazo:



KICD Kimeidhinishwa na KICD

(i) Vyakula vya protini ni kama vile maziwa, mayai, nyama na maharagwe.
(ii) Achanikaye kwenye mpini, hafi njaa.
(iii) Anwani yangu ni 209876, Nuru.
(iv) Kaka aliniambia,"Ni vyema kusema ukweli kila wakati."
(v) Nilimwandikia mjomba wangu barua, nikaweka mtajo:
**Kwa mpendwa mjomba,**

(b) Chorea mviringo koma katika sentensi ulizozinakili.

(c) Ukiwa katika kikundi, waeleze wenzako matumizi ya koma katika sentensi ulizonakili.

**Shughuli ya 2:** Kutumia koma ipasavyo

1. Ambatisha matumizi ya kiakifishi koma na mfano sahihi kwenye chati.

| Matumizi | Sentensi |
|---|---|
| (a) Kuandika mtajo | Sanduku la Posta,<br>0981287,<br>Niru. |
| (b) Kutenga vitu katika orodha | Juma alisema, " Nimefaulu kabisa kuwanasa walanguzi wote." |
| (c) Pumziko fupi | Kwa Mkurugenzi, |
| (d) Kutoa maelezo zaidi | 4,987,521 |
| (e) Kuandika anwani | Tulipogundua ametoweka, tulipiga ripoti kwa polisi. |
| (f) Kuandika tarakimu | Alinunua samaki, nyanya, vitunguu, chumvi na sukari. |
| (g) Katika usemi halisi | Mkuu wa Wilaya, Bi. Sera, amehakikisha watoto wako salama. |

2. Andika sentensi tano kuonyesha matumizi mbalimbali ya koma.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi matumizi ya koma uliyojifunza.

**Changamkia**

Tunga kifungu kifupi cha aya moja kuonyesha matumizi mbalimbali ya kiakifishi koma na kiulizi.

### Tembea na majira

Piga chapa kifungu ulichokitunga katika changamkia huku **ukikolezea wino** mahali ambapo viakifishi koma na kiulizi vimetumika.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

## D. SARUFI

### Ngeli na upatanisho wa kisarufi

### I. Ngeli ya A - WA

**Kichocheo**

Ni vitu gani katika mazingira yako vilivyo na majina yanayopatikana katika ngeli ya A - WA?

**Shughuli ya 1:** Nomino za ngeli ya A - WA

1. (a) Andika daftarini nomino za ngeli ya A - WA zilizo kwenye mwavuli ufuatao:




(b) Ukiwa na mwenzako soma shairi lifuatalo:

**Ulanguzi gonjwa baya**

Ulanguzi gonjwa baya, dada sema hadharani,
Limeenea Ulaya, hata kwetu kiamboni,
Mama baba bila haya, wote wamelilaani,
Ulanguzi gonjwa baya, hata kama ni wa nyani.

Ni jukumu letu sote, usalama kutetea,
Tushirikiane kote, tuwinde maharamia,
Tukikaa macho sote, hawawezi kuvamia,
Ni jukumu letu sote, viumbe kuwatetea.

(c) Andika daftarini nomino za ngeli ya A - WA zilizotumika kwenye shairi.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 2:** Viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya A – WA katika matini

Mkiwa wawiliwawili onyesheni viambishi vya upatanisho wa kisarufi katika sentensi hizi:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Kijana alichora picha ya kuvutia. | Vijana walichora picha za kuvutia. |
| 2. | Mlanguzi atachukuliwa hatua kali. | Walanguzi watachukuliwa hatua kali. |
| 3. | Samaki anacheza majini. | Samaki wanacheza majini. |
| 4. | Kasuku ametibiwa leo. | Kasuku wametibiwa leo. |
| 5. | Chura anaimba kwa sauti. | Vyura wanaimba kwa sauti. |

**Shughuli ya 3:** Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya A–WA

1. (a) Andika daftarini sentensi tano ukitumia nomino mbalimbali za ngeli ya A – WA.
   (b) Msomee mwenzako sentensi ulizoandika daftarini mwako.
2. (a) Andika daftarini kifungu kifupi ukitumia nomino mbalimbali za ngeli ya A – WA.
   (b) Msomee mwenzako kifungu ulichoandika.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kupiga chapa kifungu kifupi ulichoandika kuonyesha matumizi ya nomino mbalimbali za ngeli ya A – WA.
2. Weka katika *italiki* nomino za ngeli ya A – WA ulizotumia.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako kifungu ulizozipiga chapa ukitumia kifaa cha kidijitali.
2. Mwombe akupe maoni yake.

## II. Ngeli ya U – I

### Kichocheo

Ni vitu gani katika mazingira yako vilivyo na majina yanayopatikana katika ngeli ya U – I?

**Shughuli ya 1:** Nomino za ngeli ya U – I

1. (a) Tambua nomino za ngeli ya U – I katika mraba wa maneno ufuatao:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | T | A | R | O | O | M |
| K | S | D | E | A | V | K |
| E | B | M | U | W | A | O |
| B | M | K | U | K | I | N |
| E | T | K | U | K | I | O |
| H | A | I | M | T | I | D |
| C | A | J | P | T | E | B |
| M | L | A | N | G | O | S |

(b) Andika daftarini nomino ulizozitambua kwenye mraba.

**Shughuli ya 2:** Viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya U – I

1. Ukishirikiana na mwenzako pigia mstari viambishi vya upatanisho vya ngeli ya U – I katika sentensi zifuatazo:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | Mkebe una maji. | Mikebe ina maji. |
| (b) | Mlango umefungwa. | Milango imefungwa. |
| (c) | Mfuko umenunuliwa. | Mifuko imenunuliwa. |
| (d) | Mti umepandwa. | Miti imepandwa. |

**Shughuli ya 3:** Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U – I katika matini

1. (a) Ukiwa na mwenzako, tunga sentensi ukitumia nomino za ngeli ya U – I katika umoja.
   (b) Mwombe mwenzako kuzibadilisha ziwe katika hali ya wingi. Zingatieni upatanisho wa kisarufi.
2. (a) Ukitumia maneno ya ngeli ya U – I yasiyopungua sita, andika kifungu cha maneno sitini.
   (b) Pigia mstari nomino hizo pamoja na viambishi vya upatanisho wa kisarufi.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Tembea na majira

1. Piga chapa sentensi mlizotunga na mwenzako ukitumia kifaa cha kidijitali.
2. **Kolezea wino** nomino za ngeli ya U – I na viambishi vya upatanisho wake wa kisarufi.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizozipiga chapa ukitumia kifaa cha kidijitali.
2. Mwombe akupe maoni yake.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Tatua

1. Unapenda sana kuendesha baiskeli lakini huna. Jirani yako amekuwa akikuambia kuwa ana baiskeli ambayo angetaka kukupatia. Angetaka uende kwake kuichukua baiskeli bila kumwambia mtu yeyote. Je, ungefanya nini?
2. Tafiti nomino tano katika ngeli ya A - WA na U - I kisha uzitungie sentensi.

# 9 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA MAWASILIANO

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza kwa kina

**Kichocheo**

Ni maneno yapi unafahamu ambayo yana sauti **d** na **nd**?

**Shughuli ya 1:** Sauti **d** na **nd** katika silabi na maneno

| | |
|---|---|
| ba, bi, bu, bo, be | do, da, di, du, de |
| chu, chi, cha, cho, che | ndi, ndu, nde, nda, ndo |

Kadi za silabi

| | |
|---|---|
| doa | ndoa |
| dege | ndege |
| poda | ponda |
| duni | nduni |
| dume | ndume |
| dau | ndau |
| dimba | ndimba |
| dimu | ndimu |
| dago | ndago |
| dugu | ndugu |

Chati ya maneno

1. Ukiwa na mwenzako:
   (a) Tamkeni silabi kwenye kadi za silabi.
   (b) Tambueni silabi zilizo na sauti **d** na **nd** kutoka kwenye chati ya maneno.
   (c) Tamkeni maneno yaliyo kwenye chati na mtambue sauti **d** na **nd**.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya sauti **d** na **nd** ipasavyo ili kuzitofautisha kimatamshi katika silabi na maneno

1. Ukiwa na mwenzako mtamkie jozi la maneno yaliyo kwenye chati yenye sauti **d** na **nd** kwa sauti.
2. Mkiwa katika kikundi undeni vitanzandimi kwa kutumia jozi hizo za maneno.

**Changamkia**

Mkiwa wawiliwawili someni kwa sauti vitanzandimi mlivyoviunda huku mkisikiliza matamshi ya kila mmoja.

### Tembea na majira

1. Ukitumia kifaa cha kidijitali, jirekodi ukitamka vitanzandimi mlivyounda.
2. Mshirikishe mwenzako kusikiliza vitanzandimi ulivyovirekodi. Muombe akutolee maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Muombe mzazi au mlezi kusikiliza vitanzandimi ulivyoviunda.
2. Muombe akupe maoni kuhusu utamkaji wako.

## B. KUSOMA

### Ufahamu wa kifungu cha kushawishi

#### Kichocheo

1. Je, ni ujumbe gani wa kushawishi umewahi kupewa?
2. Ni nini kilichofanya ukashawishika na ujumbe huo?

**Shughuli ya 1:** Habari mahususi katika kifungu cha ufahamu

1.(*a*) **Soma kifungu kifuatacho**:

Tawa alizaliwa na kulelewa na wazazi wake kule Kita. Alijiunga na shule ya msingi huko huko. Tawa alikuwa na bidii za mchwa. Msukumo huu wa ndani kwa ndani ulitawala na kuelekeza maisha yake. Shuleni alikuwa mwepesi darasani. Si hivyo tu, alikuwa pia mwepesi wa kusaidia wenzake. Alijifunza maadili kutoka kwa walezi wake. Hili lilifanya apendwe na walimu pamoja na wanafunzi wenzake. Alikuwa na mlahaka mwema na kila aliyehusiana naye.

Siku moja wakati wa likizo ya muhula wa pili, Tawa alitumwa na mzazi wake kununua bidhaa sokoni. Alipokuwa anakaribia soko, aliona gari kubwa jeusi limeegeshwa kando ya barabara. Ndani kulikuwa na watu ambao walikuwa na darubini mikononi. Kila mmoja alikuwa na darubini yake ambayo ilielekezwa kwenye boma la mkazi mmoja aliyeitwa Haji. Tawa alishtuka na kusimama. Alikita macho walipokuwa. Alijificha ili asionekane. Miguu ikawa mizito. Alihisi joto na baridi kwa wakati mmoja.

'Lazima hapa pana tatizo!' alijiambia. Aliwaza na kuwazua. Alijiuliza maswali mengi kimoyomoyo. "Hawa ni kina nani? Mbona wana darubini? Wanaangalia nini kwa Haji? Ikiwa ni wageni wake mbona wasiende langoni wafunguliwe? Mbona gari limeegeshwa mbali upande ule mwingine? Nivunje safari au niendelee?" Tawa alipiga moyo konde na kuamua kuendelea na safari yake. Ujasiri fulani ukamwingia. Akapata nguvu mpya za kuendelea na safari.

Kabla ya kuondoka alichukua nambari ya usajili ya gari la watu hao. Alipita kwa kasi mahali hapo. Alielekea katika KITUO CHA POLISI CHA MAVUNO. Alikata kauli kwenda kuripoti yale ambayo aliyaona. Aliwaambia askari alishuku matendo ya waliokuwemo garini. Aliwapa nambari ya usajili wa gari hilo.

Askari hawakusita. Waliondoka mara moja kwenda kuwanasa majangili hao. Walipokaribia, majangili waliondoka kwa gari lao kwa kasi. Muda si muda ving'ora vilisikika hewani. Mlio wa ving'ora uliwavutia wanakijiji mahali hapo. Haji pia alifika hapo. Haji aliwatuliza wanakijiji ambao walikuwa wameghadhabishwa na kutoroka kwa majangili hao.

"Tulieni, tulieni, tulieni jamani! Msiwe na wasiwasi. Hapa kwangu nimeweka kamera za siri. Nina hakika kamera hizo zimewanasa watu hao waliokuwa hapa. Polisi watazikagua na kuzitumia kuwasaka."

Mkuu wa polisi aliyekuwepo alisema, "Wananchi msiwe na hasira. Ningependa kumpongeza Haji kwa kuziweka kamera za siri. Ninawaahidi kuwa teknolojia hii ni njia moja ya kulinda usalama wetu. Bila shaka watu hao watapatikana."

Uchunguzi wa polisi kupitia kamera za siri uliwawezesha kutambua na hatimaye kuwanasa watu hao.

**Maswali:**

(b) Ukiwa na mwenzako, jibu maswali yafuatayo:

(i) Nini kiliwasaidia polisi kuwanasa majangili?
(ii) Majangili walielekeza darubini zao wapi?
(iii) Jadilini sifa za Tawa jinsi zinavyojitokeza kwenye kifungu?
(vi) Gari la majangili lilikuwa la rangi gani?

2. Jadili na mwenzako mambo yanayokuongoza kudondoa habari mahususi katika kifungu.

### Shughuli ya 2: Maana ya msamiati na vifungu vya maneno katika kifungu cha ufahamu

1. Mkiwa katika kikundi:
   (a) Dondoeni maneno mageni yaliyotumika katika kifungu ulichokisoma.
   (b) Elezeni maana ya maneno hayo kama yalivyotumika katika kifungu ulichokisoma.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

(c) Tumieni kamusi kuthibitisha maana ya maneno yaliyotumika katika kifungu.

**Shughuli ya 3:** Maelezo ya habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi

Ukiwa na mwenzako:

1. Elezeni ujumbe katika kila aya ya kifungu mlichokisoma kwa sentensi moja moja.
2. Tumieni sentensi hizo kueleza habari za kifungu mlichokisoma kwa ufupi.

**Changamkia**

Chagua makala kwenye gazeti kuhusu matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mawasiliano. Soma makala hayo kisha udondoe habari muhimu. Eleza habari hizo kwa ufupi.

### Tembea na majira

Tumia kifaa cha kidijitali kuandika habari muhimu uliyosoma kuhusu matumizi ya vifaa vya kidijitali.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Muonyeshe mzazi au mlezi wako habari muhimu kuhusu matumizi ya vifaa vya kidijitali uliyoandika.
2. Muombe mzazi au mlezi wako akupe maoni yake.

## C. KUANDIKA

### Insha za kubuni — Masimulizi

### Kichocheo

Ni mambo yapi yaliyokuvutia uliposimuliwa kisa fulani?

**Shughuli ya 1:** Vipengele vinavyozingatiwa kujenga wazo katika insha ya masimulizi

1. Msimulie mwenzako kisa kifupi kuhusu siku yako ya kwanza shuleni katika Gredi ya 7.
2. **Soma kielelezo kifuatacho cha insha ya masimulizi**:

NGIRI NA WANAWE

Hapo zamani za kale paliondokea Ngiri na wanawe. Walipenda kula matunda ya mwituni yaliyoiva. Hata hivyo, tatizo kubwa lilikuwa namna ya kuyapata matunda hayo. Ngiri aliwaza na kuwazua ili apate utatuzi wa tatizo hilo.

Siku moja Ngiri na wanawe walimuona Ndovu na wanawe wakila maembe yaliyoiva kwa furaha. Ngiri alikwenda kumuuliza Ndovu siri ya kuangua matunda

yaliyoiva. Ndovu alisema, "Ndugu yangu, kuangua matunda ni rahisi sana. Mimi hushika shina la mti kwa mkonga wangu kisha hutingisha kidogo tu. Kusudi ni kuhakikisha tu nimeangua matunda kiasi yaliyoiva. Wajua lazima nihakikishe kuwa siangui matunda yote. Kuna leo na kuna kesho eti!" "Alah! Kumbe ni rahisi hivyo! Laiti ningekuwa na mkonga, pia ningewaangulia wanangu matunda." Ngiri alisema. "Huna mkonga lakini una akili. Akili ni mali itumie." Ndovu alimshauri Ngiri. Ndovu alimkaribisha Ngiri na wanawe kula maembe hadi shibe yao.

Ngiri na wanawe walimshukuru Ndovu na kwenda zao. Siku iliyofuata Ngiri aliuona mpera uliokuwa na mapera yaliyoiva. Alikumbuka nasaha za Ndovu. Alikimbia mbio na kugonga shina la mpera kwa kichwa chake. Mpera ulitingika na mapera yaliyoiva yakaanguka. Kwa bahati mbaya meno ya Ngiri yalikwama kwenye shina la mpera. Kumbe alikuwa amesahau kufunga kinywa alipogonga shina la mpera.

Ngiri alianza kujivuta kutoka kwenye shina la mpera huku akisaidiwa na wanawe. Kadri alivyoendelea kujivuta ndivyo meno yake yalivyoendelea kurefuka. Mwishowe Ngiri alijinasua lakini meno yake mawili ya kando yalichomoka na kuwa marefu kama pembe. Ngiri alifurahi kuwa alivumbua mbinu ya kuangulia wanawe matunda. Siku hiyo wanawe walikula mapera kwa furaha. Baadaye Ngiri aligundua kuwa pembe zake mpya zingemsaidia kupambana na adui. Alienda kwa Ndovu kumshukuru kwa ushauri wake mzuri.

**Maswali:**

3. Ukiwa na mwenzako, tambua vipengele vifuatavyo vya insha ya masimulizi uliyosoma:
   (a) utangulizi
   (b) mwili
   (c) hitimisho
   (d) mada inayozungumziwa.

### Shughuli ya 2: Vipengele vinavyojenga wazo kuhusu insha ya masimulizi

1. Shirikiana na mwenzako kujibu maswali yafuatayo kuhusu insha ya masimulizi uliyosoma katika shughuli ya 1.
   (a) Ipatie insha hiyo kichwa kingine kinachofaa kando na kile kilichotolewa.
   (b) Insha ya masimulizi ilihusu nini?
   (c) Insha hiyo ya masimulizi ilianza kwa njia gani?
   (d) Hoja zinajengwa vipi katika kila aya?
   (e) Insha inamalizika vipi?

### Shughuli ya 3: Kuandika insha ya masimulizi

1. Jadili na mwenzako vidokezo vya insha ya masimulizi utakayoandika kuhusu '**Safari ya ajabu**'.
2. Andika vidokezo mlivyojadili daftarini mwako.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

3. Andika insha hiyo ya masimulizi ukikuza wazo katika kila aya ipasavyo.
4. Wasomee wenzako insha hiyo darasani.
5. Waombe ili wakutolee maoni yao.

### Tembea na majira

Piga picha insha uliyoiandika daftarini kisha msambazie mwalimu wako kwa njia ya mtandao.

### Shirikisha mzazi na mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako insha ya masimulizi uliyoiandika kuhusu 'Safari ya ajabu'.
2. Mwombe akutolee maoni yake.

## D. SARUFI

### Ngeli na upatanisho wa kisarufi

### I. Ngeli ya KI - VI

#### Kichocheo

Ni vitu gani katika mazingira yako ya shuleni viliyo katika ngeli ya KI - VI?

**Shughuli ya 1:** Nomino katika ngeli ya KI - VI katika matini

1. (a) Soma maneno yaliyo kwenye chati.



(b) Ukiwa na mwenzako tambua maneno ya ngeli ya KI – VI kwenye chati hiyo.

2. Mshirikishe mwenzako kutaja vifaa vya shuleni vyenye majina yaliyo katika ngeli ya KI – VI.

**Shughuli ya 2:** Viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI – VI

1. (a) Soma sentensi zifuatazo:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (i) | Kifutio kilitumika kufuta maandishi. | Vifutio vilitumika kufuta maandishi. |
| (ii) | Kipakatalishi kitatumiwa kuhifadhi kazi ya mwanafunzi. | Vipakatalishi vitatumiwa kuhifadhi kazi za wanafunzi. |
| (iii) | Chumba cha mgeni kinafagiliwa. | Vyumba vya wageni vinafagiliwa. |
| (iv) | Kisa alichosimulia kilimvutia mwanafunzi. | Visa walivyosimulia viliwavutia wanafunzi. |
| (v) | Chombo cha mawasiliano kitanunuliwa. | Vyombo vya mawasiliano vitanunuliwa. |

(b) Ukiwa na mwenzako, tambueni viambishi vinavyowakilisha nomino za ngeli ya KI – VI katika sentensi mlizosoma.

2. (a) Andika daftarini sentensi ulizosoma katika jedwali. Piga mstari nomino na viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI – VI.

(b) Pigia mstari nomino na viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI – VI.

**Shughuli ya 3:** Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya KI – VI

1. Tunga sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia nomino zifuatazo. Zingatia upatanisho wa kisarufi.
   (a) kibanio
   (b) kizingiti
   (c) kiambaza
   (d) cheo
   (e) cherehani.
2. Msomee mwenzako sentensi ambazo umetunga.
3. Mkishirikiana na mwenzako onyesheni viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI – VI vilivyotumika katika sentensi ambazo umetunga.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Changamkia**

1. Chagua nomino zozote kumi katika ngeli ya KI - VI. Zitumie kutunga sentensi kumi tofauti kuonyesha upatanisho wa kisarufi wa ngeli hii ya KI - VI.
2. Wasomee wenzako sentensi ulizotunga ili wakupe maoni yao.

### Tembea na majira

Ukitumia kifaa cha kidijitali, piga chapa sentensi ulizotunga katika sehemu ya changamkia. **Koleza rangi** nomino na viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI - VI.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mwonyeshe na kumsomea mzazi au mlezi wako sentensi ulizotunga. Mwombe akutolee maoni yake.

## II. Ngeli ya LI - YA

### Kichocheo

Ni vitu gani katika mazingira yako ya shuleni vilivyo katika ngeli ya LI - YA?

**Shughuli ya 1:** Nomino za ngeli ya LI - YA

1. (a) Soma maneno yaliyo kwenye chati.

| | |
|---|---|
| jiwe | mawe |
| tawi | matawi |
| kilima | vilima |
| jina | majina |
| uovu | maovu |
| jembe | majembe |
| neno | maneno |
| ziwa | maziwa |
| jicho | macho |
| tunda | matunda |

(b) Ukiwa na mwenzako:
   (i) Tambua nomino za ngeli ya LI - YA kwenye chati ya 1(a).
   (ii) Jadilini kuhusu nomino za ngeli ya LI - YA mlizozitambua kwenye chati.
2. Mshirikishe mwenzako kutaja vifaa vya shuleni vyenye majina yaliyo katika ngeli ya LI - YA.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa nomino za ngeli ya LI - YA ni majina ya sehemu za mwili, matunda na vitu vinginevyo.

## Shughuli ya 2: Viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya LI - YA

1. (a) Soma sentensi zifuatazo:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| (a) | Tingatinga linatumia teknolojia ya kisasa kuvuna mpunga. | Matingatinga yanatumia teknolojia ya kisasa kuvuna mipunga. |
| (b) | Sikio lake limetibiwa. | Masikio yao yametibiwa. |
| (c) | Jibu lilisomeka vizuri kwenye kiwambo cha simu. | Majibu yalisomeka vizuri kwenye viwambo vya simu. |
| (d) | Gari litafungwa mlango kwa kiungambali. | Magari yatafungwa milango kwa viungambali. |
| (e) | Duka liliwekwa kamera ya siri. | Maduka yaliwekwa kamera za siri. |

(b) Ukiwa na mwenzako, tambueni viambishi vinavyowakilisha nomino za ngeli ya LI - YA katika sentensi mlizosoma.

2. (a) Andika daftarini sentensi ulizosoma katika jedwali.

(b) Piga mstari nomino na viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI - YA.

## Shughuli ya 3: Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI - YA

1. (a) Tunga sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia nomino zifuatazo. Zingatia upatanisho wa kisarufi.
   (i) shamba
   (ii) soko
   (iii) ua
   (iv) jokofu
   (v) tawi.

(b) Msomee mwenzako sentensi ambazo umetunga.

(c) Mkishirikiana na mwenzako onyesheni viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya LI - YA vilivyotumika katika sentensi ambazo umetunga.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Changamkia

(a) Chagua nomino zozote tano katika ngeli ya KI – VI na tano za ngeli ya LI – YA. Zitumie kutunga sentensi tofauti kuonyesha upatanisho wa kisarufi wa ngeli hii ya LI – YA.

(b) Wasomee wenzako sentensi ulizotunga ili wakupe maoni yao.

### Tembea na majira

1. Ukitumia kifaa cha kidijitali, piga chapa sentensi ulizotunga.
2. **Koleza wino** nomino na viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI - VI na LI - YA.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwonyeshe na kumsomea mzazi au mlezi sentensi ulizozipiga chapa katika kifaa cha kidijitali.
2. Mwombe akutolee maoni yake.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Jumuika na jamii

Mwalimu wenu mkuu amewaalika viongozi wa wanafunzi kutoka shule jirani kwa mkutano wa viranja shuleni kwenu. Mkutano utahusu kujadili njia za kidijitali ambazo zinaweza kutumiwa kudumisha nidhamu. Pendekeza njia mbalimbali za kidijitali ambazo zinaweza kutumiwa kudumisha nidhamu katika shule hizi.

# 10 KUJITHAMINI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### I. Nyimbo za kazi

**Kichocheo**

1. Je, unajua nyimbo gani?
2. Je, unajua nyimbo gani za kazi?

**Shughuli ya 1:** Maana ya nyimbo za kazi

1. (a) Sikiliza wimbo ufuatao ukiimbwa:

*Uzembe ndio hasimu wa ujenzi wa nchi,*
*Kwa kuwa ndio sababu hasa chanzo cha njaa.*
*Ewe mwenzi wangu kumepambazuka,*
*Chukua jembe na uma tukalime.*
*Pia wewe dereva kumepambazuka,*
*Huu ndio muda wako, wa kwenda kazi.*

*Uzembe,*
*Ndiye hasimu wa kujenga nchi,*
*Tujitenge, na uzembe tuijenge nchi.*

*Mwenzi wangu,*
*Kumekucha toka twende shamba,*
*Tujitenge, na uzembe tuijenge nchi.*

*Askari wee*
*Kumekucha kashike doria,*
*Tujitenge, na uzembe tuilinde nchi.*

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wimbo wa kazi huimbwa wakati wa kufanya kazi au kuwahimiza watu wapende kazi.

(b) Mweleze mwenzako ujumbe katika wimbo ambao umesikiliza ukiimbwa.

(c) Unafikiri wimbo kama huu huimbwa kwa nini? Mweleze mwenzako.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

## Shughuli ya 2: Mazingira ambamo nyimbo za kazi huimbwa

1. Imbeni wimbo huu darasani:

Mimi hapa ni mwalimu × 2
Niko ndani ya darasa × 2
Nitakupa kitabu kizuri,
Mwanafunzi soma kwa furaha.

Na mimi ni daktari × 2
Niko hapa hospitali × 2
Ninatibu wagonjwa vizuri,
Mwanafunzi soma kwa furaha.

Mimi nami ni mchuuzi × 2
Nimefika sokoni mapema × 2
Nauza matunda mazuri,
Maembe, ndizi hata na mapera.

2. Tajeni wafanyakazi wanaozungumziwa katika wimbo huu.
3. Elezeni mahali pa kazi palipotajwa.

## Shughuli ya 3: Ujumbe katika nyimbo za kazi

Ukiwa na mwenzako:

1. Imbeni wimbo wa kazi mliosikiliza katika shughuli ya 1.
2. Elezeni watu wanahimizwa kufanya nini katika wimbo huo?
3. Elezeni aina za kazi zilizotajwa katika wimbo huo.
4. Elezeni mambo ambayo wimbo huo unahimiza.

## Shughuli ya 4: Uwasilishaji wa nyimbo za kazi kwa kuzingatia hisia na ishara za mwili

1. Mwimbie mwenzako wimbo mmoja wa kazi.
2. Tumia ishara za mwili na uso kuonyesha hisia unapoimba.

**Changamkia**

1. Wasilisha wimbo wowote wa kazi mbele ya wenzako darasani.
2. Waombe wenzako kutoa maoni yao kuhusu wimbo uliowasilisha.

### Tembea na majira

Mwombe mwenzako kukunasa kwa kutumia kifaa cha kidijitali ukiimba wimbo wa kazi.

Iwapo huna kifaa cha kidijitali, imba mbele ya wenzako wakupe maoni kuhusu uimbaji wako.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwimbie mzazi au mlezi wako wimbo wowote wa kazi.
2. Tumia ishara za mwili na uso kuonyesha hisia unapoimba.
3. Mwombe akupe maoni yake kuhusu uimbaji wako.

## II. Nyimbo za dini

### Kichocheo

Je, unajua nyimbo gani za dini?

**Shughuli ya 1:** Maana ya nyimbo za dini

1. (a) Sikiliza wimbo ufuatao ukiimbwa:

Mungu yu mwema,
Mungu yu mwema,
Mungu yu mwema,
Yu mwema kwetu.

Yu mwema ametubariki,
Yu mwema ametushibisha,
Yu mwema ametupa nguvu,
Yu mwema kwetu.



(b) Mweleze mwenzako ujumbe katika wimbo ambao umesikiliza ukiimbwa.

(c) Unafikiri wimbo kama huu huimbwa kwa nini? Mweleze mwenzako.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wimbo wa shughuli ya 1 huimbwa wakati wa kumtukuza Mungu na katika shughuli za kidini.

**Shughuli ya 2:** Mazingira ambamo nyimbo za dini huimbwa

Mkiwa katika vikundi, zungumzieni kuhusu nyimbo za dini. Maswali yafuatayo yatawaongoza:

1. Ni kina nani ambao huimba nyimbo hizo?
2. Nyimbo za aina hiyo huimbwa mahali gani?



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 3:** Ujumbe katika nyimbo za dini

Ukiwa na mwenzako:

1. Imbeni wimbo wa dini mliosikiliza.
2. Tajeni anayesifiwa katika wimbo huo.
3. Elezeni sababu zinazofanya mliyemtaja kusifiwa.
4. Ni ujumbe gani unaopata kutokana na wimbo uliouimba?

**Shughuli ya 4:** Nyimbo za dini kwa kuzingatia hisia na ishara za mwili

Mwimbie mwenzako wimbo mmoja wa dini. Tumia ishara za mwili na uso kuonyesha hisia unapoimba.

**Changamkia**

1. Wasilisha wimbo wowote wa dini mbele ya wenzako darasani.
2. Waombe wenzako kutoa maoni yao kuhusu wimbo uliowasilisha.

### Tembea na majira

1. Mwombe mwenzako kukunasa unapoimba wimbo wa dini akitumia kifaa cha kidijitali.
2. Sikiliza wimbo ulionaswa kwenye kifaa cha kidijitali.
3. Hifadhi wimbo huo ili kuurejelea baadaye unapouhitaji.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwimbie mzazi au mlezi wako wimbo wowote wa dini.
2. Tumia ishara za mwili na uso kuonyesha hisia unapoimba.
3. Mwombe akupe maoni yake kuhusu uimbaji wako.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa kina — Wahusika

### Kichocheo

1. Je, unawakumbuka wahusika gani katika novela uliyosoma?
2. Ni mambo gani yanayokuwezesha kuwakumbuka wahusika katika novela uliyosoma?

**Shughuli ya 1:** Wahusika katika novela

1. Mkiwa katika kikundi, someni sehemu ya novela iliyoteuliwa na mwalimu.
2. Ukiwa na mwenzako:

   (a) Tajeni majina ya wahusika katika sehemu ya novela hiyo.

(b) Tajeni shughuli wanazofanya wahusika hao.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa wahusika ni viumbe ambavyo hutumiwa na mwandishi katika kazi ya fasihi. Wahusika wanaweza kuwa watu, vitu au wanyama.

## Shughuli ya 2: Sifa za wahusika katika novela

Mkiwa katika kikundi:

1. Zungumzieni kuhusu matendo ya wahusika katika novela mliyosoma.
2. Kutokana na matendo mliyozungumzia ya wahusika, tajeni sifa za wahusika hao.
3. Chagua nafasi ya mhusika katika novela uliyosoma uigize.
4. Andikeni sifa za mhusika uliyeigiza.
5. Waeleze wenzako sifa ulizoandika za mhusika uliyeigiza.

## Shughuli ya 3: Uhusiano kati ya wahusika katika novela

Wahusika katika novela uliyosoma wana uhusiano gani? Unaweza kutilia maanani uhusiano wa:

1. kiumri
2. ndoa
3. ujirani
4. kazi
5. tabia.

## Shughuli ya 4: Muhtasari wa sifa za wahusika katika novela

Ukiwa na mwenzako:

1. Andikeni kwa ufupi sifa za wahusika mbalimbali katika novela mliyoisoma.
2. Wasomeeni wenzenu kwa zamu darasani muhtasari wa sifa za wahusika katika novela mliyosoma.

## Shughuli ya 5: Mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika katika novela

1. Endelea kusoma novela ili uendelee kutambua matendo ya wahusika.
2. Jadili mafunzo yanayojitokeza kutokana na matendo ya wahusika katika novela hiyo.
3. Somea mwenzako mafunzo mliyojadili.

**Changamkia**

Je, umejifunza nini kutokana na matendo ya wahusika katika novela uliyosoma? Mweleze mwenzako.

### Tembea na majira

Tumia kifaa cha kidijitali kuandaa jedwali la kuonyesha sifa na mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika wa novela ulizosoma. Tumia mfano huu.

| | Anwani | Mwandishi | Mhusika | Sifa | Funzo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |

Iwapo huna kifaa cha kidijitali, chora jedwali hili daftarini kisha ulijaze.

Wasilisha kazi hii kwa mwalimu ili akupe maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi wako maelezo kwenye jedwali uliloandaa.

## C. KUANDIKA

### Barua ya kuomba msamaha

**Kichocheo**

1. Je, mambo gani ambayo yanaweza kukufanya uombe msamaha?
2. Je, unaweza kutumia njia gani kuomba msamaha?
3. Utazingatia nini unapoandika barua rasmi ya kuomba msamaha?

**Shughuli ya 1:** Umuhimu wa barua rasmi ya kuomba msamaha

Ukiwa na mwenzako:

1. Someni barua hii:

Shule ya Msingi ya Jiimarishe,
S.L.P. 03246-001,
MASOMONI.
11.01.2023

Bi. Zuru,
Shule ya Msingi ya Mlindeni,
S.L.P. 04326-001,
MASOMONI.

Kwa mwalimu wangu wa Gredi ya Saba,

KUH: KUKOSA KUHUDHURIA SHULE WIKI HII

Naandika barua hii ili kukuomba radhi. Samahani sikukujuza mapema kuwa sitaweza kuhudhuria shule wiki hii. Nimelazwa hospitalini baada ya kuumia mguu wakati wa wikendi nilipokuwa nikicheza.

Naomba uwaruhusu wenzangu katika kikundi chetu kuwasilisha mradi wangu kwa niaba yangu. Nakusihi pia unitumie kazi ya mazoezi kwa njia ya kidijitali nifanyie huku hospitalini nikiweza. Tafadhali tumia anwani ya baruapepe ya mzazi wangu chema442@gmail.com.

Nikimalizia, nakuomba uwajuze wenzangu kuhusu ajali hii iliyonifika. Wasalimie wote. Tutaonana wiki ijayo majaliwa.

Wako mwaminifu,

Moris Juma Kinabwa.

2. Zungumzieni sababu zilizomfanya Moris Juma Kinabwa kuiandika barua hii.
3. Jadilini umuhimu wa barua rasmi ya kuomba msamaha.

**Shughuli ya 2:** Ujumbe katika barua rasmi ya kuomba msamaha

1. Ukiwa na mwenzako:
   (a) Someni tena kielelezo cha barua rasmi ulichopewa.
   (b) Jibuni maswali haya:
      (i) Ni kwa nini Juma aliomba Bi. Zuru msamaha?
      (ii) Juma alikuwa na tatizo gani?
      (iii) Taja mambo ambayo Juma alimwomba Bi. Zuru amfanyie.
   (c) Andikeni majibu yenu kwenye daftari.

**Shughuli ya 3:** Vipengele vya kimuundo vya barua rasmi ya kuomba msamaha

1. Jadili na wenzako sehemu kuu za kuzingatia unapoandika barua rasmi ya kuomba msamaha. Maswali yafuatayo yatawaongoza:

(a) Anwani ya mwandishi wa barua uliyosoma ni ipi?
(b) Anwani ya aliyeandikiwa barua uliyosoma ni ipi?
(c) Barua hii inahusu nini?
(d) Ni mambo gani yanayozungumziwa katika barua hii?
(e) Sahihi iliyowekwa katika barua hii ni ya nani?

2. Andikeni majibu katika daftari.

**Shughuli ya 4:** Barua rasmi ya kuomba msamaha inayozingatia ujumbe, muundo na lugha ifaayo

1. Jadili na mwenzako kuhusu lugha inayofaa katika kuandika barua rasmi ya kuomba msamaha.
2. Umechelewa kurudi darasani baada ya kupewa ruhusa. Mwalimu wako amekuambia uandike barua rasmi ya kuomba msamaha. Andaa vidokezo vya barua rasmi ya kuomba msamaha utakayoandika.
3. Andika barua rasmi ya kuomba msamaha kwa kuzingatia ujumbe, muundo na lugha ifaayo. Rejelea vidokezo ulivyoandika ili kukuelekeza.
4. Msomee mwenzako barua yako ili akutolee maoni yake.
5. Tumia maoni ya mwenzako kufanyia insha yako marekebisho.

**Changamkia**

Wewe na rafiki yako mmechelewa kujiunga na wenzenu kwenye gwaride. Mmekutana na mwalimu mkuu akawaonya. Mmeona ni vyema mmwandikie barua rasmi ya kuomba msamaha. Mkiwa katika kikundi chenu, andikeni barua hiyo.

### Tembea na majira

1. Sambazieni wenzenu barua ambayo mmemwandikia mwalimu mkuu katika kikundi chenu kwa njia za kidijitali.
2. Waombeni wenzenu waitolee maoni. Iwapo huna kifaa cha kidijitali, andika barua hiyo na umwonyeshe mwalimu, mzazi au mlezi ili akutolee maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako barua mliyomwandikia mwalimu mkuu.
2. Mwombe mzazi au mlezi wako atoe maoni yake kuhusu barua hiyo.
3. Andika maoni ya mzazi au mlezi wako kwenye daftari lako ili yakusaidie kuimarisha uandishi wako katika siku za usoni.

## D. SARUFI

### Vinyume vya maneno

### I. Vinyume vya nomino

### Kichocheo

1. Je, unajua vinyume vya maneno gani? Mwambie mwenzako.

2. Mtajie mwenzako maneno mawili yenye vinyume ili akutajie vinyume vyake.

**Shughuli ya 1:** Kinyume cha maneno

1. Tazama picha hizi. Mwambie mwenzako unaona nini.




2. Mkiwa katika kikundi, tungeni sentensi kutokana na picha mlizotazama.
3. Mmetambua nini kuhusu sentensi hizo?

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa kinyume ni neno lenye maana inayopingana na maana ya neno lingine.

**Shughuli ya 2:** Vinyume vya nomino katika fungu la maneno

1. Ukiwa na mwenzako:
   (a) Chagua neno na kinyume chake kwenye kadi za maneno zifuatazo.




(b) Nakili maneno uliyochagua kwenye daftari lako.

2. Nakili mafungu haya ya maneno katika daftari lako. Pigia mstari nomino na kinyume chake katika kila fungu la maneno.

| | A | B |
|---|---|---|
| (a) | Ana ujasiri, aliwakomesha | mafisadi wenye uoga. |
| (b) | Hivyo basi, huzuni hutokea | haki ikikosekana nayo furaha huja haki ikipatikana. |
| (c) | Talanta yake ilimpa faida, akaepuka | hasara ya kupoteza muda wake kwa kuketi tu. |
| (d) | Mwenye shibe | hamjui mwenye njaa. |

3. Soma kifungu hiki cha hadithi.

Sungura alijidai mwerevu. Aliwaona wanyama wenzake kuwa wajinga sana. Hakujua kuwa pwagu anaweza kupata pwaguzi. Sungura alianzisha biashara ya kuwekea wanyama pesa benkini. Kobe alikuja kuweka pesa zake. Baada ya muda Kobe alienda kutoa hela kidogo. Sungura alimkataza Kobe kutoa pesa kidogo.

Alisema,"Huwezi kutoa hela chache hivyo. Hatutaki maskini. Hii ni benki ya matajiri," Sungura alisema kwa ukali.

"Sawa. Wacha ukali. Upole utakufaa. Sipendi ubishi. Nitatoa pesa zangu zote. Naomba unihesabie," Kobe alisema kwa unyenyekevu.

Sungura aliangalia akaunti ya Kobe. Alishangaa kuona kuwa Kobe alikuwa na mabilioni ya pesa. Alianza kumuomba Kobe msamaha kwa ujeuri wake.

"Usinione hivi. Najiamini na kujithamini ndugu yangu. Uvumilivu wangu umekupa funzo," Kobe alimwambia Sungura kwa upole kisha akaondoka.

**Maswali**:

1. Ukiwa na mwenzako, tambueni nomino zilizo na vinyume vyake katika kifungu ulichosoma.
2. Andika kila nomino na kinyume chake kutoka kwenye kifungu kuhusu sungura.

**Shughuli ya 3:** Vinyume vya nomino katika fungu la maneno

1. Jaza nafasi zilizoachwa kwa kinyume cha neno lililokolezwa rangi.
   (a) Baada ya **dhiki** ________________.
   (b) Umoja ni **nguvu**, utengano ni ________________.
   (c) _________ na **mhiniwa** njia yao ni moja.
   (d) Lililo na **mwanzo** halikosi ________________.
   (e) Mwenda__________na **omo** marejeo ngamani.
2. Tunga sentensi kwa kutumia vinyume vya nomino hizi:
   (a) baraka (c) raha (e) baridi.
   (b) utamu (d) wema

## II. Vinyume vya vivumishi

**Shughuli ya 1:** Vinyume vya vivumishi katika fungu la maneno

1. Ukiwa na mwenzako:
   (a) Chagua neno na kinyume chake kwenye orodha ya maneno yafuatayo:
   jasiri, tamu, haramu, mwoga, mwema, chungu, polepole, halali, haraka na mui.
   (b) Nakili maneno uliyochagua kwenye daftari lako.
2. (a) Nakili mafungu ya maneno yafuatayo katika daftari lako.
   (i) nyumba ndogo imejengwa kando ya nyumba kubwa
   (ii) nguo yangu ina madoa meupe na meusi
   (iii) mshipi mrefu umekatika lakini ule mfupi uko sawa
   (iv) viti vichache vimepangwa, vingi bado viko mbele ya lango.
   (b) Pigia msitari kivumishi na kinyume chake katika kila fungu la maneno katika swali la 2 (a).
3. (a) Soma fungu hili la maneno:

**Tito**

Tito ni mwanafunzi wa Gredi ya Saba. Yeye ni mrefu bali si mfupi. Anapenda kuvaa sare yake ya shati jeupe bali si jeusi. Mfuko wake mara nyingi huwa mzito bali si mwepesi. Tito hapendi kazi chafu. Anapenda kazi safi. Yeye huwasilisha kazi inayoonyesha kumakinika. Yeye ni mpole, huwaepuka watu wakali. Hapendi tabia ya zogo anapenda matukio yenye amani.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

Woga humfanya mtu kukosa nguvu ya kutekeleza na kukamilisha jambo. Tito hupenda kusema, "Ujasiri utakupa nguvu za bidii. Ukiwa mwoga utakuwa na uvivu kwa maana utapata vijisababu vya kutokamilisha lile umetenga kukamilisha."

**Maswali**:

(b) Ukiwa na mwenzako, tambueni kila kivumishi na kinyume chake katika fungu la maneno ulilosoma kuhusu Tito.

(c) Andika daftarini kila kivumishi na kinyume chake kutoka kwenye kifungu.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya vinyume vya vivumishi katika fungu la maneno

1. Andika vivumishi kumi na vinyume vyake daftarini.
2. Tunga kifungu cha maneno kwa kutumia vinyume vya vivumishi hivi:
   (a) zito
   (b) rahisi
   (c) -embamba
   (d) zuri
   (e) -ingi.

**Changamkia**

Tunga kisa kifupi cha kusisimua. Tumia nomino, vivumishi na vinyume vyake katika sentensi.

### Tembea na majira

1. Ukitumia njia za kidijitali, mtumie mwenzako kisa ulichotunga ili akutolee maoni.
2. Iwapo huna kifaa cha kidijitali, andika daftarini. Mpe mwenzako kisa ulichotunga naye akupe chake. Someni kisha mtoleane maoni.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi wako kisa ulichokitunga akupe maoni yake.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

# 11 MAJUKUMU YA WATOTO

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara

#### Kichocheo

Kwa nini watu hutumia vitendo au ishara wanapozungumza?

**Shughuli ya 1:** Maana ya kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara

1. Tazama picha ifuatayo:



2. Mweleze mwenzako unaona nini kwenye picha.
3. Ni ishara gani ambazo watu katika picha ya swali 1 wanatumia ili kuwasiliana?
4. Jadili na mwenzako maana ya kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa mtu anapowasiliana kwa kutumia maneno na vitendo huwa tunasema anazungumza kwa kuambatanisha vitendo au ishara.

**Shughuli ya 2:** Umuhimu wa kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara

1. Ukiwa na mwenzako, zungumzeni kwa kuambatanisha na vitendo jinsi ya kutayarisha chai.
2. Vitendo mlivyotumia katika mazungumzo yenu vilichangia vipi kupitisha ujumbe? Mweleze mwenzako.

**Shughuli ya 3:** Vitendo au ishara za kuambatanisha na mazungumzo

1. (a) Mtajie mwenzako vitendo mlivyotumia katika mazungumzo yenu ya shughuli ya 2.
   (b) Mweleze mwenzako maana ya vitendo mlivyovitumia katika mazungumzo yenu ya shughuli ya 2.
2. Mkiwa katika kikundi, tajeni vitendo au ishara zaidi zinazoweza kutumika katika mazungumzo yenu ya kila siku.

**Shughuli ya 4:** Mazungumzo kwa kuyaambatanisha na vitendo au ishara zifaazo

1. Ukiwa na wenzako katika kikundi, igizeni mazungumzo kuhusu wajibu wa watoto kama vile kwenda shuleni au kudumisha usafi.
2. Tumieni vitendo na ishara mwafaka katika mazungumzo yenu.

**Changamkia**

Jitazame kwenye kioo ukiigiza mazungumzo na mtu fulani. Ambatanisha vitendo na ishara mwafaka kwenye mazungumzo hayo.

### Tembea na majira

1. Tazama na kusikiliza mazungumzo katika televisheni au kifaa cha kidijitali na utambue vitendo na ishara katika mazungumzo hayo.
2. Mwombe rafiki yako akurekodi katika kifaa cha kidijitali ukiyaigiza mazungumzo hayo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mfungulie mzazi au mlezi kifaa cha kidijitali ili atazame na kusikiliza mazungumzo uliyojirekodi.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu mazungumzo yako.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa mapana

#### Kichocheo

Wewe hufurahia kusoma matini kuhusu nini?

**Shughuli ya 1:** Ujumbe wa matini ya kujichagulia

1. Chagua matini uipendayo ili uisome. Inaweza kuwa ni matini kuhusu fasihi, michezo, siasa, teknolojia au historia.
2. Jadili na mwenzako kichwa cha matini uliyosoma.
3. Mweleze mwenzako ujumbe uliopata kutokana na matini uliyosoma.

**Shughuli ya 2:** Msamiati uliotumiwa katika matini

Soma tena matini uliyojichagulia katika shughuli ya 1 kisha:

1. Uandike daftarini maneno yoyote mapya unayopata.
2. Kadiria na kufafanua maana ya neno kulingana na muktadha katika habari uliyosoma.
3. Andika daftarini maana ya maneno hayo kimuktadha.
4. Tumia kamusi kutafuta maana ya maneno mapya ili uelewe vizuri habari unayosoma.

**Shughuli ya 3:** Matumizi ya msamiati katika matini ya kujichagulia

1. Kwa kurejelea matini uliyosoma, tunga sentensi daftarini ukitumia msamiati uliojifunza.
2. Wape wenzako sentensi zako wazisome nawe usome zao.
3. Mkielekezwa na mwalimu, toeni maoni yenu kuhusu sentensi mlizotunga.

**Shughuli ya 4:** Muhtasari wa matini ya kujichagulia

1. Andika muhtasari wa matini uliyosoma.
2. Wasomee wenzako muhtasari wa matini uliouandika.
3. Waombe wenzako wakupe maoni yao kuhusu muhtasari uliowasomea.
4. Wasilisha muhtasari uliouandaa kwa mwalimu ili ausahihishe.

**Shughuli ya 5:** Mazoea ya kusoma matini

1. Jizoeshe kuchagua na kusoma matini mbalimbali mara kwa mara ili kujenga mazoea ya usomaji bora.

   Jaza jarida lifuatalo ili kuweka rekodi ya uliyosoma:


KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Jarida langu**

| | |
|---|---|
| Shule | |
| Jina | |
| Gredi | |
| Tarehe | |
| Anwani ya matini niliyosoma | |
| Muhtasari wa ujumbe niliopata na kuwasilisha kwa wenzangu | |
| Maoni ya wanafunzi wenzangu | |
| Maoni yangu | |
| Maoni ya mwalimu | |

2. Mpe mwalimu jarida lako ili atoe maoni yake.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika anwani na muhtasari wa matini hiyo uliyoisoma.
2. Hifadhi kazi hiyo ili uirejelee baadaye inapohitajika.
3. Iwapo huna kifaa cha kidijitali, fanya kazi hii kwenye daftari lako. Irejelee unapodurusu.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mwasilishie mzazi au mlezi wako muhtasari wa matini ambazo ulisoma. Mwombe akupe maoni yake.

## C. KUANDIKA

### Insha za kubuni — Maelezo

### Kichocheo

1. Insha ya maelezo uliyowahi kuandika ilihusu nini?
2. Ni mambo gani huzingatiwa ili kuandika insha nzuri ya maelezo?

**Shughuli ya 1:** Vipengele vya mpangilio wa insha ya maelezo

1. Soma kielelezo cha insha ya maelezo kifuatacho:

## MAJUKUMU YA WATOTO

Watoto wana majukumu mengi muhimu. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya, mtoto ni mtu aliye na miaka chini ya kumi na minane.

Jukumu kubwa na muhimu kwa kila mtoto ni kusoma ili kujipatia elimu. Elimu itamwezesha kupata maarifa, stadi na mitazamo ifaayo maishani. Kwa hivyo, mtoto hana budi kuwajibika shuleni huku akikumbuka kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame. Anahitajika kusoma kwa makini ili kupata umilisi unaotarajiwa. Aidha, pale anapopata changamoto, anaweza kuelekezwa na mwalimu. Wakati wote, mtoto anashauriwa kudumisha nidhamu.

Vilevile, ni jukumu la watoto kujitunza. Jukumu la kujitunza hujumuisha kunawa, kuoga, kufua na kuvaa nguo safi. Mtoto anayewajibika pia, hutunza mazingira yake shuleni na nyumbani.

Isitoshe, watoto wana jukumu la kuwatii na kuwasaidia wazazi na walezi wao nyumbani. Hii huwa pia ni fursa nzuri kwa mtoto kujifunza kazi za nyumbani, shambani na nyinginezo katika mazingira anamoishi.

Kila mtoto anafaa kutimiza majukumu yake kwa bidii. Mtoto ana wajibu wa kuchagua marafiki waadilifu. Sharti aepuke hali na mazingira ambayo yanaweza kuvuruga na kudhuru akili yake. Haya yote yatamsaidia kukua akiwa mtu muungwana.

2. Jadili na mwenzako sehemu zifuatazo za insha uliyosoma:
   (a) kichwa (b) utangulizi (c) mwili (d) hitimisho.

**Shughuli ya 2:** Mpangilio wa insha ya maelezo

1. Mkiwa wawiliwawili, orodhesheni mfuatano wa matukio kwenye kielelezo cha insha ya maelezo uliyosoma.
2. Jadilini mfuatano wa matukio kuanzia sehemu ya utangulizi hadi hitimisho.
3. Andikeni maneno matatu yaliyotumiwa katika insha kama viunganishi vya kuendeleza mawazo.

**Shughuli ya 3:** Kuandika insha ya maelezo inayozingatia mpangilio ufaao wa maelezo

1. (a) Chagua kichwa utakachoandikia insha ya maelezo.
   (b) Andika vidokezo kuhusu:
      (i) utangulizi
      (ii) mwili wa insha
      (iii) hitimisho.
   (c) Panga vidokezo hivyo jinsi vitakavyofuatana katika insha.
   (d) Tumia vidokezo hivyo kuandika insha ya maelezo. Hakikisha umezingatia mambo yafuatayo:


KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | Mambo ya kuzingatia | Weka alama ya √ ikiwa umezingatia |
|---|---|---|
| i | Kichwa | |
| ii | Utangulizi | |
| iii | Ujumbe | |
| iv | Hati nadhifu | |
| v | Sarufi sahihi | |
| vi | Mtiririko ufaao wa maelezo | |
| vii | Muundo na mtindo ufaao | |
| viii | Msamiati na tahajia sahihi | |

2. Weka insha uliyoandika katika potifolio na kumpa mwalimu ili aisahihishe na kukupa maoni yake.

**Changamkia**

Andika upya insha ya maelezo ukitilia maanani maoni ya mwalimu wako. Msomee mwenzako insha hiyo naye akupe maoni yake. Hifadhi insha safi kwenye potifolio ili kumwonyesha mzazi au mlezi.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika nakala safi ya insha ya maelezo uliyomsomea mwenzako.
2. Hifadhi nakala hiyo kwenye faili ya kidijitali ili kuirejelea utakapohitaji kufanya hivyo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi insha ya maelezo uliyoandika. Mwombe akupe maoni yake kuhusu insha yako.

## D. SARUFI

### Mnyambuliko wa vitenzi

### I. Kauli ya kutenda

**Shughuli ya 1:** Kauli ya kutenda

### Kichocheo

1. (a) Tazama picha.



(b) Ukiwa na mwenzako, jibu maswali yafuatayo ukitumia maneno yaliyokolezwa rangi.

(i) Ni nani **anayemwoshea** vyombo?

(ii) Unafikiri ni nani **anayemwoshea** mwingine vyombo?

(iii) Je, vyombo **vilivyooshwa** vimewekwa wapi?

2. Umegundua nini kuhusu maneno yaliyokolezwa rangi?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa mnyambuliko wa vitenzi ni jinsi vitendo vinavyobadilika kutegemea kauli mbalimbali. Mfano ni kitenzi **osha** kimebadilika na kuwa **oshea** na **oshwa**.

3. (a) Soma maneno yafuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **rukia** | **pikika** | **lisha** | **kimbizwa.** |
| **andika** | **omba** | **beba** | |
| **soma** | **chora** | **tafuta** | |

(b) Chagua vitenzi vilivyo katika kauli ya kutenda kutoka kwa orodha uliyoisoma.

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa vitenzi katika kauli ya kutenda huonyesha kitendo katika hali yake ya kawaida. Mifano ni; osha, soma na lima.

**Shughuli ya 2:** Matumizi ya vitenzi katika kauli ya kutenda

Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo:

(a) futa (b) osha (c) vua

(d) fua (e) tembea (f) choma.

## II. Kauli ya kutendea

**Shughuli ya 1:** Kauli ya kutendea

1. (a) Soma maneno yafuatayo:

   samehe, safishia, chorea, shikwa, oshea, furahia, fungulia, rushiana, fikiria, chekesha, washia, tembelea, safishia, zibia

   (b) Chagua vitenzi vilivyo katika kauli ya kutendea kutoka kwa orodha uliyoisoma.

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa:

(a) Vitenzi katika kauli ya kutendea huishia kwa -ia, -ea na wakati mwingine -lia na -lea. Kwa mfano safishia, oshea, fungulia na tembelea.

(b) Kauli ya kutendea huonyesha hali ya kufanya kitendo:

(i) kwa niaba ya mwingine k.m. Nilimwoshea mama vyombo

(ii) kwa kutumia kifaa fulani k. m. Nilitumia sabuni kuoshea vyombo

(iii) kwa ajili ya mwingine k.m. Nilimfungulia mgeni mlango aingie.

**Shughuli ya 2:** Kutumia vitenzi katika kauli ya kutendea

Panga maneno ili kutunga sentensi sahihi.

(a) mkeka aliwatandikia wageni yangu dada juzi

(b) mbuga tulitembelea uliopita muhula za wanyama pori

(c) aliwapikia mpishi kitamu wageni chakula

(d) nitamwandikia kwa simu ujumbe mfupi baba

(e) kiti ili abiria waketi alimsongea pamoja

(f) mgonjwa alimlipia dawa yangu kaka.

### III. Kauli ya kutendwa

**Shughuli ya 1:** Kutambua kauli ya kutendwa

1. (a) Soma maneno yafuatayo:

   fungwa, gawa, imbwa, fikiwa, jazwa, vutia, pakwa, pendwa, ponywa, ongea, takaswa

   (b) Chagua vitenzi vilivyo katika kauli ya kutendea kutoka kwenye orodha uliyoisoma.

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa vitenzi katika kauli ya kutendwa huonyesha hali ya kuathirika kutokana na kitendo au kufanywa kwa kitendo k.m. mlango umefungwa.

**Shughuli ya 2:** Kutumia vitenzi katika kauli ya kutendwa

1. Geuza sentensi hizi ziwe katika hali ya kutendwa:
   (a) Mama amepika chakula.
   (b) Mwalimu amefunga mlango.
   (c) Akinyi ameandika ujumbe.
   (d) Mogambi alitandika kitanda.
   (e) Dereva aliendesha gari.
2. Kamilisha sentensi kwa kugeuza kitenzi kilicho kwenye mabano kiwe katika kauli ya kutendwa:
   (a) Majukumu yote yali_______________ ifaavyo.(tekeleza)
   (b) Keki ili__________ vizuri sana.(oka)
   (c) Mwizi aliye____________ amepelekwa mahakamani.(shika)
   (d) Makosa yaliyo_______________ yamerekebishwa.(fanya)
   (e) Wimbo wa Jumuiya Ya Afrika Mashariki uli_________katika sherehe. (imba)

### Changamkia

Shirikiana na mwenzako kukamilisha jedwali lifuatalo:

| | Kauli ya kutenda | Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendwa |
|---|---|---|---|
| (a) | Cheza | | |
| (b) | | bebea | |
| (c) | | | igwa |
| (d) | Tega | | |
| (e) | | hamia | |

### Tembea na majira

Nakili kifungu kifuatacho katika kifaa cha kidijitali na **kukoleza rangi** vitenzi vya kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa. Waonyeshe wenzako shuleni ili wakupe maoni yao.

Watu wengi walifurahia siku ya michezo shuleni. Wanafunzi walijiandaa kwa kufanya mazoezi ya kutosha. Mwanamuziki mashuhuri alialikwa. Aliwaimbia na kuwachezea waliofika nyimbo mbalimbali. Wimbo wa Taifa uliimbwa kisha kengele ikagongwa kuanzisha michezo rasmi.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi kifungu ulichoandika katika kifaa cha kidijitali. Mwombe akupe maoni yake.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada ndogo.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Tatua

Umegundua kuwa kuna mwanafunzi ambaye hapendi kuchukua majukumu yoyote katika shughuli za kikundi. Utatumia mbinu gani ili apende kushirikiana na wengine?


KICD Kimeidhinishwa na KICD

# 12 MAGONJWA AMBUKIZI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza kwa makini

#### Kichocheo

Kwa nini unafaa kutambua hoja muhimu katika habari uliyosikiliza?

**Shughuli ya 1:** Hoja muhimu katika habari uliyosikiliza

1. Sikiliza pamoja na wenzako, habari utakayosomewa na mwalimu.
2. Taja mambo muhimu kutokana na habari hiyo.
3. Habari uliyosikiliza ikisomwa na mwalimu ilihusu nini?

**Shughuli ya 2:** Uwasilishaji wa hoja muhimu katika habari

1. (a) Andika orodha ya mambo muhimu uliyoyatambua katika habari uliyosomewa na mwalimu.
   (b) Wasilisha mambo hayo kwa wenzako darasani.
   (c) Mkielekezwa na mwalimu, jadilini kuhusu hoja muhimu katika habari mliyosomewa.

**Changamkia**

1. (a) Msikilize kwa makini mwanafunzi akiwahutubia katika gwaride.
   (b) Waeleze wenzako hoja muhimu ulizosikia katika hotuba ya mwanafunzi mwenzako.
   (c) Shirikiana na wenzako kujadili hoja muhimu katika hotuba ya mwanafunzi mwenzako.

#### Tembea na majira

Kwa kuelekezwa na mwalimu:

1. Tafuta mtandaoni video kuhusu magonjwa ambukizi.
2. Chagua video mojawapo na uisikilize kwa makini.
3. Waeleze wenzako video ilizungumzia ugonjwa gani.
4. Waombe wenzako watoe maoni kuhusu ugonjwa uliozungumziwa katika video.
5. Ikiwa hutaweza kupata video, tafuta magazeti au vitabu maktabani vyenye makala kuhusu magonjwa ambukizi. Soma kisha uandike kwa ufupi ujumbe kwenye makala uliyosoma.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mweleze mzazi au mlezi hoja muhimu katika habari ulizozisikiliza kwenye video kuhusu ugonjwa ambukizi.
2. Mwombe akupe maoni yake.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa ufasaha

#### Kichocheo

Unazingatia nini ili kusoma makala kwa ufasaha?

**Shughuli ya 1:** Kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora

1. (a) Mweleze mwenzako mambo yaliyokuvutia uliposikiliza habari uliyosomewa katika somo la kusikiliza kwa makini.
   (b) Msomee mwenzako kifungu kifuatacho kwa kuzingatia matamshi bora:

**Kifuakikuu**

Kifuakikuu ni ugonjwa ambukizi. Ugonjwa wa kifuakikuu husababishwa na aina mbalimbali za bakteria. Kwa kawaida huathiri mapafu, vilevile huweza kuathiri sehemu nyingine za mwili. Kifuakikuu huambukizwa kutoka kwa mgonjwa hadi mtu mwingine. Njia kuu ya maambukizi ni kupitia hewa hasa wakati mgonjwa anapokohoa, kupiga chafya au kutema mate.

Dalili za kawaida za maambukizi ya kifuakikuu ni kikohozi sugu, kukohoa damu, homa, kutokwa na jasho usiku na kukonda. Tiba ya ugonjwa wa kifuakikuu ni pamoja na kupewa tembe za kumeza na kudungwa sindano. Uhamasishaji wa kijamii pia ni muhimu katika kuzuia maambukizi ya ugonjwa huu. Watu hushauriwa wakubali kupimwa hali zao za afya kila mara na kupewa chanjo kuzuia kupata kifuakikuu.

   (c) Jadilini kuhusu usomaji wenu wa kifungu kuhusu kuhusu **Kifuakikuu** mkizingatia matamshi bora.

**Shughuli ya 2:** Kusoma kifungu kwa kasi ifaayo

1. Ukiwa na mwenzako, someni tena kwa zamu kifungu kuhusu **Kifuakikuu**, kilicho katika shughuli ya 1 huku mmoja akimpimia mwenzake muda na idadi ya maneno aliyosoma kwa dakika moja.
2. Hesabuni idadi ya maneno yaliyosomwa kwa dakika moja.
3. Kadirieni kasi ya usomaji wa kila mmoja wenu.

**Shughuli ya 3:** Kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo

1. Ukiwa na mwenzako, someni kwa zamu aya moja ya kifungu kuhusu **Kifuakikuu** kwa sauti inayosikika ipasavyo.

2. Muombe mwenzako akueleze kuhusu kiwango cha sauti ulichokitumia wakati ulipokuwa ukisoma.

**Shughuli ya 4:** Kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo

1. Someni tena kwa zamu aya moja moja ya kifungu cha **Kifuakikuu** kwa sauti huku kila mmoja akitumia ishara pale inapofaa.
2. Muombe mwenzako akupe maoni yake kuhusu ulivyotumia ishara wakati wa kusoma.

**Changamkia**

Sikiliza au tazama habari za redio au televisheni na kuwaiga wasomaji wa habari ukizingatia matamshi bora, kasi na sauti ifaayo.

### Tembea na majira

1. Jirekodi kwenye video ukisoma matini uliyochagua. Zingatia matamshi bora, sauti inayosikika vizuri, kasi na ishara zifaazo.
2. Sikilizeni pamoja na wenzako video uliyorekodi. Waulize wenzako wakupe maoni yao kuhusu usomaji wako.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwombe mzazi au mlezi kutazama video uliyojirekodi ukisoma matini uliyochagua.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu usomaji wako.

## C. KUANDIKA

### Hotuba ya kupasha habari

#### Kichocheo

Ni habari gani ambayo watu wanaweza kupashwa kupitia kwa hotuba?

**Shughuli ya 1:** Kueleza maana ya hotuba ya kupasha habari

1. Ukiwa na wenzako, tajeni watu ambao mmewahi kusikia au kuona wakizungumzia watu katika mikutano.
2. Mweleze mwenzako habari ambazo watu uliowataja katika shughuli ya 1 walikuwa wakiwasilisha kwa wasikilizaji wao.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa hotuba ya kupasha habari ni maelezo ya kina na ya hakika kuhusu mada mahususi yanayotolewa kwa hadhira.

**Shughuli ya 2:** Kutambua hotuba ya kupasha habari katika matini

1. Mweleze mwenzako unafikiri picha ifuatayo inahusu nini.



2. (a) Ukiwa na mwenzako, someni kifungu kifuatacho:

**AFYA YETU**

Mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, walimu na wanafunzi wote hamjambo? Nina furaha tele kujiunga nanyi humu shuleni mwenu leo. Tutakuwa na fursa ya kusema mengi yanayohusu afya yetu. Kwa hakika, hatutakosea tukisema kuwa afya ni muhimu katika maisha ya binadamu.

Kuna magonjwa mengi yanayoathiri afya za waja. Leo ningependa tuzungumze kuhusu magonjwa ambukizi. Mifano ya magonjwa hayo ni kipindupindu, ukimwi, magonjwa ya zinaa, kifua kikuu, na ugonjwa wa korona.

Magonjwa haya huleta hasara kwa mtu binafsi na nchi kwa jumla. Pesa na muda mwingi hutumika katika shughuli za matibabu. Jambo hili huzorotesha uchumi wa mtu binafsi na ule wa nchi.

Isitoshe, magonjwa haya yasiposhughulikiwa kwa haraka husababish mauti kwa watu wengi. Unapopata dalili za ugonjwa wowote au unapohisi kuwa afya yako si njema, muone daktari mara moja. Si vizuri kujinunulia dawa bila ushauri wa tabibu.

Ikiwa kwa bahati mbaya kumetokea mkurupuko wa maradhi yoyote, zingatia mashauri ya wizara ya afya. Serikali huwashauri wananchi jinsi ya kujikinga na majanga ya magonjwa mara kwa mara na hasa wakati kama huo. Hutoa ushauri huo kupitia vyombo vya habari na maafisa wa serikali nyanjani.

Ni matumaini yangu kuwa sote tutazingatia hatua zifaazo kujikinga na kungamiza magonjwa ambukizi. Asanteni kwa kunisikiliza.

(b) Jadili na mwenzako aina ya kifungu mlichosoma.

**Shughuli ya 3:** Ujumbe, lugha na muundo wa hotuba

1. Elezeni ujumbe unaowasilishwa katika kila aya kwenye hotuba mliyosoma.
2. Jadilini na mwenzako kuhusu lugha ilivyotumika katika kifungu mlichosoma katika shughuli ya 2(a).
3. Jadilini na mwenzako muundo wa hotuba mliyosoma katika shughuli ya 2(a) mkizingatia:
   (a) utangulizi (b) mwili (c) hitimisho.

**Shughuli ya 4:** Kuandika hotuba ya kupasha habari

1. (a) Kumezuka homa ya kuambukizana katika eneo lako. Andika hotuba utayotoa kuhusu namna ya kuzuia maenezi ya homa hiyo.
   (b) Iweke kwenye potifolio na kuiwasilisha kwa mwalimu ili aisahihishe.
   (c) Andika nakala safi ya hotuba baada ya mwalimu kuisahihisha.
   (d) Wasomee wenzako katika darasa hotuba uliyoiandika.

**Changamkia**

Igiza hotuba ambayo umewahi kusikiliza.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kuandika tena nakala safi ya hotuba yako.
2. Ihifadhi kidijitali ili kuirejelea baadaye itakapohitajika.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi hotuba uliyoandika.
2. Muombe akupe maoni yake kuhusu ujumbe wa hotuba yako.

## D. SARUFI

### Aina za sentensi

### I. Sentensi sahili

### Kichocheo

Ni aina gani za sentensi unazozijua?

**Shughuli ya 1:** Maana ya sentensi sahili

1. (a) Soma sentensi zifuatazo:
   (i) Tumekula matunda.
   (ii) Mwanafunzi anaandika.

(iii) Gari limepata ajali.
(iv) Wanafunzi walionyesha upendo.
(v) Ng'ombe alipewa maji.

(b) Je, umegundua nini kuhusu sifa za sentensi sahili ulizozisoma?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa sentensi sahili huwa na wazo moja kwa kuwa na kitenzi kimoja. Mfano ni; Daktari amemtibu mgonjwa.

**Shughuli ya 2:** Je, utatambua vipi sentensi sahili?

Mkiwa wawiliwawili:

1. (a) Tambueni sentensi sahili kutoka kwenye orodha ifuatayo:
   (i) Watoto wote hulindwa.
   (ii) Alipendwa na watu kwa kuwa aliwaheshimu.
   (iii) Wafanyakazi walionywa dhidi ya ulevi.
   (iv) Bawabu alifungua lango.
   (v) Wanacheza uwanjani.
   (vi) Nitaoga kisha nitavaa nguo safi.
   (vii) Nyumbani kwao ni safi.
   (viii) Tudumishe amani nchini kote.
   (ix) Madaktari wamegundua tiba ya ukambi.
   (x) Walifika kwetu jana jioni.
2. Umegundua nini kuhusu sentensi ulizotambua?

**Shughuli ya 3:** Kutunga sentensi sahili

Tunga sentensi sahili tano kuhusu magonjwa ambukizi.

## II. Sentensi ambatano

### Kichocheo

1. Ni aina gani za sentensi unazozijua?
2. Aina za sentensi ulizozitaja zinatofautiana vipi?

**Shughuli ya 1:** Maana ya sentensi ambatano

1. (a) Soma sentensi zifuatazo:
   (i) Tumekula matunda kisha tukala chakula.
   (ii) Mwalimu anatoa maagizo na mwanafunzi anaandika.
   (iii) Gari limepata ajali lakini abiria hawakuumia.
   (iv) Wanafunzi hawakumcheka wala kumsuta.

(v) Ng' ombe alikula nyasi, akashiba ila hakunywa maji.

(b) Je, umegundua nini kuhusu sifa za sentensi ambatano ulizozisoma?

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa sentensi ambatano huwa na wazo zaidi ya moja kwa kuwa na vitenzi zaidi ya kimoja. Kiunganishi hutumiwa kubainisha mawazo hayo. Mfano ni Daktari amemtibu mgonjwa kisha akampa ushauri nasaha.

**Shughuli ya 2:** Kutambua sentensi ambatano

Mkiwa wawiliwawili:

1. (a) Tambueni sentensi ambatano kutoka kwenye orodha ifuatayo:
   - (i) Walisikiliza ushauri wa mwalimu kisha wakaenda hospitali kupokea chanjo.
   - (ii) Watasafiri kwa ndege.
   - (iii) Mawingu ya mvua yalitanda ingawa mvua haikunyesha.
   - (iv) Alitamani kunywa maji.
   - (v) Nilimsamehe ijapokuwa alinikosea.

**Shughuli ya 3:** Kutunga sentensi ambatano

1. Tunga sentensi ambatano nne sahihi kutokana na jedwali lifuatalo.

| | | |
|---|---|---|
| Nilikula chakula | kwa kuwa | nilichelewa kufika. |
| Nilisema naye | ingawa | sikuwa na njaa. |

**Changamkia**

1. Soma kifungu kifuatacho:

   Bosibosi alifurahi. Hakujua vizuri amefurahishwa na nini. Mambo mengi mazuri yalikuwa yametendeka. Alikuwa amechaguliwa kiranja ingawa alikuwa mgeni katika shule ile. Kuwania uongozi kisha kuchaguliwa kulimpa furaha. Alipenda kuihudumia jamii na wadhifa aliopewa ulimpa nafasi hiyo. Bosibosi pia alikuwa amepewa tabuleti mpya. Tabuleti ilikuwa ya matumizi ya majukumu aliyopewa.

2. Kutokana na kifungu ulichosoma, nakili daftarini:
   - (a) Sentensi sahili
   - (b) Sentensi ambatano



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Tembea na majira

1. Tafuta mtandaoni maelezo zaidi kuhusu sentensi sahili na ambatano.
2. Soma maelezo na mifano ya sentensi utakazopata ili ujifunze zaidi.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mweleze mzazi au mlezi kuhusu aina za sentensi ulizojifunza.
2. Jadiliana naye mifano ya sentensi sahili na ambatano katika lugha nyingine mnayotumia nyumbani.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada ndogo.

| Mada ndogo | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
| --- | --- |
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Tatua

1. Umegundua kuwa mwenzako hazingatii kanuni za kiafya anapokwenda chafya. Ni hatua gani unazofaa kuchukua ili kumrekebisha?
2. (a) Tazama picha hii:



   (b) Picha hii inakukumbusha nini? Eleza.
   (c) Eleza jinsi ambavyo mtu aliye kwenye picha anazuia kuambukizwa maradhi.
   (d) Tafiti na uandike magonjwa ambukizi mengine matano yanayoweza kumshika mtu asipovalia jinsi alivyo mtu kwenye picha ya 2(a).



KICD Kimeidhinishwa na KICD

# 13 UTATUZI WA MIZOZO

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Wahusika katika nyimbo

**Kichocheo**

1. Je, ni wahusika gani katika wimbo unaowajua?
2. Wahusika hao wana umuhimu gani katika wimbo?

**Shughuli ya 1:** Wahusika katika wimbo

1. Mkiwa katika vikundi viwili, imbeni wimbo huu kwa zamu. Kundi moja likiimba lingine litasikiliza. Mwalimu atawaelekeza.

**Kisima cha wanyama**

1. Hapo zamani za kale
   Paliishi wanyama x2
   Na kiongozi wao alikuwa Simba.
   Simba,
   Alinguruma x2
   Na wanyama wote walikwenda mbio.
2. Simba alisema,
   Tuchimbeni kisima x2
   Na tukipata maji tutakunywa sote.
   Njooni,
   Tuchimbeni kisima x2
   Na wanyama wote walikwenda mbio.
3. Sungura mjanja,
   Alijificha x2
   Asifanye kazi ya kuchimba kisima.
   Maji,
   Yakawa tayari x2
   Simba akasema Sungura asiyachote.
4. Ndovu aliambiwa,
   Ashike doria x2
   Amnase Sungura akichota maji.
   Sungura,
   Alivyo mjanja x2
   Alimfunga Ndovu akachota maji.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

5. Simba alichagua,
   Chui mkali x2
   Ashike doria amtishe Sungura.
   Sungura,
   Aliingia x2
   Ndani ya kibuyu akaenda mtoni.

6. Simba aliamua,
   Kumleta Kobe x2
   Alivyo na hekima alimshika Sungura.
   Kobe,
   Aliweka mtego x2
   Wa kipusa wa gundi akamnasa Sungura.

7. Sungura alilia,
   Oi nisamehe x2
   Sitarudia tena nimekoma utundu.
   Wanyama,
   Walimwonya Sungura x2
   Sungura alitubu na kusafisha kisima.

2. Wimbo huu unahusu nini? Waeleze wenzako.
3. Katika wimbo mlioimba na kusikiliza, jadilianeni kuhusu aina za wahusika kwa kurejelea:
   (a) mwimbaji au waimbaji
   (b) wahusika waliotajwa katika wimbo
   (c) wasikilizaji wa wimbo.

**Shabashi!**

Nimejua kuwa kuna aina mbalimbali za wahusika katika wimbo. Kuna mwimbaji au waimbaji, wahusika wanaotajwa na wasikilizaji.

**Shughuli ya 2:** Wahusika katika wimbo

1. Jadili na wenzako katika kikundi sifa za kila mhusika aliyetajwa katika wimbo wa **Kisima cha wanyama**.
2. Mweleze mwenzako jinsi kila mhusika alivyochangia kuendeleza maudhui ya wimbo.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 3:** Mafunzo kutokana na wahusika katika wimbo

Mweleze mwenzako mafunzo ambayo umepata kutokana na wahusika katika wimbo **Kisima cha wanyama** kwa kurejelea:

1. vitendo vya wahusika
2. maneno ya wahusika
3. sifa za wahusika.

**Changamkia**

Katika kikundi, imbeni wimbo Kisima cha wanyama huku mkiigiza matendo ya wahusika waliotajwa.

### Tembea na majira

1. Mkielekezwa na mwalimu, tumieni kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo.
2. Tajeni wahusika ambao wanajitokeza katika wimbo huo.
3. Andikeni maelezo kuhusu tabia na sifa za wahusika mliowatambua kutoka kwenye wimbo mliochagua.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwimbie mzazi au mlezi wimbo uliojifunza shuleni.
2. Mweleze kuhusu wahusika wa wimbo huo.

## B. KUSOMA

### Kusoma kwa kina

### Mbinu za lugha

### Kichocheo

Mbinu za lugha zina umuhimu gani zinapotumiwa katika kifungu?

**Shughuli ya 1:** Maana ya mbinu za lugha katika fasihi

1. Mkiwa katika kikundi, someni vifungi hivi.

    (a) Alimwangalia sana. Alimwangalia kwa jicho la hadubini. Alimwangalia kuona kama kweli aliyoyaona yalikuwa ni kweli. Wakati huo wote Kazana alikuwa ametulia kama maji mtungini. Alijinyamazia jii. Kazana alikuwa ametoroka nyumbani miaka mitano iliyopita. Leo amekutana ana kwa ana na babake mjini. Damu ni nzito kuliko maji. Babake alipofahamu kuwa alikuwa akimwangalia Kazana, alibubujikwa na machozi kuona hali ya mwanawe. Kazana alikuwa amedhoofika sana. Walikumbatiana kwa furaha tele. Walielekea nyumbani pamoja.

(b) Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kubebwa kwa treni. Ilikuwa ni siku ya Jumamosi. Treni ilifika saa nne mchana. Hapo kwenye stesheni tulikuwa wengi.Tulikuwa tumeilipia safari kupitia mtandao wa intaneti. Niliingia ndani ya treni. Nilipata nafasi yangu katika kiti mojawapo. Kiti hicho kilikuwa nambari kumi na saba. Nilifurahia kila hatua ya safari hiyo. Niliona watu mashambani wakijishughulisha na kilimo. Treni ilipitia ndani ya misitu yenye miti mikubwa. Kwingineko niliona miamba ya kuajabia. Nilifika salama mwendo wa saa saba.

2. (a) Waeleze wenzako kifungu ambacho kina matumizi ya mbinu za lugha.
   (b) Unafikiri mbinu za lugha ni nini?
   (c) Andika mbinu za lugha kutokana na kifungu ulichochagua.
   (d) Fafanua kila mbinu ya lugha uliyochagua.

**Shabashi!**

Mbinu za lugha ni matumizi ya maneno kwa njia ya usanii. Mifano ya mbinu za lugha ni methali, misemo, tashbihi, sitiari, takriri na majazi. Umuhimu wa mbinu za lugha ni kukuza ladha, mawasiliano, kuburudisha, kupunguza uchungu, kuhimiza na kusisitiza. Mbinu za lugha hutumiwa katika uandishi ili kuongeza ladha katika mawasiliano.

3. Tajeni na kueleza maana ya mbinu nyingine za lugha mnazojua katika fasihi.

### Shughuli ya 2: Mbinu za lugha katika novela

Mkiwa katika kikundi, rejeleeni novela mliyosoma darasani na kufanya yafuatayo:

1. Someni sehemu ya novela hiyo.
2. Tambueni mbinu za lugha zilizotumika katika sehemu mliyosoma ya novela.
3. Ziandikeni mbinu hizo daftarini huku mkitoa mifano mahali zimetumika kutoka kwenye novela mliyosoma.

### Shughuli ya 3: Umuhimu wa mbinu za lugha zilizotumiwa katika novela

1. Kwa kurejelea sehemu mahususi ya novela uliyoisoma, elezeni athari au picha unayopata akilini kutokana na mbinu za lugha zilizotumiwa.
2. Mkiwa wawiliwawili, elezeni umuhimu wa matumizi ya mbinu tofauti za lugha katika uwasilishaji wa ujumbe wa novela.
3. Toeni mifano mwafaka ya mbinu za lugha kutokana na novela mliyosoma darasani.

**Changamkia**

Mkiwa katika vikundi, tafuteni na kueleza mbinu za lugha zilizotumika katika novela nzima kwa kufuata utaratibu huu:

1. Kila kikundi kitafute mbinu za lugha tofauti na kingine.
2. Andikeni kwenye chati mbinu zilizodondolewa na kila kikundi.
3. Kila kikundi kiwasilishe darasani mbinu za lugha walizotambua kwenye novela ili kupata maoni ya vikundi vingine.
4. Bandikeni chati za mbinu za lugha darasani baada ya mawasilisho.
5. Kusanyeni mbinu zilizowasilishwa na vikundi vyote ili kuwa na mkusanyiko kamili wa mbinu za lugha zilizotumika katika novela nzima.

**Tembea na majira**

Mkiwa wawiliwawili, tumieni mtandao kutafuta mbinu nyingine za lugha na maana zake. Wasilisheni matokeo ya utafiti wenu kwa mwalimu ili atoe maoni.

## C. KUANDIKA

### Insha za kubuni — Maelezo

**Kichocheo**

1. Je, insha ya maelezo inahusu nini?
2. Je, ni vigezo vipi vinavyotumika katika kuandika insha ya maelezo?

**Shughuli ya 1:** Mambo ya kimsingi katika uandishi wa insha ya maelezo

Rejelea insha ya maelezo uliyohifadhi kwenye potifolio hapo awali kuhusu mpangilio wa insha ya maelezo. Isome ukiwa na mwenzako ili kutambua mambo yafuatayo:

1. mada ya insha
2. muundo wa insha
3. mpangilio wa aya
4. mtiririko wa hoja
5. mawazo yanayokuzwa katika insha aya baada ya aya
6. uakifishaji
7. maendelezo ya maneno
8. matumizi ya lugha.

**Shughuli ya 2:** Insha ya maelezo inayodhihirisha sifa za mtu

1. Ukiwa na mwenzako, andaeni vidokezo mtakavyotumia kuandika insha kuhusu mtu yeyote aliyesaidia watu waliogombana kuelewana. Elezeni kuhusu sura na matendo yake.
2. Vipangeni vidokezo hivyo ili viwe na mtiririko ufaao.
3. Ukiwa peke yako, tumia vidokezo hivyo kuandika nakala ya kwanza ya insha yako.
4. Ukiwa na wenzako katika kikundi someni insha mlizoandika na kusahihisha makosa mtakayogundua. Angalieni usahihi wa lugha, maendelezo ya maneno, mpangilio wa aya, uakifishaji, ubunifu wa mawazo na muundo ufaao wa insha ya maelezo.
5. Andika nakala safi ya insha yako.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kunasa insha uliyoiandika daftarini. Unaweza kuipiga picha au kuipiga chapa.
2. Wasambazie wenzako darasani waisome na kuitolea maoni.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Msomee mzazi au mlezi insha uliyoandika ili akupe maoni yake.

## D. SARUFI

### Ukanushaji kwa kuzingatia nyakati

#### Kichocheo

1. Kwa nini huwa tunakanusha kauli?
2. Tunakanusha sentensi kwa kuzingatia nyakati gani?

**Shughuli ya 1:** Maana ya ukanushaji

1. Mkiwa wawiliwawili, someni na mwenzako sentensi katika jedwali lifuatalo:

| | A | B |
|---|---|---|
| (a) | Paka alikunywa maziwa. | Paka hakunywa maziwa. |
| (b) | Mwalimu ataenda mjini. | Mwalimu hataenda mjini. |
| (c) | Maji yanachemka. | Maji hayachemki. |
| (d) | Dirisha litapakwa rangi nzuri. | Dirisha halitapakwa rangi nzuri. |
| (e) | Uzi ulikatikia pabaya. | Uzi haukukatikia pabaya. |

2. Mweleze mwenzako umegundua nini kuhusu sentensi za **A** na **B** kwenye jedwali?

**Shabashi!**

Nimetambua kuwa sentensi za **A** zinaonyesha hali ya kukubali ilhali za **B** zinaonyesha hali ya kukataa au kukanusha.

### Shughuli ya 2: Nyakati katika matini

1. Soma kifungu kifuatacho:

"Siti, njoo, ninakukumbusha tu. Wakati wa mvua, usiwe unapenda kusimama palipo na miti. Hili zingatia sana hasa wakati wa mvua na radi." Mwalimu alikamilisha usemi. Niliendelea kufikiri kuhusu maneno hayo ya mwalimu. Nilifululiza safari yangu kutoka shuleni kuelekea nyumbani. Mawingu yalitanda angani. Nilimsikia jirani yangu akinigutua, "Siti, mvua itanyesha muda mfupi kutoka sasa. Njoo ujikinge mwanangu la sivyo utanyeshewa."

2. Orodhesha daftarini maneno ambayo yanaonyesha nyakati tofauti katika kifungu ulichokisoma katika swali la kwanza.
3. Eleza ni wakati upi unaorejelewa katika kila neno uliloandika.

### Shughuli ya 3: Ukanushaji kwa kuzingatia wakati uliopita, uliopo na ujao katika matini

#### I. Hali ya kukanusha wakati uliopita

1. (a) Soma kifungu kifuatacho:

Yeye ndiye aliyeanza ugomvi. Mimi sikuwa nimemkosea kwa njia yoyote ile. Hakuhisi vizuri nilipomkataza rafiki yangu kuzungumza kwa sauti ya juu sana. Sikutaka wale waliokuwa wakimsikiliza wakasirishwe na sauti hiyo. Rafiki hakuchukulia ushauri wangu kwa uzuri.

(b) Nakili vitenzi vyote kutoka kwenye kifungu daftari.
(c) Andika vitenzi vyote vinavyoonyesha hasa kitendo kipi kutendeka.
(d) Nakili daftarini vitenzi vyote vinavyosaidia kitendo kilitendeka.

#### II. Hali ya kukanusha wakati uliopo

Rafiki yangu alikuwa mtu ambaye hakuzoea kushirikiana na watu. Tulizungumza kwa muda mrefu. Nilimshauri kuwa si vizuri kuzungumza kwa sauti ya juu. Rafiki alifanya jambo moja. Alinisikiliza kwa makini. Nilimweleza pia kama haelewani na mtu yeyote, achukue muda kutulia kwanza. Akihisi hana hasira, wanaweza kulizungumzia jambo hilo. Rafiki alifurahi sana kwa ushauri wangu na akaahidi hatazozana na watu tena.

(b) Andika vitenzi vilivyo katika hali ya kukanusha kwenye kifungu ulichosoma.

(c) Eleza vitenzi hivyo viko katika nyakati gani.

2. (a) Andika kifungu kifuatacho daftarini.

Paka wangu hakutembea haraka. Hakupita karibu na dirisha langu. Paka huyu ninampatia maziwa lakini hanywi kwa urahisi. Pia, hataweza kupanda ngazi.

(b) Pigia mstari vitenzi vilivyo katika hali ya kukanusha.

(c) Eleza vitenzi hivyo viko katika wakati gani.

### III. Hali ya kukanusha wakati ujao

3. (a) Soma kifungu hiki.

Floli hatakuwa amechoka nitakapofika kwao. Yeye hatasita kunikaribisha. Hatakosa kuniuliza habari za kwetu nyumbani. Mimi nitamweleza kuhusu maendeleo yangu ya sasa. Sitamkumbusha yaliyopita.

(b) Chorea mviringo vitenzi vilivyo katika hali ya kukanusha kwenye kifungu ulichosoma.

(c) Eleza vitenzi hivyo viko katika wakati gani.

## Shughuli ya 4: Ukanushaji wa wakati uliopita, uliopo na ujao katika sentensi

### I. Hali ya kukanusha wakati uliopita

Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya kukanusha wakati uliopita:

(a) Mama atakuwa akimpa kaka mawaidha.

(b) Daktari huwa anatushauri kuhusu magonjwa ambukizi.

(c) Dawati lake huwa linapakwa rangi.

(d) Taka zote zitakuwa kwenye jaa.

(e) Mimi sitakuwa hapo atakapofika.

### II. Hali ya kukanusha wakati uliopo

Tunga sentensi za hali ya kukanusha wakati uliopo ukitumia maneno yafuatayo:

(a)anaandika

(b)tunatengeneza

(c)wanasameheana

(d)zinapanguswa

(e)wanaelewana.

### III. Hali ya kukanusha wakati ujao

Chagua sehemu za sentensi kutoka A na B ili kutunga sentensi sahihi kuonyesha kukanusha wakati ujao.

| | A | B |
|---|---|---|
| (a) | Vikapu vikubwa vitakuwa | vikiuzwa sokoni Alhamisi iliyopita. |
| (b) | Vikapu vikubwa vilikuwa | vikiuzwa sokoni juma lijalo. |
| (c) | Ngazi zenyewe zitakuwa | sokoni kila siku. |
| (d) | Ngozi za watoto wenye harara | zilitibiwa na daktari zitapona. |
| (e) | Mikeka itakuwa ikiletewa | zikiandaliwa na fundi stadi. |

## Changamkia

Mkiwa katika kikundi, chezeni mchezo wa kutaja vitenzi na kuvitumia katika hali ya kukanusha kwa kuzingatia wakati uliobainika katika kitenzi hicho. Fuateni maagizo yafuatayo:

1. Simameni katika mviringo huku mwanafunzi mmoja akiwa na mpira.
2. Mwanafunzi mwenye mpira atatamka kitenzi na kisha kumrushia mpira mwanafunzi mmoja katika kikundi.
3. Mwanafunzi aliyerushiwa mpira ataushika kisha kukanusha kitenzi hicho.
4. Naye atamrushia mpira mwanafunzi mwingine huku akitaja kitenzi kingine.
5. Mchezo unaendelea hivyo hadi kila mwanafunzi ashiriki.

## Tembea na majira

1. Ukielekezwa na mwalimu, tumia kifaa cha kidijitali:
   (a) Kuandika sentensi mbilimbili katika wakati uliopo, ujao na uliopita.
   (b) Kanusha sentensi zote ulizotunga katika (a).
   (c) **Kolezea wino** maneno yanayoonyesha ukanushaji.
   (d) Wasambazie wenzako kazi hiyo ili watoe maoni yao.

## Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako sentensi ulizotunga na ukanushaji wake.
2. Mwombe akupe maoni yake.

## Tafakuri


KICD Kimeidhinishwa na KICD

Andika maelezo mafupi kuhusu mambo uliyoweza kufanya kwa kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada ndogo hizi |
| --- | --- |
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

**Tatua**

Kumetokea mzozo katika kikundi chenu darasani kuhusu sifa za wahusika katika novela mliyosoma. Eleza utakavyowapatanisha wenzako kwa kutumia maelezo katika novela husika.

# 14 MATUMIZI YA PESA

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Lugha katika nyimbo

### Kichocheo

1. Je, umewahi kusikiliza wimbo gani?
2. Unaweza kutambua matumizi gani ya lugha katika nyimbo?

**Shughuli ya 1:** Vipengele vya lugha vinavyotumika katika nyimbo

1. Jadili mambo mnayoyaona kwenye picha:





KICD Kimeidhinishwa na KICD

2. Sikiliza wimbo ufuatao aliounasa mwalimu kwenye kifaa cha kidijitali.

Unapopata pesa we dada aaa,
Unapopata pesa we kaka aaa,
Ukumbuke kutunza hilo jasho lako,
Utumie mapato kwa busara.x2

Usiwe kama bendera ndugu uuu,
Kupeperuka kwenye upepo ooo,
Vizuri vya dunia haviishi kaka,
Usiharibu pesa kwa anasa.x2

Nakushauri we ndugu yangu uuu,
Ujiwekee akiba yako ooo,
Hata kama kidogo weka kila mara,
Utajaza kibaba siku moja.x2

Ujana moshi utafuka aaa,
Utapofika lala salama aaa,
Utahitaji hela za matunzo dada,
Fanya hima wekeza anza leo.x2

Wasaidie na marafiki iii,
Jamaa zako na ndugu pia aaa,
Ukumbuke na wema usizidi uwezo,
Kutoa iwe moyo si utajiri.x2

3. Ukiwa na wenzako, imbeni wimbo mliousikiliza.
4. Jadili na wenzako vipengele vya lugha vilivyotumika katika wimbo mliousikiliza kwa kujibu maswali yafuatayo:
   (a) Ni maneno gani yaliyorudiwarudiwa?
   (b) Ni methali gani zilizodokezwa katika wimbo?
   (c) Wimbo umetumia ulinganisho gani wa vitu?
   (d) Je, wimbo umetumia maneno gani yasiyokuwa na maana?
   (e) Umetambua nahau gani kwenye wimbo?

**Shughuli ya 2:** Umuhimu wa vipengele vya lugha vinavyotumika katika nyimbo teule

Ukiwa katika kikundi, jadilini umuhimu wa vipengele vya lugha mlivyovitambua katika shughuli ya 1.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa utunzi wa wimbo huwa unazingatia vipengele vya lugha kama vile kurudiarudia maneno, kujumuisha methali na nahau na ulinganisho wa sifa fulani za kutoa mafundisho. Mifano ni katika wimbo wa shughuli ya 1 ujana umefananishwa na moshi kwa maana vijana wanapaswa kutumia muda vyema maana muda hupita haraka kama moshi.

**Changamkia**

Waimbie wenzako wimbo unaoupenda.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kunasa rafiki yako akiimba wimbo anaoupenda.
2. Mtumie mwalimu wako wimbo uliounasa ili awatolee wewe na rafiki yako maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Mwasilishie mzazi au mlezi wako wimbo uliounasa ukiwaimbia wenzako.
2. Mwombe mzazi au mlezi akupe maoni yake kuhusu uwasilishaji wako.

## B. KUSOMA

### Ufahamu

### Kifungu cha mjadala

### Kichocheo

1. Umewahi kusoma kifungu cha mjadala?
2. Je, ni mambo gani hukusaidia kuelewa kifungu cha ufahamu?



KICD Kimeidhinishwa na KICD

## Shughuli ya 1: Habari mahususi katika kifungu cha mjadala

1. Tazama picha hii kwa makini. Je unafikiri:




   (a) Watu katika picha hii wanazungumzia nini?
   (b) Ni ishara gani zinazoonyesha wanazungumza kuhusu suala fulani?
   (c) Toa mifano minne ya mada za mambo ambayo wewe na rafiki yako mnaweza kuzungumzia.

2. Mshirikishe mwenzako kusoma mjadala ufuatao:

Tata alimwamkua rafiki yake Faulu kisha akamshukuru kwa kuitikia mwaliko wake. Faulu naye alimhakikishia rafiki yake Tata kuwa asingekosa kufika kama alivyoalikwa kwa kuwa mtu hakatai wito, hukataa aitiwalo.

Faulu na mwenzake Tata wamefanya biashara kwa mwongo mmoja


KICD Kimeidhinishwa na KICD

sasa. Tata ndiye alianzisha mjadala. Kwanza alitazama angani kama mtu anayesoma jambo muhimu lililoandikwa mawinguni. Baada ya muda mfupi alimfunulia moyo mwenzake Faulu. Alimtaka amshauri kuhusu namna ya kujenga misingi imara katika biashara. Faulu alimwangalia Tata usoni na akaona kweli alisononeka. Aliweka mguu wake wa kushoto juu ya ule wa kulia. Akasema, "Ikiwa ushauri wangu utakufaa kuimarisha biashara yako, nitafanya hivyo bila kusita."

Tata alisema kuwa biashara haigombi. "Naona duka lako lazidi kukua huku langu likiniletea hasara kubwa. Nikiendelea kupata hasara kama hiyo ndani ya miezi miwili ijayo, nitalazimika kuifunga biashara yangu."

Faulu alimpa pole mwenzake na kumhakikishia kwamba hangetaka afunge biashara yake. "Je, wewe huweka rekodi ya biashara yako?"

Tata alishangaa kusikia neno rekodi. Alimuuliza Faulu, "Rekodi gani? Biashara ni yangu, namwekea nani rekodi?"

Faulu alimjibu Tata, "Tatizo moja ndilo hilo. Mali bila daftari hupotea bila habari. Ni vyema kuweka rekodi za biashara kila wakati. Ukifanya hivyo utajua unapopata faida au hasara."

Tata alitaka apewe mikakati zaidi ya kuiendeleza biashara yake.

"Unaweza kwenda benki ukachukua mkopo."Faulu alimshauri zaidi.

"Benki kuchukua mkopo? Mimi... La. Mimi husikia kuchukua mkopo benki ni kama kujitia kitanzi!"

"Tata, kujaribu ndiko kutenda. Mikopo imenisaidia sana kuimarisha biashara yangu. Ninatarajia kufungua duka kuu hivi karibuni. Matumizi yoyote ya pesa huhitaji bajeti. Bajeti humwongoza mtu kuwa na mpango murua wa namna ya kutumia pesa zake."

Tata alimkumbusha mwenzake, "Tofauti ni kuwa wewe ulisomea uwekezaji ila mimi maarifa yangu yanahusu ujenzi." "Nakubaliana nawe lakini si asilimia kwa mia. Mradi mtu awe na utaratibu wa kufanya biashara atafaulu. Pima uwezo wako wa kulipa mkopo unaochukua. Kumbuka kuna kodi ya kulipia biashara yako. Walipe mishahara waajiriwa wako inavyofaa tena kwa wakati. Wataiheshimu kazi yao. Watajitolea kutia bidii kazini ili wasije kuharibu mkate wao wa kila siku."

Tata alisikiliza ushauri wa Faulu kwa makini. Hatimaye aliungama, "Natambua makosa yangu. Siwalipi mishahara wafanyakazi wangu kwa wakati ufaao. Wengine wao wamekuwa wakiacha kazi kwenda kuajiriwa kwingineko. Zaidi ya hayo, sijakuwa nikilipa kodi ya biashara yangu inavyohitajika. Nikisikia maafisa wa utozaji ushuru wamo mjini kwa shughuli zao rasmi, mimi huagiza duka kufungwa mara moja hadi watakapoondoka."

"Tata, ndugu ni kufaana. Fanya biashara kwa njia halali na utafanikiwa. Nitakushika mkono inapobidi. Biashara huwa na changamoto zake ila tukishauriana mambo yatanyooka, "Faulu alitamatisha.

**Maswali:**

(a) Kwa nini Tata alimuamkua na kumshukuru Faulu?
(b) Nani aliyemwalika mwingine katika mjadala?
(c) Faulu na Tata wanazungumza kuhusu nini?
(d) Kwa nini biashara ya Faulu ilikua?
(e) Faulu na Tata walianzisha biashara zao lini?

**Shughuli ya 2:** Msamiati mpya katika kifungu cha mjadala

1. Tambua msamiati mpya uliotumiwa katika kifungu cha mjadala ulichokisoma.
2. Andika daftarini msamiati huo mpya ulioutambua.
3. Mkiwa katika kikundi, jadilini maana za msamiati huo kama ulivyotumika katika kifungu cha mjadala ulichokisoma.
4. Tumieni kamusi kuthibitisha maana za msamiati mlioutambua.

**Shughuli ya 3:** Habari za kifungu cha mjadala kwa ufupi

1. Andika sentensi moja moja kueleza ujumbe wa kila aya katika kifungu cha mjadala ulichokisoma.
2. Unganisha sentensi ulizoandika ili kueleza kwa usahihi ujumbe wa kifungu kwa aya moja.

**Shughuli ya 4:** Uchambuzi wa mitazamo katika kifungu cha mjadala

Ukiwa na mwenzako, jadilini:

1. Mfanano wa mawazo kati ya Faulu na Tata kuhusu biashara.
2. Tofauti za mawazo kati ya Faulu na Tata kuhusu biashara.

**Changamkia**

Je, wewe una maoni gani kuhusu mjadala wa Faulu na Tata wanavyosema kuhusu biashara? Jadili na mwenzako maoni mliyonayo.

### Tembea na majira

1. Tumia kifaa cha kidijitali kusikiliza au kusoma kuhusu mjadala unaoendelea.
2. Mweleze mwalimu kuhusu mjadala huo ili akupe maoni yake.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi maoni yako kuhusu mjadala wa Faulu na Tata uliousoma katika shughuli ya 1.

## C. KUANDIKA

### Insha ya maelekezo

### Kichocheo

Ni mambo gani unaweza kuandikia maelekezo?

**Shughuli ya 1:** Aina za insha za maelekezo

1. (a) Ukiwa na mwenzako someni maelekezo yafuatayo ya **A** na **B**:

(a) Hatua za A

(i) Fuata njia ya kuelekea Basu.

(ii) Hatua mia mbili hivi, utaona duka upande wa kulia.

(iii) Pinda kushoto hadi ufike kwenye daraja.

(iv) Vuka daraja na uendelee na safari hadi uone kibao ambacho kimeandikwa Shule ya Tia Fora.

(v) Fuata ishara ya kishale kwenye kibao. Hatua chache kutoka hapo utaona lango kuu la shule.

(b) Hatua za B

(i) Weka kadi yako kwenye mtambo wa kutoa pesa.

(ii) Chagua lugha ya mawasiliano.

(iii) Bonyeza nambari ya siri ya kadi yako.

(iv) Chagua huduma ya kutoa pesa.

(v) Bonyeza kiasi cha pesa unachotaka kutoa kwenye akaunti yako.

(vi) Chukua kadi yako kutoka kwenye mtambo.

(vii) Chukua pesa zinapotolewa kwenye mtambo.

(b) Mweleze mwenzako maelekezo ya **A** na **B** yanahusu nini.

2. Tajeni miktadha ambapo kila maelekezo hutumika.
3. Jadili na mwenzako unavyoweza kutumia hoja katika hatua za **A** au hatua za **B** kuandika insha ya maelekezo kwa kuipanga katika aya.

**Shabashi!**

Insha ya maelekezo huwa inalenga kumwongoza mtu namna ya kufanya jambo. Maelekezo yanalenga kumwongoza mtu hatua kwa hatua namna ya kutekeleza jambo. Mfano ni maelekezo ya kufua nguo.

**Shughuli ya 2:** Sifa za maelekezo kuhusu jinsi ya kuandika insha ya maelekezo

Mkiwa katika vikundi, jadilini sifa za insha ya maelekezo kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

1. mada



Kimeidhinishwa na KICD

2. usahihi wa habari
3. mpangilio wa maelezo katika maelekezo
4. lugha sahili
5. lugha inayoeleweka kwa urahisi
6. maelezo yanayotoka upande mmoja.

**Shughuli ya 3:** Mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo

Mkiwa wawiliwawili, shirikianeni:
1. Kuchagua mada mtakayoandikia insha ya maelekezo.
2. Kuandaa vidokezo mtakavyotumia kutoa maelekezo.
3. Kupanga vidokezo hivyo kwa mtiririko unaofaa.

**Shughuli ya 4:** Insha ya maelekezo kwa kuzingatia vipengele muhimu vya insha ya maelekezo

1. Andika insha ya maelekezo ukitumia vidokezo ulivyoviandaa katika Shughuli ya 3.
2. Zingatia vipengele kama vile: mada, usahihi wa habari, lugha sahili na maelekezo yaliyo wazi.
3. Wasilisha kwa mwalimu insha yako ya maelekezo ili aisahihishe.

**Changamkia**

1. Watolee wenzako darasani maelekezo ya kufika nyumbani kwenu kutoka shuleni kwenu.
2. Andika maelekezo hayo na kuyahifadhi kwenye potifolio.

**Tembea na majira**
1. Tumia kifaa cha kidijitali kupiga chapa insha ya maelekezo uliyoiandika ukizingatia maoni ya mwalimu.
2. Hifadhi insha yako kidijitali.

**Shirikisha mzazi au mlezi**

Msomee mzazi au mlezi wako maelekezo uliyoandika ya kufika nyumbani kwenu kutoka shuleni ili atoe maoni yake.

## D. SARUFI

### Ukubwa wa nomino

**Kichocheo**

Utatambuaje nomino katika hali ya ukubwa?

**Shughuli ya 1:** Nomino katika hali ya ukubwa katika matini

1. Hapo awali ulijifunza kuhusu ukubwa wa nomino. Jadili na mwenzako maana ya ukubwa wa nomino.
2. Ukiwa na mwenzako, tambueni nomino za hali ya ukubwa kutoka kwenye chati hii:

| | |
|---|---|
| jikoba | jishamba |
| jiko | jivu |
| ka | jicho |
| jijumba | jiatu |
| jisahani | jito |
| goma | jigari |

Chati ya nomino

3. Soma kifungu hiki:

Mzee Daima alipenda kuvaa jikofia jeusi. Alifuga nguruwe, mbuzi na jibwa jeupe. Mzee na familia yake waliishi karibu na jiji la Polea. Alipostaafu, aliendelea kutunza mali aliyokuwa nayo. Akiwa kazini, Mzee Daima alifuata wosia aliopewa na wakubwa wake. Walikuwa wakimhimiza kutumia pesa alizopata kwa makini. Kwa kweli Mzee aliwasikiza na kufanya walivyomshauri. Alitumia vizuri pesa alizopata.

Siku moja aliamua kupiga darubini ufanisi wake. Alianza kwa kufurahia jumba alimoishi. Jijumba hilo lilikuwa limesimama katikati ya jishamba lake. Mlikuwa na jito lililoteremka kwa madaha kupitia jishamba hilo. Jigari la Mzee Daima lilikuwa limeegeshwa katika jibanda lenye paa la chandarua. Lango la jibanda lilikuwa wazi. Mzee alisogea karibu na kapu lililojaa matunda. Alitoa matunda kadhaa na kuyatia kwenye jisinia. Alimwita mfanyakazi wake mmoja, "Memo, njoo." Memo alifika himahima. Mzee akashauri, "Yachukue matunda haya uyatie ndani ya jitungi lile. Yaoshe vizuri kisha uwaite wenzako waje tule pamoja."



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Maswali**:

(a) Tambua nomino zilizo katika hali ya ukubwa katika kifungu ulichokisoma.

(b) Andika daftarini nomino ulizozitambua.

(c) Mhusishe mwenzako kutambua na kuandika nomino katika hali ya ukubwa za vitu vinavyopatikana darasani.

## Shughuli ya 2: Viambishi vya ukubwa katika nomino

1. Chorea mstari viambishi vya hali ya ukubwa katika nomino zifuatazo:

| | Ukubwa |
|---|---|
| (a) | jitabu |
| (b) | jikalamu |
| (c) | jidirisha |
| (d) | jishamba |
| (e) | jimeza |

2. Umegundua nini kuhusu viambishi hivyo? Mweleze mwenzako.

## Shughuli ya 3: Kutumia nomino katika hali ya ukubwa

1. Ambatanisha nomino za hali ya wastani na hali ya ukubwa kwenye jedwali lifuatalo:

| | Wastani | Ukubwa |
|---|---|---|
| (a) | kalamu | jipira |
| (b) | kikombe | jitanda |
| (c) | chupa | jichupa |
| (d) | mtoto | jikombe |
| (e) | mpira | jikalamu |
| (f) | kitanda | jitoto |

2. Andika nomino zifuatazo katika hali ya ukubwa:

| | Wastani | Ukubwa |
|---|---|---|
| (a) | kisu | |
| (b) | kasha | |
| (c) | simu | |
| (d) | mtu | |
| (e) | mguu | |

3. Tunga sentensi ukitumia nomino ulizoandika katika hali ya ukubwa.

**Changamkia**

Mkiwa wawiliwawili, fanyeni mchezo ambapo mmoja akitaja nomino katika hali ya wastani mwenzake anaitaja katika hali ya ukubwa. Fanyeni hivi kwa zamu.

### Tembea na majira

Mkiwa wawiliwawili:

1. Tumieni kifaa cha kidijitali kuandika nomino mlizozitaja katika zoezi la changamkia.
2. Hifadhini nomino hizo kwenye faili ya kifaa cha kiditali ili mzirejelee mtakapohitaji kufanya hivyo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Msomee mzazi au mlezi wako nomino za hali ya wastani na za hali ukubwa ulizoandika daftarini.
2. Mwombe akupe maoni yake kuhusu kazi yako.

### Jumuika na jamii

1. Mwombe mzazi au mlezi akupe ruhusa kutembelea duka lililostawi karibu na nyumbani kwenu.
2. Jadiliana na mwenye duka kuhusu njia bora za uwekezaji na matumizi yafaayo ya pesa.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
| --- | --- |
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

### Tatua

Katika shule yako kumekuwa na mjadala kuhusu kiwango cha pesa ambazo mwanafunzi anafaa kupewa kwa matumizi yake. Ukiwa na wenzako katika kikundi, pendekeza kiwango cha pesa kinachofaa kwa kurejelea matumizi bora ya pesa.

# 15 MAADILI YA MTU BINAFSI

## A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Kusikiliza habari na kujibu

**Kichocheo**

Je, ni mambo gani yanayokuelekeza kuelewa suala muhimu katika habari unayosikiliza?

**Shughuli ya 1:** Masuala katika matini

1. Sikilizeni habari mtakayosomewa. Mwalimu atawaelekeza.
2. Mkiwa wawiliwawili, jibuni maswali yafuatayo:
   (a) Kisa cha mtoto kuokolewa kilitokea wapi?
   (b) Mtoto aliyeokolewa alikuwa amehatarisha maisha yake vipi?
   (c) Kwa nini ilikuwa ni ajabu kijana aliyetajwa katika habari kumwokoa mtoto?
   (d) Ni vipi vifaa vya kidijitali kwenye matini vilitumika kwa njia isiyofaa?
   (e) Ni nani anayeripoti habari hizi moja kwa moja?

**Shughuli ya 2:** Msamiati wa suala lengwa katika matini

Mkiwa katika kikundi:

1. Sikilizeni tena habari hiyo ikisomwa.
2. Andikeni maneno katika habari hii yanayoonyesha vitendo vya maadili.

**Shughuli ya 3:** Kutabiri yatakayotokea kutokana na vidokezo katika habari

Ukiwa na mwenzako, jibu maswali yafuatayo:

1. Uliposikiliza mwanzo wa habari ulidhani kijana aliyemwokoa mtoto angekuwa mtu wa aina gani?
2. Unafikiri wazazi au walezi wa mtoto huyo walikuwa wapi mtoto alipopanda kwenye paa la nyumba?
3. Unafikiri kungetokea nini kama mtoto asingeokolewa?
4. Unafikiri familia ya mtoto ilimshukuru vipi kijana aliyemwokoa mtoto wao?
5. Watu waliopiga picha na kuchukua video za mtoto akitaka kuanguka wanastahili adhabu gani?



KICD Kimeidhinishwa na KICD

**Shughuli ya 4:** Maana za msamiati wa suala lengwa kama ulivyotumiwa katika matini

1. Mkiwa katika kikundi:
   (a) Elezeni maana ya maneno mliyotambua katika shughuli ya 2 kama yalivyotumiwa katika habari.
   (b) Eleza maana za maneno yafuatayo yaliyotumika katika habari uliyosikiza:
      (i) kuwajibika
      (ii) ujasiri
      (iii) kupongeza
      (iv) maadili
      (v) amekodolea kifo macho.

**Changamkia**

Mkiwa katika kikundi, igizeni mtangazaji wa redio au televisheni akitangaza. Elezeni mambo muhimu yaliyotangazwa.

### Tembea na majira

Mkiwa katika kikundi sikilizeni habari kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu maadili. Tajeni masuala yanayoshughulikiwa katika habari hizo.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Ukiwa nyumbani, sikiliza habari za redio au televisheni kisha umweleze mzazi au mlezi habari hizo zilihusu nini.

## B. KUSOMA

### Ufupisho

### Kichocheo

1. Je, ni kwa nini watu hufupisha habari?
2. Ni mambo gani ambayo unazingatia unapoandika ufupisho?

**Shughuli ya 1:** Usahihi ujumbe wa aya za matini kwa sentensi mojamoja

1. Ukiwa na mwezako:
   (a) Someni matini hii.

Je, maadili ni nini? Dhana ya maadili hufasiriwa kwa njia tofauti na jamii tofauti. Kunazo jamii ambazo hufungamanisha maadili na dini. Kwao, ili mtu awe mwadilifu lazima afuate mafundisho ya dini. Katika jamii nyingine maadili huhusishwa na sheria za nchi. Mtu yeyote anayetii sheria hizi huonekana mwadilifu. Ufafanuzi huu wote unaonyesha kuwa mtu mwadilifu ni mtenda mema. Naye mtu ambaye ni mtovu wa maadili ni mtenda mabaya.

Hivi ni kusema kuwa maadili ni matendo mema. Maadili ya kibinafsi kwa upande mwingine ni mambo mema ambayo mtu hufanyia watu wengine kwa hiari. Matendo haya ya kujitolea mara nyingi huwa ni ya kupigiwa mfano. Mtu anapojitolea mhanga ili kuwaokoa wengine kwa mfano, tunasema ni mwadilifu. Matendo mengine ya kiadilifu ni kama vile wema, ukarimu, uaminifu, heshima, utiifu, kutenda haki, kuwajibika, kufanya usawa, kupenda amani na kuwa mzalendo.

Jamii huhimiza watu kuwa na maadili ya kibinafsi. Watu wanapotenda matendo yanayokiuka maadili huadhibiwa au kutengwa na wanajamii. Mwanafunzi anapokiuka maadili kwa mfano, hupewa onyo kali au adhabu kulingana na sheria za wizara ya elimu. Matendo yanayokiuka maadili ni kama vile wizi, uongo, ubaguzi, usaliti, kutowajibika, ubinafsi na madharau.

Maadili ya mtu binafsi humsaidia kuweza kuhusiana vizuri na watu wengine. Bila watu kuzingatia maadili, ulimwengu ungekuwa uwanja wa fujo. Maadili ya kibinafsi huwawezesha watu kuweka mipaka ifaayo wanapotangamana. Jambo hili huleta heshima baina ya watu. Heshima si utumwa, heshima ni hekima. Watu wanapoheshimiana huishi kwa amani na utulivu.

**Swali:**

(b) Elezeni kwa sentensi mojamoja ujumbe wa kila aya.

(c) Andikeni sentensi hizo kwenye madaftari yenu.

**Shughuli ya 2:** Usahihi ujumbe wa aya zote za matini kwa aya moja

Mkiwa kwenye kikundi:

1. Unganisheni sentensi mlizoandika katika swali la shughuli ya 1(c) ili kueleza kwa usahihi ujumbe wa matini nzima kwa aya moja.
2. Someni aya mliyoandika katika kikundi chenu ili wenzenu watoe maoni yao.

**Shughuli ya 3:** Ufupisho unaozingatia mtazamo wa matini ya kufupishwa

Chagua matini kwenye kitabu au mtandao usome. Andika daftarini ufupisho wa matini hiyo kwa kuzingatia yafuatayo:

1. wazo kuu katika matini
2. kuandika kwa ufupi bila kutoa ufafanuzi au mifano



Kimeidhinishwa na KICD

3. kuandika bila kuongeza mambo yasiyo kwenye matini
4. kuandika bila kuongeza mawazo yako au kutoa msimamo wako
5. kuzingatia mtiririko ufaao.

**Changamkia**

Mkiwa wawiliwawili, someni makala ya gazeti na kuyaandika kwa ufupi. Pateni ushauri wa mwalimu.

### Tembea na majira

Piga chapa ufupisho ulioandika wa makala kwa kutumia kifaa cha kidijitali. Wasambazie wenzako darasani ufupisho uliopiga chapa ili watoe maoni yao.

### Shirikisha mzazi au mlezi

1. Ukiwa nyumbani, sikiliza habari kwenye redio au televisheni.
2. Sikiliza pia muhtasari wa habari hizo.
3. Mpe mzazi au mlezi maoni yako kuhusu muhtasari huo wa habari.

## C. KUANDIKA

### Kuandika kidijitali

### Baruapepe

### Kichocheo

1. Je, unaweza kumwandikia rafiki yako baruapepe kumwambia nini?
2. Unazingatia mambo gani unapoandika baruapepe kwa rafiki yako?

**Shughuli ya 1:** Ujumbe unaoafiki baruapepe kwa rafiki

Mkiwa katika kikundi:

1. Jadilini kuhusu ujumbe ambao mnaweza kuandikia marafiki zenu katika baruapepe.
2. Nakilini hoja zenu kwenye madaftari.
3. Wasomeeni wenzenu darasani hoja zenu ili wazitolee maoni.

**Shughuli ya 2:** Vipengele vya kimuundo vya baruapepe kwa rafiki

Ukiwa na mwenzako:

1. Someni kielelezo cha baruapepe kwenye picha ya kipakatalishi inayofuata:



KICD Kimeidhinishwa na KICD




2. Jadilini vipengele vya kimuundo vya baruapepe vinavyojitokeza kwenye kielelezo mlichosoma.
3. Andikeni kwenye madaftari yenu sehemu za baruapepe mlizotambua.

**Shughuli ya 3:** Lugha inayofaa katika uandishi wa baruapepe kwa rafiki

Ukiwa na mwenzako, chagueni sifa zinazofaa kuzingatiwa katika uandishi wa baruapepe kwa rafiki. Wekeni alama ya √ na **x** pale inapofaa katika jedwali. Mfano umetolewa.

| Lugha inayofaa katika uandishi wa baruapepe ya kirafiki. | Alama √ au x |
|---|---|
| Lugha inayoeleweka kwa urahisi | √ |
| Lugha ya mafumbo | |
| Lugha yenye sentensi fupifupi | |

| | |
|---|---|
| Lugha ya heshima | |
| Lugha yenye utata wa maana | |
| Lugha ya kishairi | |
| Lugha sanifu | |

**Shughuli ya 4:** Baruapepe kwa rafiki kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao

1. Tumia kifaa cha kidijitali kifaacho ili kuingia katika mtandao wa intaneti kama vile *yahoo* au *gmail*. Mwalimu atakuelekeza.
2. Chukulia kuwa wewe ni Luka kisha ujibu baruapepe ya Kabiru katika shughuli ya 2. Zingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao.

Fuata hatua zifuatazo unapomwandikia baruapepe:

(a) Jiandae kuandika kwa kujadili na mwenzako vidokezo vya baruapepe utakayoandika.
(b) Andika anwani ya unayemtumia barua kwenye sehemu ya anwani.
(c) Andika mada ya barua.
(d) Andika barua yenyewe katika sehemu ya kuandikia ujumbe uliotoletewa.
(e) Zingatia lugha ifaayo.
(f) Soma na mwenzako baruapepe uliyoandika ili aitolee maoni.
(g) Tumia maoni ya mwenzako kusahihisha au kuboresha barua yako kabla ya kuituma.
(h) Mwonyeshe mwalimu barua uliyoiandika ili akupe maoni yake kabla ya kuituma.
(i) Tuma barua yako kwa kubonyeza penye ishara ya kutuma.
(j) Angalia kama imetumwa. Utaona ujumbe wa kukufahamisha kuwa imetumwa.

**Changamkia**

Jizoeshe kuwasiliana na marafiki wako kwa kuwaandikia baruapepe upatapo fursa.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mweleze mzazi au mlezi kuhusu baruapepe uliyomwandikia Kabiru ukimjibu ili akupe maoni yake.

## D. SARUFI

### Usemi halisi na usemi wa taarifa

### Kichocheo

1. Je, wewe huwasilisha ujumbe kwa usemi gani?

2. Je, ni mambo gani unayozingatia wakati wa kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa?

**Shughuli ya 1:** Maana ya usemi halisi na usemi wa taarifa

Mkiwa katika kikundi, someni sentensi zifuatazo:

### Usemi halisi

1. (a) Tina alisema, "Tunafaa kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo."
   (b) Kiranja alisema, "Ni muhimu kudumisha nidhamu hapa shuleni."
   (c) "Nitawapelekea watoto mayatima nguo mpya," mfanyabiashara alisema.
   (d) "Leo tutasafisha soko," mfanyakazi alisema.
   (e) Rafiki yangu alisema, "Kwetu tunashirikiana kufanya kazi za nyumbani."

### Usemi wa taarifa

1. (a) Tina alisema kuwa walifaa kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo.
   (b) Kiranja alisema kuwa ilikuwa muhimu kudumisha nidhamu pale shuleni.
   (c) Mfanyabiashara alisema kwamba angewapelekea watoto mayatima nguo mpya.
   (d) Mfanyakazi alisema kuwa siku hiyo wangesafisha soko.
   (e) Rafiki yake alisema kwamba kwao walishirikiana kufanya kazi za nyumbani.
2. Tambueni sentensi zilizo na maneno yaliyotoka kinywani mwa msemaji moja kwa moja.
3. Tambueni sentensi za habari iliyoripotiwa baada ya kusemwa na mtu mwingine.

**Shabashi!**

Nimegundua kuwa usemi halisi ni maneno yaliyotoka kinywani mwa msemaji moja kwa moja. Katika usemi wa taarifa mtu huwa anaripoti maneno ya mtu mwingine.

**Shughuli ya 2:** Kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa

Mkiwa katika kikundi, someni tena sentensi za shughuli ya 1 na kujibu maswali haya:

1. Tambueni tofauti zilizoko kati ya sentensi za usemi halisi na zile za usemi wa taarifa katika shughuli ya 1.
2. Tumieni jedwali lifuatalo kujadili mabadiliko zaidi kati ya sentensi za usemi halisi na zile za usemi wa taarifa.



KICD Kimeidhinishwa na KICD

| | Usemi halisi | Usemi wa taarifa |
|---|---|---|
| i. | Ni maneno yaliyosemwa moja kwa moja. | Ni maneno yaliyoripotiwa. |
| ii. | Hutumia alama za kunukuu " " kufungia maneno ya msemaji. | Hautumii alama za kunukuu " ". |
| iii. | 'Leo' hubadilika kuwa | siku hiyo. |
| iv. | 'Kesho' hubadilika kuwa | siku itakayofuata, keshoye. |
| v. | 'Jana' hubadilika kuwa | siku iliyotangulia. |
| vi. | 'Sasa' hubadilika kuwa | wakati huo. |
| vii. | 'Hapa' hubadilika kuwa | hapo au pale. |
| viii. | 'Kwangu' hubadilika kuwa | kwake. |
| ix. | 'Kwetu' hubadilika kuwa | kwao. |
| x. | Wakati 'na' hubadilika kuwa | -likuwa, -ki. |
| xi. | Wakati 'ta' hubadilika kuwa | -nge-. |
| xii. | Hali 'me' hubadilika na kuwa | -likuwa -me. |

**Shughuli ya 3:** Usemi halisi na usemi wa taarifa ifaavyo

Mkiwa wawiliwawili:

1. Badilisheni sentensi zifuatazo kutoka usemi halisi hadi usemi wa taarifa.
   (a) "Mimi ninawaamini wafanyakazi katika kiwanda changu," alitamka mkurugenzi.
   (b) Rais alisema, "Serikali yangu inakabiliana na mafisadi wote."
   (c) "Tutatii sheria za nchi," mfungwa alisema.
   (d) Chifu alisema, "Nimefurahishwa na ushirikiano wenu katika kijiji hiki."
   (e) Mwalimu mkuu alisema, "Kila mwanafunzi lazima adumishe usafi wa mwili na mazingira."
2. Badilisheni sentensi zifuatazo kutoka usemi wa taarifa hadi usemi halisi.
   (a) Bawabu aliwaambia wanafunzi wamwonyeshe karatasi ya idhini ya kutoka nje.
   (b) Mgeni alisema kuwa alishukuru kwa makaribisho ya siku hiyo.
   (c) Mwanafunzi alimwomba mwalimu msamaha kwa kuchelewa kufika shuleni.
   (d) Mfanyabiashara alisema amejitolea kumnunulia mgonjwa dawa.


KICD Kimeidhinishwa na KICD

(e) Waziri aliwapongeza wachezaji wa Kenya kwa kushinda medali katika michezo ya mwaka uliotangulia.

3. Mkiwa katika kikundi:
   (a) Tungeni sentensi tano za usemi halisi.
   (b) Badilisheni sentensi mlizotunga ziwe katika usemi wa taarifa.

**Changamkia**

Mkiwa watatuwatatu, chezeni mchezo ambapo mtu mmoja anasema jambo na wa pili anamripotia wa tatu jambo lililosemwa. Fanyeni hivyo kwa zamu.

### Tembea na majira

Tumia kifaa cha kidijitali kuandika sentensi mlizotunga katika shughuli ya 3 swali la 3.

### Shirikisha mzazi au mlezi

Mwonyeshe mzazi au mlezi wako sentensi ulizotunga.

### Tafakuri

Nakili jedwali hili daftarini kisha ujaze maelezo mafupi kuhusu kila mada.

| Mada | Mambo niliyoweza kufanya katika mada hizi |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | |
| Kusoma | |
| Kuandika | |
| Sarufi | |

**Tatua**

Umeokota bahasha yenye pesa katika uwanja wa shule. Wenzako darasani wanakushawishi mfiche na kuzitumia pesa hizo. Wewe kama mwanafunzi mwenye maadili utafanya nini?



KICD Kimeidhinishwa na KICD